MITUME

LEO

Paul Galligan

MITUME

LEO

Paul Galligan

HESHIMA /SHUKRANI

Yesu alisema *"**Awapokeaye ninyi* **[mitume]** *anipokea mimi; naye anipokeaye mimi, ampokea* **[Baba]** *aliyenituma"* **Mathayo 10:40**

Kitabu hiki kimetolewa kwenu **"*watakatifu wote, katika Kristo Yesu, walio kwa mataifa na mashemazi"* (Wafilipi 1:1)** na kwa mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu ambao Kristo amepeana kanisani katika kupaa kwake **(Waefeso 4:11).**

"*Ambaye katika yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani katika jina lake"* Warumi 1:5

Ninakipatiana kitabu hiki kwenu kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza; na kwa kuwaadibisha katika haki. Hapana kwa njia yoyoye ambapo nafikiria kitabu hiki kinatoshana na biblia kwa wakati wowote, lakini ninaamini mafundisho ambayo ninawaletea ni mafundisho nimepokea kutoka kwa Bwana kama vile nimejifundisha neno katika Roho wa hekima na ufunuo. Nimepata msaada kutokwa kwa wahuduma wengine wa Kristo ambao maandishi yao na mafundisho yao nimeyapokea. Ninaamini kwamba mafundisho yangu hayajakamilika kwa sababu neno la Mungu linazidi kufunguka.

Ninatia nguvu maneno ya mtume Yuda **"*ili niwaonye kwamba mwiishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu* (aya 3).**

YALIYOMO

Dibaji: **Kufikia tume** 5

Utangulizi: **Lengo ni kanisa lililokomaa** 8

Sura 1 **Mabadiriko ya uongozi –** 14
Kutoka kwa Shebna hadi kwa Eliakimu

Sura 2 **Kazi Iliyokamilika ya Yesu aliye Mtume** 24

Sura 3 **Kwa nini twahitaji mitume leo** 34

Sura 4 **Mitume ni akina baba** 44

Sura 5 **Mtume ni nini? ….**..... 51

Sura 6 **Tambia za huduma ya kitume** 63

Sura 7 **Fundisho la kitume ni nini?** 75

Hitimisho: **Ufunuo wa kitume** 90

Kiambatisho i **Baraza la kitume** 92

DIBAJI

Haikuwa mpaka mwezi wa tisa 1997 ambapo kwanza nilitafakari kwa kumaanisha kuhusu huduma ya mtume kama uhakika wa leo. Kwa wakati huo nilikuwa nikitumika kama mfanyi kazi wa baraza wa dini, nikiwa na karama ya mwalimu kwa mwili wa Kristo. Nilikuwa naelewa kuhusu mwondoko wa kiunabii kuanzia kati ya miaka ya tisini na themanini, wakati nabii aliyeitwa Paul Cain alishuhudia katika kongamano ya John Wimber Australia. Jambo moja ambalo wengi katika harakati ya kiunabii walianguka ilikuwa kutabiri urejesho wa mitume. Mimi binafsi sikuhusika katika harakati ya kinabii na hakika niliona mazao 'yasio mema' yakitoka katika shule za kiunabii hapa Australia. Hata hivyo, nilikuwa na msingi kiasi katika huduma tano za **Waefeso 4:11** pasina ufahamu kamili na pia kutofahamu huduma ya mtume.

Historia ya huduma yangu

Kabla ya huduma ya waalimu nilikuwa nikitumika kutoka mwaka 1994-97, nilikuwa nimetumika miaka sita kama mchungaji, na kabla ya hayo, miaka minne kama msimamizi wa shule ya kikristo. Kwa yote nilifurahia kazi kwa kweli ya uchungaji, kufanya kazi kwa bidii, kumpendeza Bwana, nikiwa muhuduma mwema kama vile nilivyoweza, lakini sikutoshereka ndani yangu. Kutoka mwaka wa 1985-1990 nilitumika kama mchungaji wa kuheshimiwa / honorary chaplain katika chuo hapa, nikifanya kazi ya uinjilisti nikiona mazao kidogo lakini nikijua kwamba sina karama ya uinjilisti, ijapo kwa undani nilitamani kuwa na ufanisi katika kuwafikia waliopotea.

Kwa sababu zaidi ya upeo katika utangulizi huu, niliachana na huduma mwisho wa mwaka 1990. Kwa miaka miwili na nusu nilizunguka kwa jangwa ya ajabu, nikitumika kwa masafa kutoka kwa kupaka manyumba rangi na kuwa mshauri wa kimataifa na pia kurudi katika chuo kwa masomo ya ziada. Mda huo wote nilijua nimeitwa kuwa muhuduma wa Yesu Kristo lakini nilijihisi sijahitimu na sikuwa na wazo jinsi Mungu angenirejesha kwa huduma, lakini alifanya hivyo. Katikakati ya mwaka wa 1993 nilianza huduma ya kufundisha katika kanisa la mahali pamoja ambapo nilikuwa nikihudhuria. Kwa wakati huo, niliomba kazi ya usimamizi na kanisa hilo. Kwa sababu nilifikiri kwamba hiyo ndio njia ya kurejerea huduma kwa maana kwa sasa nilikuwa nikijua Mungu ananiita.

Walioomba nafasi ya usimamizi walichunjwa mpaka wawili na kisha maamuzi yakanipendekeza. Hata hivyo, muhuduma mkuu akanifikia na kunijuza waliofikiana na sababu yangu kupendekezwa. Sifa zangu na wasifu zilikuwa zakufaa na nikaamuliwa kama aliyefaa na mwenye ombi aliyefaulu, lakini baraza likaamua kwamba sio mwito wangu, kwa maana nimeitwa 'kuhubiri na kufundisha neno la Mungu'. Licha ya kuweka tumaini la kutarajia kuipata kazi hiyo, sikuvunjika moyo, lakini kwa hakika nilihimizika kwa maana nilithibitishiwa katika mwito na karama ya kuhubiri na kufundisha. Bwana asifiwe!

Mwalimu wa neno

Baadaye mwisho wa mwaka wa 1993 nilipewa kazi na kanisa hilo hilo kama mwalimu wa neno na jukumu la kufikia kijiji. Nikaingia katika huduma ya kusisimua na kuridhisha kwa miaka minne iliyofuata. Hii ilihusisha kutoa maafundisho katika washa ya maombi na uinjiristi. Nilihusika katika kuandika vitabu vya kufundisha katika semina hizo. Huduma hii ya kufundisha ilipokelewa na makanisa mengi katika mwili wa Kristo. Katika mwaka wa 1996 nilikuwa

nikisafiri na kikundi cha wahuduma wanafunzi na Bwana alikuwa ametupa upako mzito wa kufundisha neno, kufanyiza neno kazi na kuachilia upako wa Roho Mtakatifu.
Kufikia kipindi cha pili cha mwaka wa 1997, dini ambayo ni ya kanisa ambalo nilikuwa nayo na ambayo nilikuwa nikuhudumia ilifanya makosa makubwa katika hali ya mashoga ambao hawajatubu kuwa washiriki na wasiwatenge watu kama hao katika huduma iliyo wekwa wakfu. Katika kanisa letu la pahali pamoja, mchungaji kiongozi na wengine wengi walikuwa wakistaafu na kuiacha dini hiyo. Huu ndio wakati ambapo Mungu alianza kunizungumzia kuhusu huduma ya mtume. Nilipewa baadhi ya kanda nisikize, na katika kanda moja ndugu aliongea kuhusu huduma ya mtume. Hii ilihuisha moyo wangu na Bwana akanifunulia kwamba huu ndio wito wangu. Kisha akaongoza kikundi kidogo chetu kuomba kustaafu na kuanza kupanga huduma mpya. 'Revival Ministries Australia' ndio yalikuwa matokeo. Bwana alifunua hilo jina na akadhihilisha na tukazindua huduma mnamo Januari 1998.

Nilimwona Bwana.

Wakati ulio pangwa wa kuzindua ulipokaribia, mimi binafsi nikaanza kusikia jukumu la kuongoza huduma na nilikuwa mwoga na mwenye hofu katika kutenda haya. Mpaka wakati huu, kwa miaka kumi na minne ya huduma wakati wote katika huduma tatu tofauti za kanisa, nilikuwa kila wakati nikiwa katika jukumu la kusaidia mtu ama Yule anaye muwakilisha mtu mwingine. Sasa ikawa mimi ndimi nitakayekuwa kiongozi! Nilikuwa sijaonyesha uoga wangu kwa yeyote, bali Bwana alijua. Niliamka saa saba usiku asubuhi kumwona Bwana Yesu akisimama mwisho wa kitanda changu, nilipo mtazama, akaachilia ujasiri ndani yangu kwenye moyo wangu, kwa njia ya kuonekana. Huu ulikuwa ni wakati wa ajabu sana na ujuzi wa kutosahaulika: 'Nilimwona Bwana' na akanihudumia kwa njia ya kuyabadilisha maisha, kuniandaa na kunitia nguvu kwa kazi ya huduma ambayo alikuwa akiniita ndani yake. Bila kupenda kupoteza uhakika wa nguvu wa kumwona Bwana, niliamka kutoka kwa kitanda changu na nikaenda chumba changu cha kusomea, nikaasha sitima na nikachukua Biblia yangu. Bila kumwona Bwana Yesu, nilijua kwamba yupo pamoja nami na kwa wazi akanielekeza kufungua **Joshua 1**. Ikawa ni kama alinisomea aya za kwanza tisa, ambazo zilihimiza 'uwe hodari na moyo wa ushujaa'.

Kutumwa kuwa mtume

Kwa wakati ambapo nilikuwa sifikirii kwa ufahamu juu ya huduma ya mtume lakini nilijua, tangu wakati huo, huku ndiko kutumwa kwangu na Yesu niwe mtume, moja ya jambo kuu katika kusoma, **Joshua 1:1-9,** ni neno ***"urithi".*** Wakati ambapo katika mazingira Mungu anamwambia Joshua kwamba ataigawanyisha nchi kama urithi kwa watu wa Mungu, nilijua kwamba wajibu wangu ingekuwa katika "kutumia neno la kweli kwa halali**" (2 Tim 2:15).** Nguvu zangu katika huduma wakati huo ulikuwa ni wa mwalimu na sasa mimi ni mtume ambaye anafundisha, na Bwana ameniwezesha kurejesha 'urithi' kwa watu wake. Sikujua kwamwe nitaandika kitabu, **"kutembea katika urithi wetu"** [2004].

Shule ya Tirano

Sehemu ya maono ambayo Bwana alitia ndani ya moyo wangu kutoka siku hizo za kwanza ya kupanga huduma na kuizindua Revival ministries Australia, iliimarishwa kwa wakati wake, kituo cha mafundisho / maandalizi. Tuliandika kuhusu haya na tukawa na maono ya na kwamba siku moja Mungu atatuwezesha kuwa na muundo wa kisasa wa "shule ya Tirano" (**Mdo 19:9-10).** Baada ya safari ya umoja wa Myanmar (Iliyojulikana kama Burma) mapema 1999,

tuliimarisha shule ya kujifunza ya wiki sita Juni/julai ya mwaka huo, tukitumia vifaa vya kukondeshwa. Kwa wakati huo huduma ilikuwa na msingi katika nyumba nyingi tofauti. Tulikuwa tumefanya shule moja ya muda kule Myanmar na tukawa tumepelekwa kuhudumu kwa miji tofauti, haswa kwa kanisa za nyumbani ambazo zilikuwa zimeimarishwa na wanafunzi ambao walikuwa wamejiandaa kwa huduma. Mungu alikuwa akinionyesha kuhusu muundo wa kanisa la kitume katika matendo: Shule za muda za kuwaandaa wanafunzi kwa huduma na kuimarisha kwa kanisa la nyumbani. Mwisho wa 2000, mwana biashara mmoja, ambaye ni sehemu ya kikundi cha huduma, alipata kununua jengo katikati mwa mji, la Revival ministries Australia. Kutoka wakati huo tuna mahali petu pa msingi kituo cha mafundisho ya kitume. Tumekuwa tukifanya shule za wiki mbili, mara mbili kwa mwaka kutoka mwaka wa 2001. Mnamo mwezi wa nne mpaka juni 2006, tulikuwa na miezi mitatu ya mafunzo ya kimataifa tukiwa na wajumbe kumi na wanane wakihudhuria kutoka kwa mataifa saba tofauti. Mungu ametuwezesha ‘kuleta upya’ maono ya kwanza ambayo alituonyesha katika maandiko.

Miaka yote kuanzia mwanzo wa 1998, nimewezeshwa na Bwana kuandika mafundisho kadhaa/ vitabu za mafundisho. Nilikuwa nimejifunza kuandika vijitabu nikiwa katika huduma ya zamani, kwa hivyo nilitumia ujuzi ule. Miongozo iliyojitokeza iliongoza ramani ya safari yetu katika ufunuo wa utume ambao tunatembea ndani yake leo. Kitabu hiki ‘mitume leo’ inahusisha mafundisho kutoka kwa vitabu hizo, ikileta pamoja fundisho na ufahamu wa mitume leo, ikihusisha utangulizi wa fundisho la kitume. Hata hivyo, yaliyomo yote na nyenzo, yanaleta pamoja halalisho, imepanuliwa na kusawasishwa katika nuru ya ufunuo unaoendelea na masomo na matemdo kutoka kwa ujuzi tulioupata.

UTANGULIZI

Lengo ni kanisa timilifu

Yesu Kristo anajitayarishia ***"kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa"*** **Waefeso 5:27.** Analiandaa kanisa lake ***"kwa lulitakasa na kulisafisha kwa maji katika neno"*** **Waefeso 5:26**. Hili ndilo kanisa ambalo limekuwa na kufikia ukomavu likifikia ***"Umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufikia cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*** **Waefeso 4:13**. Hili ndilo kanisa ambalo ***"limeufikia ukomavu",*** likiisha kuwekewa msingi wa ***"kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa imani kwa Mungu, mafundisho ya mabatizo na kuwekewa mikono, mafundisho ya kufufuliwa wafu na wa hukumu ya milele"*** **Waebrania 6:1-2.**

Hili ndilo kanisa ambalo Yesu anajiletea;
kanisa lenye utukufu ambalo halina ila wala kunyanzi wala lolote
kama hayo, kanisa takatifu bila mawaa.

Tunaenenda katika utimilifu (ukomavu) na hayo tutafanya ***"Mungu akitujalia***"**(Wabrania 6:3*)*** na Mungu atatujalia tu wakati kanisa lina msingi imara. Yesu Kristo ndiye huo "msingi": **"*msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuweka"* (1wakorintho 3:10-11);** yesu Kristo ndiye ***"mwamba huo"*** **(1 Wakorintho 10:4).** Kila mmoja wetu anahitaji kujenga maisha yetu katika Kristo juu ya msingi wa kuzitubia kazi zisizo na uhai na imani kwa Mungu, ubatizo wa maji mengi na kuwekewa mikono kupokea Roho Mtakatifu, na kutembea katika ufunuo wa kufahamu ukweli wa uhakika wa fundisho la kufufufuliwa wafu na hukumu ya milele. Hivyo hivyo kanisa lahitaji kujengwa juu ya msingi wa Kristo, mitume na manabii zikiwa ndizo huduma za msingi **(Waefeso 2:20)** ambayo inapatia kanisa msingi mwema wa kukua na kuendelea na kuwa mtu mtimilifu wa **Waefeso 4:13.**

Kanisa lililokomaa limewakilishwa na wanawali watano katika **Mathayo 25:1-13**. Kanisa hili lenye utukufu litapakwa na Roho Mtakatifu; taa zake zitaangaza vyema katika dunia hii ya giza ambayo imejipatiana kwa mpinga –Kristo, kanisa hili limejiandaa kwa kuja kwake Bwana!

Hili ndilo kanisa ambalo linafahamu siri ya mwili wa Kristo **(Waefeso 3:6)** ambalo limejengwa na Wayahudi na Mataifa, pamoja, kama warithi pamoja. Yesu mwenyewe ***"aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake, akafanya amani"*** **Waefeso 2:14-16.**

Hili ndilo kanisa ambalo lilipokea hekima ya ndani ya Mungu ***"ambayo Mungu aliazimu tangu milele kwa utukufu wetu"*** **(1 Kor 2:6-7).** Ni kanisa lote kwa jumla, likitembea katika ukomavu, ambalo linapokea "nia ya Kristo" **(aya 16).**

Kuna mafundisho Mengi katika maandiko kuhusu kanisa lililokomaa, kanisa ambalo litakua na kuufikia utimilifu kwa maana hilo ndilo kusudi la Mungu kwetu. Paulo anasema kazi yake kuu kama muhuduma ilikuwa ni kumhubiri Kristo, ***"tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo"*** **Wakolosai 1:28.**

Yesu Kristo Alitoa Vyote Kwa Ajili Ya Kanisa Lake

Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alipitia hali ya kunyenyekeshwa hata akafanyika kuwa mwanadamu, ***"Alijifanya hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba"*** **(Wafilipi 2:7-8),** ili alipate kanisa**.** ***"Yeye ndiye mwokozi wa mwili"*** **Waefeso 5:23.** Zaidi, ***"alishuka mpaka shehemu zilizo chini ya nchi***" **Waefeso 4:8-10** [mpaka kuzimu yenyewe **1Petro 3:18-19]** na kisha akapaa juu, aliteka mateka. Kupitia kushuka kwake na kupaa kwake, Yesu alijipatia ushindi wa nguvu ambao ulibadilisha historia milele, kama matokeo ya kazi yake ya ukombozi, alipata kutoa kwa kanisa lake huduma tano ya mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji na mwalimu. Bila huduma hizi kaanisa haliwezi kuufikia ukomavu na utimilifu. Wajibu wa huduma tano ni wa namna nyingi katika kuleta mwili ulio komaa wa Kristo ***"Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"*** **Waefeso 4:16.**

Huu ndio mwili uliokomaa ambao BWANA analeta duniani,
na anafanya haya kwa njia ya kuachilia karama ya mtume,
nabii, mwinjilisti, mchungaji na mwalimu

Mungu analijenga kanisa

Yesu alisema katika **Mathayo 16:18** ***"Nitalijenga kanisa langu***". Mungu anajenga nyumba [hekalu]. Hekalu inajengwa na mawe yaliyo hai; sisi watakatifu, ndio mawe yaliyo hai. Tunajengwa kuwa nyumba ya roho ya Mungu kudumu **(Waefeso 2:22)** ambayo ndani yake sisi ni makuhani, kuzitoa dhabihu za kiroho kwa Mungu **(1Peter 2:5).**
Jengo linajengwa juu ya msingi ambao kwanza ni mitume, kisha manabii (**Waefeso 2:20).** Hizi ndizo huduma za kimsingi ambazo zinashikilia jengo lote, zikiunganisha kanisa kwa mwamba wa msingi 'ambaye ni Kristo' (**1Wakorintho 3:11).** Bila mitume na manabii jengo halitajengeka kulingana na muundo wa kibiblia. Ni mafundisho ya mitume, ambayo kanisa inatakiwa kujitoa kwake **(Mdo 2:42).**

Mitume wanaweka msingi,
wanaangalia jengo la kanisa
na kulikamilisha.

Zerubabeli ni mfano wa Mtume

Kufahamu huduma ya mtume tunahitaji kutazama huduma ya Zerubabeli ambaye alikuwa gavana wa Yerusalemu. Alikuwa na jukumu la kujenga upya hekalu ya Mungu wakati wa urejesho kutoka uhamisho wa Babeli.

"Mikono yake Zerubabeli imeiweka misingi ya nyumba hii" **Zekaria 4:9.** Zerubabeli alikuwa ameuweka msingi, kwa hivyo ni mfano wa mtume; anajenga nyumba ya Mungu, aya inaendelea kusema ***"na mikono yake ndiyo itakayoimaliza kisha mtajua kwamba BWANA wa majeshi amenituma kwenu".*** Hii inaongea kuhusu huduma ya mtume. Wakati Mungu anamuinua mtume, anampatia mtume picha kubwa ya jinsi ya kujenga kanisa. Paulo anasema alikuwa ***"mjenzi mkuu"*** **(1Wakorintho 3:10);** kwamba alikuwa amepewa na Mungu mipango ya kujenga kanisa. Paulo anafunua mipango hiyo mingi kwetu katika kitabu cha Waefeso.

Kujengwa kwa Nguvu za Roho

Katika **Zekaria 4:6**, malaika analeta utafsiri wa maono ya BWANA kwa Zerubabeli ***"si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema BWANA wa majeshi".*** Hili ndilo neno la BWANA kwa mtu aliye jukumishwa na kazi ya kujenga upya Hekalu. Kazi yaweza tu kufanywa kupitia upako wa Roho Mtakatifu. Neno la BWANA kwa Zerubabeli ni, 'si kwa uwezo wa kibinadamu au nguvu; ni kwa Roho Mtakatifu, kwa ufunuo, kwa upako wa Mungu, ya kuwa kanisa lake litajengeka'.

Kujengwa kwa Neema

Zerubabeli alikuwa ameagizwa na Mungu, kupitia nabii Hagai na nabii Zekaria, kujenga nyumba ya Mungu. Huyu ndiye mjenzi, mtume ambaye ataweka msingi, kuangalia kuta zikijengwa na kuleta jiwe la kumalizia kwa sauti ya ***"neema, neema juu yake!"*** **aya7.** Inajengwa na neema kupitia imani***, "ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu"*** **Waefeso 2:8-9.** Ni kwa "***neema na utume***" **Warumi 1:5** ambapo kanisa litajengwa, mungu anafunua mpango wake mkubwa wa jinsi kanisa inapaswa kujengwa katika siku hizi za mwisho na neema imepatianwa kwa mitume ili wajulishe muundo na kuangalia kujengwa kwa kanisa.

Kumbuka kwamba Paulo anajiita mjenzi mwenye hekima **1Wakorintho 3:10** na haswa Yesu alitangaza kwa Petro **Mathayo 16:18-19** kwamba atakuwa jiwe la msingi katika kanisa ambalo Yesu anajenga juu ya 'Mwamba'. Kama mtume aliye msingi, alizipokea funguo za ufalme wa mbinguni. Petro anafunua zaidi kuhusu mpango mkuu wa kulijenga kanisa katika nyaraka **1Petro 2:4-10.** Kama Paulo, Petro Mtume alikuwa mjenzi mwenye hekima.

Inajengwa kwa Imani

"Nani wewe, Ee mlima mkubwa? Mbele ya Zerubabeli utakuwa nchi tembarare!" **Zekaria 4:7.** Neno la Mungu linasema kwa Zerubabeli ya kuwa mlima wa upinzani utashindwa. Unabii huu unaonyesha ya kwamba mitume wana uweza wa kukabiliana na upinzani kwa makusudi ya Mungu. Katika **2Wakorintho 10:3-6** Paulo anatuambia "***silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uweza katika Mungu hata kuangusha ngome; tukiangusha mawazo na kila kitu kilicho inuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo".*** Hivi ndivyo mlima wa upinzani wa dini unakabilianwa nao katika kanisa la kitume.

Isaya 40:4, ikizungumza kuhusu huduma inayokuja ya Yohana mbatizaji, anasema ***"Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa",*** kunyosha njia za BWANA. Yohana mbatizaji 'aliteremshaje milima'? ilikuwa ni huduma ya neno, akitangaza mambo ambayo Mungu alikuwa amemfunulia. Hii ni sawa na ***"Nguvu juu ya mataifa"*** ambayo Yesu aliahidi kwa wale watakao shinda (**Ufunuo 2:26-27).** Alisema kwamba kanisa litapokea nguvu zile zile ambazo alikuwa amepokea kutoka kwa Baba, ***"kuwatawala (kuchunga) kwa fimbo ya chuma".*** Yesu alisema ***"Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake"*** **Mariko 11:23.** Hii ni imani katika matendo.

Iwe na imani ya Mungu nawe utahamisha milima.
Hii ndio imani itakayoijenga kanisa.

Yesu ndiye Mtume wa Mungu, akijenga kanisa

Mikono yake yule aliyeweka msingi ndio itakayomalizia. Yesu Kristo ndiye aliyeweka msingi wa kanisa la Mungu! Yesu Kristo ndiye atakayekamilisha kazi hiyo! Yesu atafanyaje mambo hayo? Kupitia mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu ambao amepatiana (**Waefeso 4:11).** Wakati kanisa litakamilika kila mmoja atasema, 'hakika hili ni kanisa la Mungu aliye hai'. 'Litazame kanisa hili la ajabu, ambalo Mungu ameinua kutoka kwa kila taifa, kutoka kwa kila lugha na ulimi, kila kikundi cha watu, ili kuonyesha wazi utukufu wa Mungu katika Kristo'.

Urejesho wa Kitume Umeanza.

"***Maana ni nani aliyedharau siku ya mambo madogo***?" **Zekaria 4:10a.** Ni lazima kazi ianzie na mIsingi, kwa mambo madogo! Ufufuo wa Welsh wa 1904-5 ilikoma pakubwa kwa sababu ya ukosefu wa huduma tano na haswa mitume na manabii, lakini pia wachungaji wa kweli na walimu walikuwa wachache. Katika matokeo ya ufufuo wa Welsh kulikuwa na muondoko wa kitume na kinabii miongoni mwa wandugu ambao walitambua ya kwamba huduma hizi mbili zilikuwa za muhimu kwa kunjenga kanisa. Muondoko uliinuka ambao ulitabua mitume na manabii na huduma zingine tano. Muondoko huu uko Australia leo kama dini ya kipentekoste ambao bado wanatabua huduma zote tano. Muondoko huu ulikuwa kama utangulizi na ilijulikana tu na watu wachache.

Kuzaliwa kwa muondoko wa kitume na kinabii kulifanyika wakati wa muondoko ilioitwa mvua ya mwisho/ Latter Rain ambao ulianza 1948 ukiwa na ufufuo ambao Bwana alirejesha mengi ya hekima ya ndani na mafundisho ya maandiko. Ilikuwa ni katika ufufuo wa mvua ya mwisho/Latter Rain ambako wandugu walianza kufahamu kuhusu Hema ya Musa, Sikukuu za Israeli, mpangilio wa Melkizedeki, kuwekea mikono ili kupokea Roho Mtakatifu [kabla ya haya wapentekosti walikuwa na mikutano ya 'kungojea' Roho Mtakatifu aje]. Ukweli mwingine na huduma zilirejeshwa kwa wakati huo. Ni ya kushangaza kutambua muondoko wa kwanza wa kitume na kiunabii kutoka kwa ufufuo wa Welsh ulitupilia muondoko wa mvua yaMwisho/ Latter Rain kama zilivyofanya dini zingine za Kipentekosti.

Wakati tulianzisha huduma ya Revival ya Australia mwaka wa 1998, kitabu cha kwanza tulicho ongozwa kuandika kilikuwa ni 'Misingi ya Imani Yetu' ikiwa na msingi katika kanuni sita za elimu ya kwanza ya kutoka **Waebrania 6:1-2**. Kwa miaka mitano huduma ya Revival Ministries Australia 1998-2002, tulikuwa tukifanya kazi majifichoni, tukiweka misingi na kujifundisha kuhusu huduma ya mitume. Tulijua vyema kabisa kwamba hapa ndipo Mungu alikuwa nasi na tulijifundisha 'kutodharau siku za mambo madogo'.

Timazi ni Neno la Mungu

***"Nao watafurahi, nao wataiona timazi katika mkono wa Zerubabeli; naam, hizi saba ndizo macho ya BWANA"* Zakaria 4:10b.** Hizo saba zinawakilisha Roho saba za Mungu. Macho saba ni Roho saba za Mungu (**Ufunuo 5:6).** Yesu ndiye Yule aliyepakwa ambaye alipokea Roho Mtakatifu bila kipimo (**Yohana 3:34).** Roho Mtakatifu wa Mungu hufurahi akiiona timazi mkononi mwa Zerubabeli. Timazi hutumika kupima unyofu wa ukuta. Ni jambo la kupima. Tunatakiwa kupima sawa na neno la Mungu. **Timazi ni neno la Mungu mikononi mwa Zerubabeli, mfano wa mtume.** Kanisa la nyakati za mwisho latakiwa kupima sawa na neno la Mungu. Wakati watu wa Mungu wameruhusu wahukumiwe na neno la Mungu, na kukaa sawa na maandiko, na wasipungukiwe na utukufu wa Mungu kutokana na dhambi, kisha Roho

Mtakatifu anafurahia na upako unaongezeka, wakati watu wa Mungu wanaruhusu jengo la kanisa lao na mazoea kuhukumiwa na neno na kukaa sawa na maandiko, kisha kanisa lenye utukufu litaonekana.

Huduma ya Nabii

Nabii anafanya kazi pamoja na mtume, akiweka nguvu misingi na kuweka kanisa kwenye njia. Huduma ya nabii ni kuelekeza kanisa katika utimilifu. Nabii huleta ufunuo wa neno laMungu kanisani. Wakati huduma ya mtume na ya nabii zinainuliwa na kufanya kazi pamoja, kama mfano wa Paulo na Sila **(Mdo 15:40),** kisha kanisa litakuwa na msingi wa nguvu na kuweza kuenda katika utimilifu. Ni kwa mitume na manabii ambapo Mungu anapatiana ufunuo wa siri kupitia Roho (**Waefeso 3:5)**.

Huduma za mitume na manabii ni za msingi; ni huduma hizi ambazo zinaleta kanisa katika utimilifu kupitia kuhubiri ***"Siri za Kristo zisizo julikana, kufanya wote kuona ushirika wa siri"*** **Waefeso 3:8-9.**

Huduma ya mwinjilisti.

Mwinjilisti huenda nje kwa machimbo ya dunia ili achimbe mawe mapya ambayo yanafaa kujenga ukuta wa kanisa (**1Petro 2:5).** Mwinjilisti ni huduma ya hadhara. Kwa mfano, mji wote wa Samaria alimsikiza mahubiri ya Filipo (**Mdo 8).** Mwinjilisti huchimbua mawe ambayo yanafanyika mawe yaliyo hai kwa kuzaliwa mara ya pili, na anawaleta kanisani. Ukuta wa kanisa unaitwa 'ukuta wa wokovu' (**Isaiya 26:1).** Mwinjilisti anahubiri wokovu na nafsi zinaokolewa, na kisha yanajengwa kuwa kuta za hekalu.

Elewa kwamba Filipo kama mwinjilisti, aliyebatizwa! Petro na Paulo wote walifanya kazi ya uinjilisti wakihubiri injili katika maeneo ambayo yalikuwa hayajasikia. Wote Petro na Paulo waliamuru ubatizo mara moja pia na kuhudumu ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa waumini wapya. Kwahitajika kuwa na kurejelea unjilisti wa kimaandiko ukitiliwa mkaso juu ya ubatizo wa maji kama jambo muhimu, mwitikio unaohitajika kwa wale ambao wameshawishika kupitia neno.

Huduma ya Mchungaji

Mchungaji anachukuwa mawe mapya anaanza kuyachonga, na kuilainisha na kuiunganisha. Hatua ya kwanza muhimu kwa mchungaji ni kuwalea waumini wapya kwa kuweka misingi ya imani yetu (**Waebrania 6:1-2).** Waumini wapya wanahitaji kunyweshwa na maziwa ya neno ili waweze kukua katika wokovu (**1 Petro 2:20).** Huduma ya pili ya muhimu ya mchungaji ni ***"kuwalisha wana kondoo"*** **Yohana 21:17.** Mchungaji ni lazima awe na uweza wa kufundisha neno kwa wote watoto katika Kristo na waumini wote, 'kufanya wanafunzi' **Mathayo 28:19-20.** Hatua ya tatu muhimu ni kuchunga watu wa Mungu ambayo inahusisha kuangalia nafsi za watu, wakipatiana mwelekeo na ulinzi. Paulo aliwaambia wazee katika Efeso ***"lisheni kanisa lake Mungu"*** **Mdo 20:28** na Petro anasema, ***"Lichungeni kundi la Mungu lililoko kwenu, na kulisimamia"*** **1Petro 5:2.**

Mchungaji analeta urejesho kwa watu wa Mungu. Aya ya kwanza ya zaburi ya mchungaji inaelezea haya vyema: ***"Bwana ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu"*** **Zaburi 23:1.** Mchungaji anapatiana kwa wakristo mahitaji ya neno la Mungu na upendo wa Mungu. ***"Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, Kando ya maji ya utulivu huniongoza"*** **aya 2.** Mchungaji hulisha kondoona chakula chema; anatafuta pahali ambapo pana usalama kwa waumini, ambapo wanaweza kukuzwa na kukua. Wanahuishwa nafsi zao!

Huduma ya mwalimu

Huduma ya mwlimu ni kuweka msingi kwa waumini wote katika neno: kufundisha neno ***"Amri juu ya amri, amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni, huku kidogo na huko kidogo"*** **Isaya 28:10.** Mwalimu analisha neno kwa wakristo ambao wamelelewa ili mwanafunzi ahitimu kwa chakula kigumu na anahimizwa aenende katika ukomavu. Mpaka sasa, waalimu wengi wamepata tu maelezo ya huduma yao katika vyeo na shule za Biblia. Hata hivyo, huo sio muundo wa Biblia. Maandiko yako wazi: Waalimu ni wale ambao wamepewa karama na Kristo na karama ya kupaa ya waalimu na wale ambao wamefundishwa vizuri na mitume, na wamefikia kujua ufunuo wa siri.

Katika SHILOH, hapa Toowoomba, tumeona ukweli huu ukifunguka. Mmoja wa wachungaji wetu amejipatiana kwa fundisho la mitume, akipokea kikamilifu ufunuo wa mitume, na sasa anafanya kazi kwa nguvu katika huduma ya mwalimu. Katika mwaka 2006, tunayo shule ya Biblia ambayo inafanyika mara moja kwa juma, ikiwa na idadi ya kama wanafunzi kumi wakihudhuria. Wandugu hawa wanaandaliwa kufundisha neno. Hii inafanyika kwa kuwafundisha neno na kuwapatia nafasi ya kufundisha neno. .

Katika siku hizi za urejesho, waalimu wanainuliwa katika makanisa ya pahali pamoja na kufundisha kwa neno kunakuwa na kuongezeka.

Huduma Zikifanya Kazi Kwa Mpangilio

Mtume na nabii wanaweka msingi: msingi imara katika neno la Mungu. Katika msingi huo mwinjilisti anatiwa nguvu kuondoka na kwenda ulimwenguni na kuhubiri wokovu na nafsi nyingi zinaokoka. Mwinjilisti anajua kwamba anaweza leta muumini mpya kwa kanisa lenye nguvu na limewekwa msingi mwema, ambapo pana kikundi cha wachungaji/wazee ili kumkuza mkristo mpya. Mkristo mpya anatakiwa alishwe na 'maziwa ya neno' na aimarishwe kikamilifu katika elimu ya kwanza ya msingi wa imani. Kisha mwalimu [mara kwa mara mmoja wa wazee wa mahali pamoja] anawaimarisha waumini katika neno, akiwapa nidhamu katika neno, wanafunzi katika neno la Mungu kwa kuwafundisha amri na maagizo ya neno la Mungu. Watakatifu kisha wako tayari kufundishwa na mitume na manabii ili waweze kuinuliwa katika huduma. Huduma inahusisha kuwa na uwezo wa kufundisha neno, wakihudumu karama za Roho Mtakatifu na kutembea katika upako na nguvu za Mungu katika kuwahudumia wengine. Kizazi kipya cha wahuduma kinaweza kuinuliwa cha mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu.

Tunaporudia na kurejesha muundo wa kitume wazi kama ilivyoko katika maandiko, tunafahamu kuwa wazee wa kanisa la pahali pamoja [kanisa la mahali pamoja likiwa kanisa la mji wote] wamewekwa na mitume. Hivyo wazee [wachungaji na waalimu] wana uhusiano wa kuendelea na mtume. Wakati kanisa linafanya kazi kulingana na muundo wa maandiko, huduma zote tano zinapata nafasi na kuonekana zikitenda kazi ya huduma ambayo inafanya kazi ***"kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe, hata na sisi sote tutakapofikia umoja wa imani, na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufikia kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*** **Waefeso 4:12-13.**

Sura ya kwanza

MABADIRIKO YA UONGOZI

Uongozi na utawala wa kanisa uko mikononi mwa mitume, kwa jumla,
na mikononi mwa wazee katika miji ya mahali pamoja na jiji.

Mamlaka ambayo mitume wamepewa haitegemei mwanadamu lakini
Kristo mwenyewe ambaye anaita na kuchagua mitume

Eliakimu ni mfano wa mtume, aliyeinuliwa na Mungu na kiongozi
aliye na uwezo wa kutimiza mwito na kusudi la Mungu.

Ni Mungu huita na kuchagua mitume na viongozi wa kitume kwa kanisa lake.
"Mungu ameweka kanisani mwake kwanza mitume"

Kiongozi mpya - **Isaya 22:21**
"Nami nitamvika vazi lako,
nitamtia nguvu kwa mshipi wako,
nami nitamkabidhi yeye mamlaka yako;
naye atakuwa baba kwa wenyeji wa Yerusalemu"

Kutoka kwa shebna mpaka Eliakimu- Isaya 22-15-25

"Bwana, BWANA wa majeshi, asema hivi, Haya! Enenda kwa huyu mtunza hazina, yaani Shebna, aliye juu ya nyumba, ukamwambie, Unafanyaje hapa? Nawe una nani hapa? hata ukachimba kaburi hapa; ukamchimbia kaburi huko juu, na kumchongea makao katika jabali!

Tazama, BWANA atakutupa kwa nguvu, kama mtu mwenye nguvu; naam, atakuzonga-zonga. Hakika atakukuja na kukutupa kama mpira, mpaka nchi iliyo mbali; huko utakufa, na magari ya utukufu wako yatakuwa kuko huko, ewe uliye aibu ya nyumba ya bwana wako. Nami nitakusuma na kukutoa katika mahali pako, naye atakuzusha utoke hapa usimamapo.

Na itakuwa katika siku ile nitamwita mtumishi wangu Eliakimu, mwana wa Hilkia; nami nitamvika vazi lako, nitamtia nguvu kwa mshipi wako, nami nitamkabidhi yeye mamlaka yako; naye atakuwa baba wa wenyeji wa Yerusalemu, na kwa nyumba ya Yuda.

Na ufunguo wa nyumba ya Daudi nitauweka begani mwake; yeye atafungua wala hapana atakayefunga; naye atafunga wala hapana atakayefungua. Nami nitamkaza kama msumari mahali palipo imara; naye atakuwa kiti cha utukufu kwa nyumba ya baba yake.

Nao wataangika juu yake utukufu wote wa nyumba ya baba yake; wazao wake na watoto wao, kila chombo kidogo tangu vyombo vya vikombe hata vyombo vya makopo vyote pia.

Katika siku ile, asema BWANA wa majeshi, ule msumari uliokaswa katika mahali palipo imara utalegea; nao utakatwa na kuanguka chini na ule mzigo uliokuwa juu yake utakatiliwa mbali; maana BWANA amesema haya."

Ni Nani Aliye na Ufunguo wa Daudi?

Katika **Ufunuo 3:7** Bwana wetu Yesu anatangulizwa kama "***aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye".*** Katika barua hii, Yesu anaongea na kanisa la Filadelfia na anafunua kwa kanisa kwamba ameweka ***"Mlango uliofunguka mbele yao".*** Yesu anatambulika katika ***Waebrania 3:1*** kama ***"Mtume … wa maungamo yetu".*** Ni yesu aliye mtume aliye na ufunguo wa Daudi. Katika siku hizi za urejesho, kanisa mara tena linaitwa ***"kumtafakari mtume Yesu Kristo";*** Jambo ambalo kanisa halijafanya kwa kumaanisha kwa pengine miaka 1,800. Yesu, kama mtume anashika ufunguo wa Daudi na kumbuka ya kuwa Yesu alipatiana "***funguo za ufalme wa Mbiguni"*** kwa Petro akiisha kutambua kwamba Petro alikuwa ni jiwe la msingi katika kulijenga kanisa la Yesu Kristo (**Mathayo 16:18-19).** Petro alikuwa ameitwa na Yesu kuwa mtume awali (**Mathayo 10).** Yesu, mtume, alimpa Petro, mtume na mwakilishi wa mitume wote, funguo za ufalme akiwapa mitume mamlaka ya kufungua na kufunga. Kwa hivyo mitume wameshika ufunguo wa Daudi kama walivyopewa na Yesu.

Tangia kati ya mwaka wa 1990 Bwana Yesu amekuwa akirejesha huduma ya mitume kwa kanisa lake duniani kote. Ilianza kwa njia ndogo na kubwa isio julikana lakini, kwa mwaka wa 2006, neno 'mtume' na kutafakari uhakika na athari ya huduma hii zinakuwa na ushawishi hata kama, kwa wengine, ina msimamo wa kukataliwa wazi. Katikakati ya haya, Bwana anaathiri mabadiriko ya uongozi, '**kutoka kwa Shebna mpaka kwa Eliakimu'.**

Uongozi wa Zamani

Kanisa kwa jumla limeongozwa na mchungaji mkuu, na maaskofu, na wahuduma waliofaulu, na baadhi ya wainjilisti ambao wametambulika, hata na wengine wenye karama za uponyaji au miujiza. Baadhi ya wahuduma hawa waliofaulu wanaonekana wakiwa kama wakurugenzi wakuu, wakiwa na biashara na ujuzi wa mjasiriamali, kuliko mtume wa agano jipya. Makanisa ya kidini kwa jumla yanaongozwa na wasimamizi walio mbali na watendaji wa serikali, mara nyingi wakiwa na mambo yao ya kibinafsi na ageda za kisiasa ambazo zinapingana na injili na neno la Mungu. Katika Australia, mojayapo ya dini kubwa, katika hali ya idadi ya washiriki, inaongozwa na msimamizi wa serikali ambaye anafanya kazi kanisani ambaye anaunga mashoga kwa kuwekwa wakfu katika huduma. Kwa miaka, yeye na wengine walikuwa wafanya siasa na ujuzi katika dini hiyo kwa kiwango ambapo 2003, katika kongamano la miaka elfu tatu ya dini hiyo kirasmi walikubali kuwekwa wakfu kwa wahuduma washoga na sasa baadhi ya parokia zao wana wale wanaoitwa wahuduma walio na wenzao wa jinsia moja katika makazi. Wakati huu ni jambo imekithiri, inaonyesha msiba ambao inaweza inaweza kusababisha kanisa kuondoka kutoka kwa na kukana huduma ya mitume na kutopokea fundisho la mitume.

Uongozi wa Agano Jipya

Makanisa mengi hayaongei kuhusu uongozi wa kibiblia kama ilivyoonyeshwa katika Agano Jipya. Viongozi wakuu waanapata makosa ya wachungaji wakuu au wamewekwa wakfu kama maaskofu au wakitumia mamlaka juu ya kanisa moja ama nyingi. Bodi na komitii za dini wanatawala dini, wakitangaza kwamba hao ndio wenye mamlaka ya kanisa. Hakuna mamlaka ya kibiblia kama hayo ya utawala.

Katika Agano jipya –
Uongozi na serekari iko mikononi mwa mitume kijumla,
na miongoni mwa wazee, katika miji ya mahali pamoja na jiji.

Katika kuleta ufahamu wa mwili wa Kristo,(**1Wakorintho12:12-30)** Paulo anaeleza wazi ***"Mungu ameweka wengine kanisani, wa kwanza mitume, wa pili manabii na watatu waalimu, baada ya hayo…"*****aya 28.** Hii ni kauli wazi ya mpangilio wa vile Mungu ameweka uongozi kanisani. Mapema sana baada ya kuandika Maandiko ya Agano jipya, kanisa lililo inuka lilianza kuona maasikofu wakiinuka katika utawala juu ya kanisa la mji na maaskofu hao wakichukua kwa nguvu mamlaka ya mitume, wakaanza kuweka mamlaka ya uongozi wa kiaskofu kanisani.

Ukoloni wa Kanisa

Ukoloni wa kibeberu umeisha kuonekana duniani. Sasa kuna mataifa mengi huru na kujitawala ambayo zamani yalikuwa yakitawaliwa na mataifa ya uingereza yenye nguvu, hata hivyo dini za kikristo zimeendelea kutoka kwa ukoloni kanisani pakiwa na vikundi vingi vya kidini wakienda kwa mji au eneo na kupanda kanisa tofauti. Vikundi hivi vinapata ushindi kwa mafundisho yao na mazoezi iliyo pangwa ya kidini, wakijiimarisha peke yao kando na vikundi vingine vya kanisa ambao wameimarika katika mji ule. Kwa jumla makao makuu ya vikundi hivi vya dini yako na ofisi kubwa katika mji wa mbali. Kama matokeo kuna migawanyiko ya taasisi zilizo gawanyika katika mwili wa Kristo. Wakristo wengi hawajalidhika kamwe na mipangilio hii na Mungu kamwe hajalidhika. Ni wakati wa mabadiriko kanisani upande wa uongozi na utawala. Hapo ndipo umoja wa kweli utakuwa hakika kwa kila mji na eneo.

Urejesho wa Uongozi wa Kibiblia na Utawala.

Bwana anapoleta urejesho wa uongozi wa kibiblia na Mungu mara tena anaweka ***"kwanza mitume, pili manabii, tatu waalimu",*** kanisa linarejeshwa kwa muundo wa Agano jipya.

Mamlaka yanayopatianwa kwa mitume haimtegemei mtu
lakini inamtegemea Kristo Mwenyewe
ambaye anaita na kuchagua mitume.

Kama mitume wanapoinuliwa na Kristo Anawapatia mamlaka kama yalivyowakilishwa katika 'unguo wa Daudi'. Mamlaka hayo, yanapita, kuchukua nafasi ya 'maasikofu' ikiwakilisha uchaguzi wa watu kwa uongozi wa kanisa.

Mabadiliko ya uongozi ni jambo la muhimu sana katika maisha ya kanisa leo. Bila urejesho wa uongozi wa kibiblia na utawala, kanisa litaendelea kukosa mwito wake. Limeitwa kuhubiri ufalme wa Mungu na mambo kuhusu Yesu (**Mdo 8:12),** ikiadhiri ulimwengu, ikileta mavuno mengi ya nafsi katika ufame wa Mungu, na kuliandaa kanisa kwa kurudi kwa Bwana na kuwaandaa watakatifu kutawala na kutamalaki na kristo duniani.

Mungu anaanzisha mabadiliko ya Uongozi

Katika **Isaya 22:15-25,** kuna mafundisho yenye maelekezo mengi kuhusu mabadiliko ya uongozi kutoka kwa Shebna, mtunza hazina, mpaka kwa Eliakimu, mtu ambaye Mungu aliinua. Shebna ni mfano wa kiongozi aliyeinuliwa na watu kama msimamizi aliyechaguliwa katika ofisi, askofu aliyewekwa wakfu na watu, mchungaji mkuu kiongozi ambaye anachukua ofisi na kadhalika.

Eliakimu ni mfano wa mtume,
Aliyeinuliwa na Mungu, aliyechaguliwa na Mungu
na aliyepakwa na Mungu, Na hivyo kiongozi mwenye uwezo
wa kutimiza wito na kusudi la Mungu.

Mungu Anaongea na Uongozi wa Kanisa

Kama unafanya kazi katika huduma na uongozi wa kanisa leo, unajua wito na uchaguzi wa Mungu, au umewekwa tu katika huduma na uongozi kwa kuchaguliwa na watu? Kama hii ya nyuma ni ya kweli, haimaanishi kwamba 'haujaitwa na Mungu' lakini inamaanisha kwamba umeupatiana wito wako kwa njia na taasisi za wanadamu, na kama matokeo , hautaachiliwa katika moja wapo wa huduma tano ambayo Kristo alikuwekea.

"Bwana, BWANA wa majeshi, asema hivi, Haya! enenda kwa huyu mtunza hazina, yaani, Shebna, aliye juu ya nyumba, ukamwambie" **Isaya 22:15**. Neno la Bwana linamjia nabii Isaya na linazungumziwa Shebna ambaye ni mtunza hazina juu ya nyumba. Nyumba ambayo inazungumziwa ni nyumba ya Yuda na miji wa Yerusalemu. Huyu mtu alikuwa ndiye msimamizi mkuu wakati wa utawala wa Mfalme Hezekia. Alikuwa amechaguliwa na watu [na mfalme] na Mungu alikuwa hajafurahia uongozi wake au na mazao ya huduma yake, msimamizi ni nani katika kanisa la leo? Mzimamizi amewakilishwa na 'askofu' au msimamizi, au 'mchungaji', mtu anayesimamia kanisa la mahali pamoja, mtu aliye kiongozi wa makanisa, katika mji ama katika dini yote. Msimamizi huyu katika mazingira ya wakati huu amewekwa wakfu na watu, kuchaguliwa na watu ama, kwa hali zingine, amejichagua.

Mungu Anahukumu Kazi za Uongozi wa Kanisa

"Unafanyaje hapa? nawe una nini hapa? hata ukachimba kaburi hapa; ukamchimbia kaburi huko juu, na kumchongea makao katika jabali!" **Isaya 22:16.** Bwana anauliza maswali mawili, 'wewe ni nani?' Na 'wewe una nini hapa?' Msimamizi anawajibika kwa Mungu kwa yale ambayo amekuwa akitenda. Mungu anasema kwa huyu msimamizi, 'umekuwa ukijijengea kitu, ukijifanyia jina, ili ukumbukwe utakapokufa'. Badala yakuwa msimamizi ukiangalia nyumba ya Mungu, amekuwa akijijengea kitu. Wakati mwingine tumeona mjengo maridadi mpya wa kituo cha kuabudia cha kanisa la mahali pamoja ukiwa na vifaa vyote kwa sababu ya starehe ya wanaoabudu; au tunaona kiongozi mkuu akikua kifedtha akijipatia mali nyingi za kibinafsi. Wakati maagizo ya kuihubiri injili kwa kila kiumbe (**Mariko 16:15-16),** na kueneda kwa mataifa yote na kufanya wanafunzi (**Mathayo 28:19-20)** imepuuzwa.

Kuna mifano mingi ya haya kutoka Europa iliopita. Makanisa mengi makubwa, yaliyo jengwa na watu, wakati mwingi ikichukua mwingo mingi kujengwa ukiwaghalimu watu maisha yao, ni minara ya watu, shelli tupu, kaburi! Watu wengi wanatembelea maeneo haya lakini hawakutani na Mungu; wanafurahia tu michoro na kazi ambayo inawapa watu sifa. Mijengo kama hiyo ilijengwa na 'wasimamizi' [maaskofu] ambao walitakiwa kuwa waangalizi na wakilichunga kundi la Bwana nyumba ya Mungu, hivyo ni kuyajenga maisha ya watu kujua na kuangaza utukufu wa Kristo, lakini wamejikwaa na kutazama kazi zao, nyumba zao 'wenyewe' wakitafuta kujijengea jina wenyewe, hata jina ambalo litabaki baada ya hao kutoweka.

Mungu Huhukumu Uongozi wa Kanisa.

"Tazama, BWANA atakutupa kwa nguvu, kama mtu mwenye nguvu; naam, atakuzonga-zonga. Hakika atakukuja na kukutupa kama mpira, mpaka nchi iliyo mbali; huko utakufu, na magari ya utukufu wako yatakuwa kuko huko, ewe uliye aibu ya nyumba ya Bwana wako" **Isaya 22:17-18.** Mungu anasema yakuwa 'mambo' ambayo huyu msimamizi amejikusanyia yataondolewa. Msimamizi atayapoteza maisha yake. Mambo ambayo msimamizi amejenga yatakuwa hakika mambo ya aibu na haitaleta utukufu kwa bwana. Yesu alituonya, ***"tukipenda kuyaweka maisha tutayapoteza".*** Paulo alisema kuna vyombo[wahuduma], ***"vingine vina heshima, vingine havina"*** **2Timotheo 2:20.**

Msimamizi huyu alifanya makosa kujaribu kujijengea kitu. Mungu alikiita kaburi, ambayo ni mahali pa kuzika. Hivyo ndivyo Mungu anafikiri kuhusu kazi zetu. Wengi siku ya leo wanaufwata mtindo wa msimamizi Shebna. Wanamtumikia Bwana, chakusikitisha wanadhania Mungu ni mkuu! Wanajenga Kathedral; wanaendesha magari ya kifahari katika mataifa ya dunia ya tatu, maaskofi wa kipentekosti wanavaa shati za langi ya zambarau za maaskofu wa kirumi na mtu anabaki amedwaa: 'wako wapi mitume?' 'lipo wapi kanisa ambalo Yesu anajenga?'
"Nami nitakusukuma na kukutoa katika mahali pako, naye atakushusha utoke hapo usimamapo" **Isaya 22:19**. Mungu atamtoa huyu msimamizi kutoka kwa ofisi, kwa sababu mambo ambayo amekuwa akitenda hayampendezi Mungu. Ni Mungu ainuaye na ni Mungu azushaye.

Kutakuwa na Mabadiliko ya Uongozi

"Na itakuwa katika siku ile nitamwita mtumishi wangu Eliakimu, Mwana wa Hilkia" **Isaya 22:20.** Eliakimu inamaanisha 'Mungu wa kuinua', Hilkia inamaanisha 'sehemu ya [Yahweh/BWANA]'. Mungu anainua uongozi mpya: Mungu ansema, ***"nitaita"*** Mungu anasema 'nitamuinua ambaye nimechagua- sehemu Yangu'.

Ni mungu huita na kuinua mitume
Na uongozi wa kitume kwa kanisa lake-
"Mungu ameweka kanisani wa kwanza mitume"

Mabadiliko ya uongozi inafanyika. Mtindo wa uongozi wa kale ambayo imekuwa ikijijengea nyumba inaangushwa, inawekwa kando. Mungu anawainua ambao wataliinua Jina Lake duniani. Siku inakuja, na siku imefika, ambapo Mungu anaita watumishi wake – wale ambao atakaowainua wawe viongozi kwa kanisa lake.

Sauli, Chaguo la Watu – Daudi, Chaguo la Mungu

Katika **1Samueli 8:10,** Sauli ameinuliwa kwa mapenzi ya watu awe mfalme wao. Yeye ni kama msimamizi wa taifa la Mungu, Israeli. Lakini akaonyesha kwamba hawezi kutegemewa; alikubaliana; alikataa kutii maelekezo ya Mungu; alichagua kufanya mambo kwa njia yake. Alikuwa akihofu watu, ambayo matokeo yake ilikuwa kutoa sadaka ambazo hazikukubaliwa (**1Samweli 13).** Mungu alimbadilisha Sauli na yule wa chaguo lake, Daudi. Mabadiliko kutoka kwa Sauli mpaka kwa Daudi ni sawa na mabadiliko ya uongozi katika **1saya 22.** Mungu anaondoa watu ambao hawamtii na kuweka watu wale amechagua, ambao watatii neno lake na kutimiza mapenzi yake.

Kiongozi Mpya

"Nami nitamvika vazi lako, nitamtia nguvu kwa mshipi wako, nami nitamkabidhi yeye mamlaka yako; naye atakuwa baba kwa wenyeji wa Yerusalemu na kwa nyumba ya Yuda" **Isaya 22:21.** Kuna mambo manne ya kuelewa kutoka kwa aya hii: kuvikwa na vazi, kutiwa nguvu na mshipi, kupokea kuwajibika mikononi, na kuwa baba kwa wenyeji wa Yerusalemu.

Kuvikwa Vazi

Kiongozi mpya atakuwa amevikwa vazi. Hii ni nguo ambayo inatambulisha kiongozi aliyechaguliwa. Yakobo alimtambua mwanawe Yusufu, kama mwana spesheli aliyechaguliwa kwa kumwekea juu yake ***"kanzu ndefu"*** **Mwanzo 37:3.** Wakati 'mwana mpotevu' alirudi kwa baba yake, baba alimpokea kama mtoto wake na akasema ***"leteni vazi lililo bora, mkamvike***"

Luka 15:22. Vazi linamtabulisha mwana kama mwenyeji, na kuwa mmoja pamoja na, Baba. Ni ya kupendeza ya kwamba maasikofu katika kukua kwa 'kanisa', kwa jumla wameenda kwa njia ya kujivika na mavazi ya kidini yaliyo tengenezwa na wanadamu ambayo inaleta uvuto kwa ofisi nje, lakini hawajajua upako wa Kristo ambao unafunika.

Kuna **vazi mpya** ambalo linakuja kanisani; sio tena vazi la msimamizi/ maaskofu, sio tena vazi la dini au idara, lakini vazi ni vazi la Yesu mwenyewe. Hii inakuja kwa Yule ambaye Mungu amemweka! Yesu ndiye Yule ambaye Mungu amemweka. Kristo ndiye kichwa cha kanisa na hakuna mwingine. Watakatifu wote ni washiriki wa mwili na wakati kanisa liko katika mpangilio wa kitume [likiongozwa na mitume] kisha vazi la Kristo na upako ni wazi na inafanya kazi.

Eliakimu ni mfano wa Kristo, lakini pia ni mfano wa kiongozi wa kitume ambaye Mungu anainua siku hizi za mwisho. Mungu anaweka vazi hili lake juu ya uongozi mpya, ambao ataliandaa kanisa kwa **kivuli cha utukufu** ambao Mungu ameahidi ***"juu ya makao yote ya mlima Sayuni, na juu ya makusanyiko yake"*** **Isaya 4:5**. Mungu ameahidi kwamba kanisa la siku za mwisho litafunikwa kabisa na utukufu wake "***wingu na moshi wakati wa mchana, na mwangaza wa miali ya moto wakati wa usiku"*** **Isaya 4:5.** Ni kanisa la siku za mwisho, ambalo limewekwa na kufanya kazi katika mpangilio wa kitume, ambalo litavikwa na Mungu katika Kristo.

Hata Yesu alipowafundisha wale thenashara ambao alichagua kuwa mitume, na baadaye Roho Mtakatifu akainua kizazi kipya cha mitume katika Agano Jipya ikianzi kwa Paulo na Banaba katika **Mdo.13**, kwa hivyo Mungu leo anainua kizazi kipya cha mitume ambao wataongoza kanisa siku hizi za mwisho. Huu ndio uongozi mpya!

Kutiwa nguvu na mshipi

Mungu atamtia kiongozi mpya nguvu kwa mshipi. Huu ni mshipi wa kweli **Waefeso 6:14. Yohana 17:17** inasema ***"neno lako ndiyo kweli".*** Petro anatuambia ***"vifungeni viuno vya nia yenu"*** **1Petro 1:13.** Viuno vinafungwa na mshipi. Ni nia zetu ambazo zinatakiwa kutiwa nguvu kwa mshipi wa kweli. Tunafanya haya kwa kuwa na neno la Mungu ndani yetu, na kwa kuamini yale neno la Mungu linasema. Mitume huja na kivuli cha Bwana Yesu Kristo na mamlaka na uhuru ya kunena neno la kweli, sio kwa kudhibitiwa na kuwekewa vikwazo na mwanadamu. Mitume wanatangaza ***"kusudi lote la Mungu"*** **Mdo 20:27.**

Petro alisema baada ya kuchaguliwa kwa wale mashemazi wa kwanza katika **Mdo 6:4,** ya kuwa mitume wanatakiwa ***"kujipatiana daima kwa maombi na huduma ya neno***" matokeo ya uongozi wa huduma ya kitume ikifanya kazi kama ilivyo nakiliwa katika **Mdo 6,** ilikuwa ***"Neno la Mungu likaenea; na idadi ya wanafunzi ikazidi katika Yerusalemu; jamii kubwa ya Wayahudi wakatii ile imani"*** **aya 7.** Ni ya muhimu mshipi wa kweli kuwekwa juu ya wale ambao Mungu anainua ili kuwe na urejesho kamili wa neno na kusudi la Mungu katika siku zetu.

Kuweka Uwajibikaji Kwa Mkono

Uwajibikaji unawekwa mkononi mwa kiongozi mpya. Mkono unawakilisha mamlaka na pia ni kwa mkono ambapo kazi inafanyika, ukiongea kuhusu karama. Mungu anasema atachukua uwajibikaji kutoka kwa kiongozi aliyeko na apatiane mikononi mwa Yule anainua. Katika **Kutoka 28:41**[NASB] kuna maneno mawili ya Kiebrania { SC#4390 kujaza na 3027 mkono] imetafsiriwa 'kuweka wakfu/kusimika' ikimaanisha 'kujaza mkono', Mungu atapatiana mamlaka yake kwa wale ambao anajua watamtii. Mamlaka ambayo msimamizi alikuwa nayo [hivyo ni, uongozi wa zamani] unapatianwa na Mungu kwa mtume [uongozi mpaya]. ni Mungu huinuwa

uongozi, anawatuma na kuwaweka wakfu kwa kuwatia mamlaka na uweza kwa kuwapa karama ili kuifanya kazi.

Baba kwa Wenyeji wa Yerusalemu

Ambaye Mungu anainua atakuwa 'baba', sio tena msimamizi lakini baba. Kuna mabadiliko ambayo yanatendeka hapa: viongozi wa kanisa hawatakuwa tena wasimamizi au waangalizi [maaskofu]; watakuwa akina baba, mitume, waliochaguliwa na Mungu sio wanadamu, mtume inamaanisha 'aliyetumwa'. Eliakimu inamaanisha "Mungu anainua'

Mitume ni wale ambao Yesu anaita, anainua na kutuma.

Mtume Paulo aliwaambia Wakorintho kwamba ***"Hata kama mna waalimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi, maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo kwa njia ya injili***" **1Wakorintho 4:15.** Wengi kanisani leo hawana baba. Duniani-kote, kanisa limekuwa halina baba lakini, kwa kuwa Mungu amekuwa akiinua mitume tena. Amewarejesha akina baba na kanisa limekuwa lina uhusiano kama iupasavyo mwili unaohusiana na Kichwa, Yesu Kristo.

Ufunguo wa Daudi Unapatianwa kwa Yule Mungu Anainua.

"***Na ufunguo wa nyumba ya Daudi nitauweka begani mwake; yeye atafungua wala hapana atakayefunga; naye atafunga wala hapana atakayefungua"*** **Isaya 22:22.** Hii ndiyo aya ambayo imenukuliwa kutoka **Ufunuo 3:7,** na ni Yesu aliye na ufunguo wa Daudi. Yeye ndiye afunguaye na hakuna afungaye, na afungaye na hakuna afunguaye.

Unguo wa Daudi ni nini? Ni ufunguo uliokuwa na msimamizi wa nyumba ya Yuda. Msimamizi alikuwa ni yule mtu aliyewakilisha mfalme ambaye aliangalia kazi ya ufalme. Shebna alimwakilisha mfalme Hezekaya, akiisha kuchaguliwa naye, na alikuwa na ufunguo ambao ulimpatia mamlaka ya mfalme. Ufunguo utachukuliwa kutokakwa Shebna, msimamizi, na upewe Eliakimu, ambaye Mungu anainua. Nafasi ya msimamizi itachukuliwa na mtume.

Ufunguo ni sawa na ile pete ya mfalme ambayo ilitumiwa na mfalme ishara ya mamlaka. Farao alimpa Yusufu pete yake na ikampa mamlaka ya kufunga na kufungua, kuamuru Misri yote, watu wake na uchumi wake (**Mwanzo 41:42).** Katika **Hagai 2:23** Bwana anamwambia Zerubabeli gavana [mjenzi wa kanisa/nyumba ya Mungu, ***"Nitakufanya uwe pete yangu ya mamlaka, kwa kuwa nimekuchagua***". Mungu anamtambua mtume kama yule avaae pete ya mamlaka. Pete ya mamlaka ni sawa na ufunguo wa Daudi. Wakati mwana mpotevu alirudi nyumbani, baba alimvisha pete kwa kidole pia. Baba akamtambua kama mwana akisema, ***'****una urithi wote, na pete hii inakupatia mamlaka kama niliyo nayo'.*

Yesu Ameshika Ufunguo wa Daudi

Yesu ndiye aliyepewa mamlaka hayo na Mungu (**Mathayo 28:18).** Ameshika ufunguo wa Daudi, lakini alipatiana funguo za ufalme kwa mtume Petro (**Mathayo 16:18-19)** akimwambia ***"Lo lote utakalofunga (kukataa) duniani litafungwa mbinguni, na lo lote utakalofungulia (kukubali) duniani litafunguliwa mbinguni".*** Haya ndiyo mamlaka ambayo Yesu amepatia mitume wake. Eliya alikuwa na mamlaka hayo ya kufungua na kufunga mbingu. Alikuwa na uwezo wa kumwambia Ahabu, ***"Kama BWANA, Mungu wa Israeli, aishivyo, ambaye ninasimama mbele zake, hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii, ila kwa neno langu"*** **1Wafalme 17:1.** Alikuwa na mamlaka ya kufunga mbingu. Hayo ndiyo mamlaka

ambayo Mungu anapatia mitume. Katika msingi wa mamlaka yake, Yeu aliwatuma mitume "***kufanya mataifa yote kuwa wanafunzi"*** **Mathayo 28:19.**

Petro, mtume, alipewa funguo.

Yesu alisema kwa Petro, ***"wewe ndiwe Petro, (jiwe kubwa ama mwamba mdogo) na juu ya mwamba huu (akimaanisha mwamba mkubwa – akinena kuhusu Kristo mwenyewe) nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda".*** Petro amewekwa na Yesu kama jiwe la msingi ambalo Yesu atalijenga kanisa. Kisha Yesu akapatiana funguo kwa mtume za kufungua na kufunga na akasema kwamba hakuna jambo litazuia kanisa lake kujengwa. Petro ni kiongozi wa kitume, aliyechaguliwa na Yesu, kuweka msingi katika kanisa la kitume. Peto ni jiwe la msingi, kama mtume, aliyewekwa juu Mwamba Wenyewe. Kumbuka Paulo baadaye anasema kanisa limejengwa juu ya ***"msingi wa mitume na manabii"*** **Waefeso 2:20,** na Petro mwenyewe aliandika kwamba tunapaswa kuja kwa Yesu ***"jiwe lililo hai"*** na ***"kama mawe yaliyo hai" "kujengwa kuwa nyumba ya Roho"*** **1Petro 2:4-5.**

Petro alipewa funguo kuona ufalme wa Mugu
umedhihirishwa duniani kupitia kanisa,
kama mtume aliyechaguliwa na kutumwa na Yesu Kristo.

Tambua kwamba funguo za ufalme zimepatianwa kwa Petro haswa mara tu Yesu alipotangaza kwamba milango ya kuzimu haitalishinda kanisa. Funguo na milango zote zinazungumzia uhakika uliofanana. Milango inawakilisha mahali pa mamlaka na funguo zinafunga ama kufungua milango. Kwa wakati huo, mmoja angesema kwamba ufalme wa mbinguni ulikuwa ungali umefungwa lakini Petro alikuwa amepewa funguo kufungua milango ya mbinguni na kila jaribio na shetani kuzuia tukio hilo haingefaulu. Kanisa ndilo gari ambalo Mungu amepachagua pa ufalme wake kudhihirishwa. Tangu msalaba na kufufuka, Yesu ameshika ***"funguo za mauti na za kuzimu"*** **Ufunuo 1:18.** Yesu alikuwa akipatia Petro funguo za ufalme wa mbiguni, akijua kwamba angepambana kupata funguo za mauti na kuzimu kutoka kwa shetani kupitia msalaba.

Misingi ya kanisa la Yesu Kristo iliwekwa vyema na mitume ambao Yesu binafsi aliwatayarisha na kuwachagua, na kwa mitume ambao aliita na kuwapa karama baada ya kupaa kwake (**Waefeso 4:8-11).** Funguo zile ambazo Petro alipokea zilipatianwa kwa mitume wote na Paulo anaonyesha katika **Mdo 19,** na mahali kwingine, ya kwamba alikuwa na funguo za kudhihirisha ufalme wa Mungu, kwa kuimarisha kanisa ka Yesu Kristo vyema, kulingana na muundo wa kimaandiko.

Mungu anainua uongozi mpya wa kanisa lake katika siko hizi. Shebna, msimamizi, anawakilisha uongozi wa zamani ambao umekuwapo kwa miongo katika makanisa ya haiba/Pentekosti na kwa karne nyingi kwa baadhi ya makanisa ya kidini. Eliakimu anawakilisha uongozi mpya ambao Mungu anainua, uongozi wa mitume ambao watakuwa 'akina baba' kwa watu wake na ambao watahubiri fundisho la kitume na kufanya kama vile fundisho linasema.

Athari za Uongozi Mpya

*"**Nami nitamkaza kama msumari mahali palipo imara; naye atakuwa kiti cha utukufu kwa nyumba ya baba yake"*** **Isaya 22:23.** Wakati uongozi wa kitume utarudi pahali pake, utakuwa kama msumari ulio salama ambao utaleta usalama kwa watu wa Mungu kwa kutoa msingi mwema wa imani na matendo. Kwa maana mitume wemewekwa, kanisa ***"Litafanyika***

enzi ya utukufu kwa nyumba ya baba yake". Kanisa litaanza kuwa kanisa lenye utukufu ambalo lilikusudiwa liwe, ili enzi ya Bwana Yesu Kristo, Ufalme wa Yesu Kristo utafunuliwa duniani. Yesu ataenziwa miongoni mwa kanisa lake. Hivi ndivyo Yohana alimwona ***"katikati ya vile vinara saba"*** **Ufunuo 1:12-16**. Zile vinara saba zinawakilisha kanisa lililokamilika (saba).

Kupitia kuhubiri ***"Utajiri wa Kristo usiojulikana",*** ambao ndio ujumbe kamili wa injili ya ufalme wa Mungu, Yesu Kristo atainuliwa. Ni kupitia kanisa kujua ***"Ushirika wa siri",*** kujua kikamilifu unamaanisha nini kuwa ***"ndani ya Kristo"*** na Kristo ni nani ndani yetu, yakuwa Ubwana wa Yesu Kristo utajulikana na mamlaka na nguvu katika himaya ya mbinguni, kwa watu duniani na wakaazi wa kuzimu (**Wafilipi 2:9-11).**

Ni wakati wa kumfanya Yesu kuwa mfalme; ni wakati wa kuyatengeneza mambo; ni wakati wa kanisa kupokea uongozi mpya kulingana na mpangilio wa Mungu – ***"wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu"*** **1Wakorintho 12:28.** Ni wakati wa kanisa kutakaswa na kuoshwa ili tuletwe tukiwa ***"kanisa lenye utukufu"*** **Waefeso 5:26-27.**

Utukufu Utafunuliwa.

"Nao wataangika juu yake utukufu wote wa nyumba ya baba yake; wazao wake na watoto wao, kila chombo kidogo tangu vyombo vya vikombe hata vyombo vya makopo vyote pia" **Isaya 22:24.** Wakati mitume wanainuliwa, wale ambao wanamwakilisha Kristo, basi kutakuwa na akina 'baba' katika nyumba, na akina 'baba' wanawapata 'wana'. Mungu atawaondoa wale ambao wameinuliwa na watu, wasimamizi na maaskofu ama watawala. Wakati ninasema Mungu atawaondoa hawa, haya yatatendeka kwa njia moja ama mbili: Awe mtu aliye kwenye ofisi ni msimamizi au askofu apokee ufunuo wa kitume, apokee hali ya kufanywa mwana na kuanza kutembea katika huduma ya kitume; ama mtu akatae kupokea mafundisho ya ndani na makamilifu ya neno la Mungu na kujipatiana kwa taasisi na mifumo, wakiwa na kutoelewa wito wa juu wa Mungu na kuufikia ukomavu.

Tumeshuhudia askofu, muangalizi wa makanisa mengi, ambaye baada ya siku moja katika semina ya kitume ambapo tulikuwa tukifundisha, alijiuzuru katika ofisi aliopewa na watu ofisi ya uaskofu kwa kuwa alipokea upako wa kitume. Huyu ndugu alipata mabadiliko katika maisha yake na sasa anatembea katika uwana [ukomavu unaoletwa na Roho ya kufanyika mwana] na katika huduma ya kitume, akiwaongoza wachungaji vyema na kupatiana uangalizi kama baba katika makanisa yote ambayo anahusika nayo.

Wakati kanisa limewekwa katika mpangilio na mitume wamewekwa, kisha utukufu wote wa baba utafunuliwa katika Yesu, ambaye atakuwa miongoni mwa kanisa lake. Kila mshirika kuanzia yule mdogo mpaka yule mkubwa atafunua utukufu wa baba. Paulo anatufundisha kwamba katika mwili ***"vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi"*** **1Wakorintho 12:23.** Paulo pia anatufundisha tujenge na ***"dhahabu, au fedha, au mawe ya dhamani"*** kwa maana moto utajaribu kazi (**1Wakorintho 3:12)**, na Paulo anatuhimiza kung'ang'ana tuwe vyombo vya dhahabu au fedha (**2Timotheo 2:20-21).**

Pasina mitume kanisa limekatwa

*"**Katika siku ile, asema Bwana wa majeshi, ule msumari uliokazwa katika mahali palipo imara utaregea; nao utakatwa na kuanguka chini, na ule mzigo uliokuwa juu yake utakatiliwa mbali; maana BWANA asema haya"*** **Isaya 22:25.** Kama uongozi wa kitume haupo katika mpangilio kila kitu kinaanguka. Kanisa litabaki likiwa limevunjika na kugawanyika ampapo linatawaliwa na waangalizi badala ya kuongozwa na akina baba mitume ambao Mungu amewainua. Kanisa ambalo liko duniani leo, licha ya mambo yote mazuri ambayo yametendeka

kwa neema ya Bwana na upako wa Roho Mtakatifu, halijawakilisha Yesu Kristo vya kutosha na halijafikia utukufu, hata kama mabaki.

Mungu Anaweka Kanisa Lake Litembee Katika Uwana

Katika mwanzo wa huduma ya Yesu, wakati wa ubatizo wake, sauti ya Baba ilisema ***"Huyu ni mwanangu mpendwa wangu ninayependezwa naye"*** **Mathayo 3:17.** Huu ndio uliokuwa mwanzo wa Yesu kutembea katika uwana (kuwekwa na Roho katika mahali pale pa ukomavu kuyatenda mapenzi ya Baba). Wakati Yesu alipokuwa akija katika kikomo cha huduma yake alienda juu mlimani akiwa na Petro, Yakobo na Yohana, na alibadilishwa katika utukufu machoni pao. Sauti ya Baba ilisema tena***, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, msikieni yeye"*** **Mariko 9:7**.

Yesu alidhibitishwa na Baba kuingia katika uwana mwanzo wa huduma yake. Katika mlima wa kugeuzwa, alionekana katika utukufu wake wote na Mungu akatoa maagizo kwa wanafunzi wake 'kumsikiza'. Katika huduma ya Yesu ya mda mfupi alionyesha kutembea kwake na Mungu kikamilifu hapa duniani. Alifikia utimilifu. Utukufu wote wa Babaye alifunuliwa ndani katika mlima wa kugeuzwa. Haya hayakutendeka katika ubatizo wake hata kama alipokea Roho wa Baba yake bila kipimo. Hata hivyo, kanisa mwisho wa nyakati (ama angalau kikundi cha mabaki) ni kutembea katika utimilifu wa uwana na ni kupitia mabaki haya ambapo sauti ya Baba itasikika.

Kanisa Litachukua Utukufu wa Kristo

Mungu anainua uongozi mpya ili kanisa lifike kiwango cha ukomavu, likiuchukua utukufu wake. Ni nani auchukuaye utukufu? Katika **Zekaria 6:11:13** BWANA anapeana maagizo kwa Yoshua mwana wa Yehosadaki, kuhani mkuu, kuwa na taji amevikwa kichwani mwake, na kisha katika **aya 13** BWANA anasema ***"yeye atalijenga hekalu la BWANA; naye atauchukua huo utukufu; ataketi akimiliki katika kiti chake cha enzi; na kutakuwa na kuhani katika kiti chake cha enzi".*** Yoshua ni kuhani akivikwa taji kama mfalme. Yesu alitimiza unabii huu na kufanyika mfalme/kuhani. Yesu anachukua utukufu wa Baba na kanisa limewekewa hatima ya kubeba utukufu wa Yesu ambao ni utukufu wa Baba. Yesu alionyesha katika huduma ya binafsi alipotembe katika nguvu za Roho na kufikia mahali ambapo utukufu wa Mungu ungedhihirika ndani yake (kugeuzwa), hata hivyo analiandaa kanisa lenye utukufu bibi arusi duniani ambao watadhihirisha utukufu wake duniani.

Wakati mitume wamewekwa mahali pao

Kanisa limerejeshwa

Yesu ataenziwa miongoni mwa kanisa lake

Kanisa litauchukua utukufu wake!

Sura ya pili

KAZI ILIYOMALIZIKA YA YESU ALIYE MTUME

Mambo muhimu ya kuelewa ya kitume:
Ni wakati tutakapowapokea wale ambao wametumwa
ambapo tunampokea Yule aliyetumana

Kazi ya kitume ya Yesu, ambayo Baba alimpa,
ilikuwa ni kujipatiana kwa wale watu kumi na wawili
Katika hali ya kuwafundisha na kuwaandaa ili watumwe kama mitume

Imani kwanza ililetwa kwa mitume
Na wale ambao, walioamini neno la mitume,
walikuwa wawe mmoja na kuendelea katika umoja

Yohana 17:
Aya 4 "Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye.
Aya 6 Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu; walikuwa wako, ukanipa mimi, na neno lako wamelishika.
Aya 8 ***Kwa kuwa maneno ulionipa nimewapa wao; nao wakayapokea, wakajua hakika nalitoka kwako, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.***
Aya 10 ***Na wote walio wangu ni wako, na walio wako ni wangu; nami nimetukuzwa ndani yao.***
Aya 11-12 ***Wala mimi simo tena ulimwenguni, lakini hawa wamo ulimwenguni, nami naja kwako. Baba mtakatifu, kwa jina lako ulilonipa uwalinde hawa, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo. Nilipokuwapo pamoja nao, mimi niliwalinda kwa jina lako ulilonipa, nikawatunza; wala hapana mmojawapo wao aliyepotea, ila yule mwana wa upotevu, ili andiko litimie.***
Aya 13 ***Na sasa naja kwako; na maneno haya nayasema ulimwenguni, ili wawe na furaha yangu imetimizwa ndani yao.***
Aya 14 ***Mimi nimewapa neno lako; na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wa sio wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.***
Aya 17 ***Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli.***
Aya 18 ***Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo nawatuma hao ulimwenguni.***
Aya 20-21 ***Wala si hao tu nawaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.***
Aya 22-23 ***Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo na umoja; Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi".***

Yesu aliye Mtume

"Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu" **Wabrania 3:1.** Aya hii huvutia mawazo yetu kwa mambo mawili muhimu ya huduma ya Bwana wetu Yesu Kristo: Yeye ni Mtume na Kuhani Mkuu. Kwa miaka 1800 ama zaidi kanisa bila kufikiria juu ya Yesu aliye Mtume na asiri ya kitume ya kanisa. Licha ya ukweli wa imani ambao umesemwa kanisani la kitume,walisema pia kanisa lilikuwa la kikatoleki na watu wengi waliosema imani hawakuelewa mambo hayo mawili. Maandiko yanasema tunatakiwa 'kumtafakari Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu'. Neno hili 'kukiri' ni ya muhimu sana. Limeundwa na maneno mawili ya Kiyunani: *homo* ikimaanisa sawa, na *logeo* ambayo imetoka kwa *logos* neno; homologeo kihalisi inamaanisha 'kuongea neno moja'. Tunatakiwa kujua kutoka kwa neno la Mungu ya kuwa Yesu ndiye Kuhani Mkuu na tunajua kwamba, kama Kuhani Mkuu, alitoa sadaka kamilifu yake msalabani, na hiyo inatuokoa. Anaendelea daima kama Kuhani Mkuu, akituombea sisi katika enzi ya neema. Tunapaswa kujua pia kutoka kwa neno kuwa Yesu ndiye Mtume.

Yesu Mtume wa Mungu hajanenwa sana na wapendwa wengi hawana kukiri kwa Yesu aliye Mtume. Mtume ni nini?

Mtume ni Yule ambaye ametumwa kwa niaba ya mwingine
kumwakilisha huyo na kufanya kazi
ambayo ametumwa kufanya.

Yesu alitumwa kutoka mbinguni na Baba kumwakilisha Mungu na kufanya ajulikane, na kazi aliyopewa kufanya ilikuwa kuandaa jengo la kanisa, nyumba ya Mungu. Mtume ndiye mjenzi mkuu (**1Wakorintho 3:10).** Ni huduma ya kitume ambayo hufanya kazi kuziinua huduma zingine na kuzitia nguvu kufanya kazi ya huduma ***"kuwakamilisha watakatifu na kujenga mwili waKristo, hata na sisi sote… mtu mkamilifu"*** **Waefeso 4:12-13.** Huduma zote mbili ya Mtume na ya Kuhani Mkuu zilikamiliswa duniani na Yesu. Hii ilikuwa kutimiza mpango wa Mungu.

Katika **Yohana 19:28-30** Yesu ***"hali akijua ya kuwa yote yamekwisha kumalizika"*** alitangaza ***"Imekwisha",*** na kisha akafa. Ni nini imekwisha?

Yesu alikuwa amekamilisha kazi ya ukombozi
kama Kuhani Mkuu kwa kujitoa kwake msalabani.

Hata hivyo katika **Yohana 17:4,** Yesu alikuwa amesema msemo kama huo na hakuwa akionyesha kazi yake ya ukombozi.

Mazingira ya **Yohana 17** ni ya Yesu akizingumza na wanafunzi wake katika chakula chake cha mwisho (chakula cha pasaka) usiku ambao alisalitiwa. Yesu alikuwa akiwaagiza wanafunzi wake kuhusu mambo mengi kuhusu kifo chake kilichokuwa njiani na kufufuka. Mafumdisho yake katika chakula cha mwisho ilianza katika **Yohana 13** kwa kuwatawadha wanafunzi wake miguu.

Tukuza Mwanao

Hatimaye kabla yake kuondoko na kwenda katika bustani ya Gethisemane, Yesu ***"akainua macho yake kuelekea mbinguni"*** akasema maneno haya, ***"Baba, saa imekwisha kufika. Mtukuze mwanao, ili Mwana wako naye akutukuze wewe; kama vile ulivyompa***

mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote uliompa awape uzima wa milele" **Yohana 17:1-2**. Utukufu huja kutoka kwa Baba hata kwa Mwana, na kupitia Mwana inaleta uzima wa milele kwa wale ambao Baba amepatiana. Mwana humtukuza Baba kwa kuleta kipawa cha wokovu kwa binadamu, ambayo hufanyika kwa kuzaliwa upya. Wakati nafsi inaokolewa na kumpokea Yesu, hii inamletea Mungu utukufu. Maisha halisi ya Mungu imeingia ndani ya mtu kwa Roho wa Mungu. Adamu mwanzo alipokea uzima kama kiumbe kilichoubwa kwa kupokea **"pumzi ya uhai" Mwanzo 2:7**. Sasa kupitia Yesu akiisha kukamilisha kazi yake duniani, kazi ya Kikuhani na ya Kitume, mtu anaweza kupokea **"uzima wa milele".**

"Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliye mtuma" **Yohana 17:3**. Uzima wa milele ni kumjua Mungu katika Yesu Kristo. Neno hili 'jua' ni ' *epignosis'* na inamaanisha kuwa na usadiki wa ndani, na kujua kwa ndani Mungu ni nani. Tunapaswa kumjua Yule ambaye 'ametumwa'. Neno hili tumwa ni neno '*apostello'* kwa Kiyunani. Yesu ndiye Yule aliyetumwa na Mungu; alikuwa ni mtume wa Mungu. Ni Yesu aliye Mtume ambaye anaomba ombi hili kwa wale aliowainua na amewaandaa kutumwa ulimwenguni kama mitume. Yeye anasema mitume aliokuwa nao walikuwa wamepokea uzima wa milele kwa kuwa walikuwa wamempokea yeye.

Jambo la muhimu la kufahamu la kitume:
ni tunapompokea yule aliyetumwa tunampokea Yule aliyetumana.

Nimemaliza Kazi

Katika **Yohana 17:4**, Yesu anasema, ***"mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye".*** Kazi 'iliyokamilika' ni gani ambayo Yesu alikuwa akimaanisha hapa? Haimaanisha kazi zake za mbadala msalabani. Tayari tumeona, katika **Yohana 19:30**, Yesu akitangaza kazi ya ukombozi ikimalizika. Hamaanishi kazi yake ya ukombozi ambayo ni kazi ya Kuhani Mkuu, lakini anamaanisha kazi yake ya utume ambayo ilikuwa ni ya kuwainua wale thenashara.

Ni huduma ya kitume ya Yesu, ambayo imeterekezwa katika historia ya kanisa. Katika siku yetu Mungu anawarejesha mitume kwa kanisa lake na kupitia hao anaonyesha, tena, Yesu kama mtume. Kazi kuu ya mtume ni kujenga nyumba ya Mungu (kanisa) na njia ambayo Mungu amechagua kulijenga kanisa lake ni kupitia huduma ya mitume na kisha, na kwa wakati ufaao, kupitia huduma zile zingine ambazo amepeana, tunatambua kwamba Yesu hakuwachagua manabii kumi na wawili, ama wachungaji kumi na wawili kuwa huduma ya msingi ya kanisa lake na kuwajibika kwa kulijenga kanisa, hatimaye wakiliongoza kanisa katika kukua kwake hadi utimilifu.

Yesu aliinua huduma mpya: huduma ya mitume.

Huduma ya Yesu ya kitume ilikuwa kwa watu kumi na wawili

Yesu anasema, katika **Yohana 17:6-19**, kwamba kazi aliyokuwa amekamilisha ilikuwa ni kuwaanda wale thenashara kuwa mitume. Jambo muhimu la kwanza ambalo Yesu anaripoti kwa Baba katika kuwaandaa wale kumi na wawili liko katika aya **ya 6** ***"jina lako nimewadhihirishia ((kufunua) watu wale ulionipa katika ulimwengu; walikuwa wako, ukanipa mimi, na neno lako wamelishika"***. Injili tatu, Mathayo, Mariko na Luka, wote wanataja kwa wazi wale mitume kumi na wawili wa kwanza walioitwa na kuchaguliwa na Yesu. Kumbuka, ya kuwa huduma ya mitume ni huduma ya agano jipya ambayo ilianzishwa na Yesu: Alikuja kama mtume wa Mungu

kuwainua mitume miongoni mwa watu kwa kulijenga kanisa lake. Yesu anaonyesha ndani yake huduma kamili ya mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji na mwalimu, lakini ni huduma ya mtume ambayo haswa alikuja kuanzisha. Hii ndiyo huduma ya muhimu ambayo inatakikana kujenga nyumba (kanisa) ya Mungu. Yesu ako wazi: Mungu alimpa watu wachache, na mmoja wao ni mwana wa "upotevu", kwa hivyo katika **Yohana 17,** ana wanafunzi kumi na mmoja.

Yesu alifanya tu kazi ya Baba.

Kuna somo kubwa la ndani letu sisi sote tusome: kazi ya Yesu ya kitume ambayo Mungu alimpa ilikuwa ni kumakinika kwa watu kumi na wawili katika hali ya kuwatayarisha. Moja wapo wa wale kumi na wawili alipungunga lakini Yesu anamshukuru Baba yake na kumwomba Baba aachilie utukufu wake kwa watu hawa. Watu hawa 'ni taji yake na utukufu!'. Katika kuja katika tamati ya huduma yake, Yesu hamkumbushi Baba kuhusu wale wote ambao walikuwa wameponywa! Hakumkumbusha Baba kuhusu wanafunzi wote ambao alikuwa amefundisha! Hakumkumbusha Baba kuhusu wale sabini ambao aliwatayarisha na kuwatuma katika **Luka 10!** Lahasha, Yesu alikuwa akihusiana na Baba kuhusu ufanisi aliokuwa nao katika kuwainua mitume kumi na wawili (nafasi ya Yuda iskarioti ilichukuliwa na Mathiya katika **Mdo 1**). Hii ndio ilikuwa kazi haswa ambayo Baba alimpa. Twahitajika kufanya kazi ambayo Baba ametupatia. Katika hesabu ya mwisho haitakuwa ni namba za wale tuliohudumia, idadi ya kusanyiko, mijengo ambayo tumejenga au huduma ya ishara na maajabu ambayo tumefanya, lakini itakuwa: 'tulikuwa watiifu kwa mwito wa Baba kufanya kazi yake?'

Yesu alidhihirisha jina la Baba

Hii inamaanisha nini? Katika injili, Yesu anamuonyesha Mungu kama Baba, ama ananena na Mungu kama Baba mara 170. Je 'Baba' ni jina ambalo Yesu alidhihirisha kwa wanafunzi wake? 'Baba' ni jina? Kikawaida Baba ni kichwa alichopewa yeye ambaye ni Baba na ni sawa na Mungu. Yesu hatuambii kuwa jina la Mungu ni Baba lakini, bali anatutambulisha kwa Mungu kama Baba Yetu. Huu ulikuwa ni ufunuo kali wa agano jipya: **Mungu ni Baba yetu.**

Kwa hivyo ni jina gani alilolidhihirisha kwa wanafunzi wake? Wakati Mungu alimwita Musa, katika **Kutoka 3**, na kumtuma aende misri, Musa alisema, ***"nawaniulize, jina lake ni nani? Niwaambie nini?"*** **aya 13.** Mungu akamwambia Musa, ***"MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli; mimi niko amenituma kwenu"*** **aya 14.** Jina hili lililofunuliwa la Mungu limetafsiriwa ***'Yahweh ama Yehova'*****, (Kutoka kwa *YHWH)*** lakini sanasana katika Biblia ya Kingereza ni vigumu kutamka jina la Kiebrania la Mungu, hivyo anapewa 'BWANA' (zaidi ya mara elfu sita). Hili ni jina lililofunuliwa la Mungu katika agano la kale. Yesu alisema, ***"nimedhihirisha jina lako kwa wale watu ulionipa".***

Kwa Jina Langu

Kwa hivyo jina lililofunuliwa ni lipi katika agano jipya? Wakati malaika alimtangazia Mariamu ya kuwa Mungu alikuwa anamleta mwana wake kupitia yeye, alisema***, "na jina lake utamwita Yesu"*** **Luka 1:31**. Yesu ni jina fupi la ***Yehoshua*** ambayo inamaanisha ***'Yahweh ni wokovu'*** ama ***'BWANA aokoa';*** kutoka kwa haya tunapata jina 'Mwokozi'. Mara nyingi katika injili Yesu anaonyesa kwa jina lake mwenyewe ***"katika jina langu".*** Alisema maombi yatajibiwa kwa jina langu; mapepo wanakemewa kwa jina langu; wagonjwa wanaponywa kwa jina langu. Pia utafahamu kuwa jina ambalo linakupatia mamlaka juu ya mapepo ama juu ya maradhi ni jina la Yesu. Haiwezekani kufaulu kumkemea pepo aende 'katika jina la Baba na

mwana na Roho Mtakatifu' ama katika jina la Mungu mwenye nguvu zote. Mungu ametupa jina la YESU. Petro alitangaza katika **Matendo 3:16** kwamba yule kiwete alipokea nguvu ***"kupitia imani kwa jina lake",*** na katika **Mtendo 4:12** Petro anatangaza kwamba ***"hapana jina jingine chini ya Mbingu waliopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo".*** Jina gani? **YESU**.

Maandiko yanasema ***"kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkiria Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe la vitu vya mbinguni, (ikizungumzia mamlaka na nguvu – mbingu ya mapepo) na vya duniani (watu) na vya chini ya nchi (mapepo ya kuzimu) na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana kwa utukufu wa Mungu Baba***" **Wafilipi 2:9-11**

Nguvu na mamlaka ni katika jina la YESU!
Jina katika Agano jipya ni YESU!
Jina lake kamili ni BWANA YESU KRISTO!

Jina Katika Ubatizo

Katika **Mathayo 28:18**, Yesu alitangaza kwa mitume ***"nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani".*** Yesu ndiye mtawala mkuu juu ya mbingu na dunia na wakati aliamuru mitume ***"kuenda na kufanya mataifa yote kuwa wanafunzi"*** aliwaambia wabatize ***"kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu***" **Mathayo 28:19.** Tambua alisema 'jina' kwa umoja, sio 'majina'. Tunapotambua haya, tunaweza kuelewa kwa nini Petro, katika **Mdo 2:38**, alikuwa akifanya kazi katika kutii, wakati aliamuru wale walioamini katika injili wabatizwe ***"katika jina la Yesu Kristo".*** Hakika katika kumbukumbu zote za ubatizo wa maji katika kitabu cha **Mdo** wanarejerea jina kwa umoja. Katika habari za Paulo na towashi wa Kushi, jina lililotumika katika ubatizo halijatajwa. Paulo alikuwa na ujuzi wa ajabu alipokutana na Bwana na akasema, "nani wewe Bwana?' Kisha Bwana akasema, 'mimi ndiye Yesu"' **Mdo 9:5.** Paulo alifikia kumjua Bwana Yesu, kwa hivyo tunaweza kudhania alibatizwa kwa jina la Bwana Yesu. **Mdo 8:16** inasema waumini wapya katika Samaria ***"walikuwa wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu***", tunaweza kudhania Filipo alimbatiza huyo mtu wa Kushi kwa jina hilo pia. Petro aliamuru waumini wa mataifa ambao walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu katika nyumba ya Kornelio "***wabatizwe kwa jina la Bwana"*** **Mdo 10:48.** Paulo katika **Mdo 19:5** alibatiza ***"kwa jina la Bwana Yesu".*** Hatua ya kwanza ambayo tunatakiwa kuchukua katika kuwafanya wanafunzi ni kuwabatiza wote ambao wanaamini kwa jina.

Tunapaswa kudhihirisha kwa wanafunzi
vijana jina la Bwana

Nimewapa yale maneno

Jambo la pili ambalo Yesu alisema kwa Baba ambalo alikuwa amefanya katika kuwatayarisha mitume liko katika **Yohana 17:8***.* ***"Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao; nao wakayapokea, wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma".*** Matokeo ya wanafunzi kopokea neno ilikuwa wajue Yesu alikuwa nani, na ya kuwa alikuwa ametoka kwa Mungu. Kusudi la kimsingi la neno ni kumdhihirisha Mungu na kufanya ajulikane. Hii ndio huduma ya mitume katika **Mathayo 10:40** ***"Awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenituma".*** Yesu alikuja kama mtume wa Mungu na kwa kushiriki neno la Mungu kwa wale ambao Mungu alikuwa amemtuma

na wale ambao walikuwa wamempokea kama Masihi, walikuja kujua Yeye alikuwa nani na kwa kufanya hayo kumjua Baba.

Yesu alisema ***"maneno uliyonipa nimewapa wao";*** Aliwafundisha wanafunzi neno la Mungu. **Hii ni huduma ya kufundisha.** Hatua ya pili katika kuwafanya wanafunzi ni ***"kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi"*** **Mathayo 28:20.** Yesu aliwafundisha mitume na akaachilia ndani yao maneno ambayo Mungu alikuwa amempa. Hii ni ya ajabu sana! Yesu kwa wepesi anasema ya kwamba alifaulu kuwafundisha mitume kwa kudhihirisha jina la Mungu kwao na kuwapa neno la Mungu. Yesu anasema, nimewapokea wale ulionipa; nimelifunua jina lako kwao; nimewafundisha neno ulilonipa lao. Yesu alikuwa mtiifu kwa mapenzi ya Baba.

Nimetukuzwa ndani yao

Jambo la tatu ambalo Yesu alisema kuhusu kuwatayarisha wale mitume kumi na wawili iko katika **aya 10*. "Na wote walio wangu ni wako, na walio wako ni wangu; nami nimetukuzwa ndani yao".*** Yesu aliwapokea wale thenashara ambao walikuwa wawe mitume kutoka kwa Baba. Aliwaleta katika kiwango cha ukomavu ambapo aliweza kujidhihirisha kwao. Akiisha kudhihirisha jina la Mungu kwao na kuliweka neno la Mungu kwao, Yesu husema sasa yeye ***"ametukuzwa ndani yao".*** Mtume Paulo anasema lengo lake kama mtume ni kuwajulisha watakatifu ***"utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu"*** **Wakolosai 1:27**. Yesu alikuwa amewaleta wale thenashara kufikia mahali ambapo alitukuzwa ndani yao. Kwa njia ingine, watu hawa sasa waliweza kuubeba uwepo wa utukufu wa Bwana ndani yao na kumwakilisha kikamilifu kwa wale ambao wangelichuckua neno lao.

Lengo ni Kristo atukuzwe katika watakatifu.
Kanisa la Yesu linatakiwa kuufikia ukomavu,
Kutembea katika utukufu.
Hili ndilo lengo la huduma ya kitume:
Kristo kudhihirishwa katika kanisa lenye utukufu.

Katika **Warumi 8: 29-30,** tunaona kwamba "***aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita; na wale aliowaita hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza".*** Kufanyika haki inafanyika kupitia damu ya msalaba: tumeokolewa! Lakini kutukuzwa huja kwa sababu damu iyo hiyo ilichukuliwa na yesu katika hema ambayo haikufanywa na mikono ya mwanadamu, katika mbingu yenyewe na kuwekwa katika kiti cha rehema halisi ikionyesha kwamba Mungu amewaita watu wake katika utukufu katika Kristo Yesu (**Waebrania 9:11-12, 24, 1Petro 5:10).** Yesu aliwainua mitume kwa kiwango cha ukomavu ambapo angetukuzwa ndani yao kisha nao, kupitia karama ya huduma ya mtume, ingeleta kanisa katika ukomavu kutembea katika ufunuo wa siri, ambao ni "***Kristo ndani yenu".*** Lengo la Mungu ni kuandaa ***"kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyazi"*** **Waefeso 5:27.**

Kuhifadhiwa kupitia jina.

Jambo la nne ambalo Yesu anarejelea ni kuuliza Baba ***"kwa jina lako ulilonipa uwalinde hawa, ili wawe na umoja kama tulivyo"*** **Yohana 17:11.** Katika **aya 12,** Yesu alisema kwamba ***"mimi naliwalinda"*** katika jina la Baba. Kwa njia nyingine Yesu alikuwa amewaonyesha nguvu

za jina lake na alikuwa na uhakika kwamba, baada ya kuondoka wataendelea kujua 'nguvu za kuhifadhi za Mungu' Yuda anasema ***"yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa"*** **aya 24.** Bwana anaahidi kwamba ***"Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa"*** na ***"mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo"*** **1 Wathesalonike 5:23-24.**

Jambo kuu katika kuja katika ukamilifu ndani ya Kristo wakati mambo yote yanaonekana kuwa mazito na magumu kwetu, ni kuleta mazao, 'kukata tamaa', kusema kwa Mungu 'siwezi kuyafanya haya'. Hekima kutoka kwa Mungu ni ***"tayari kusikiliza maneno ya watu"*** **Yakobo 3:17.** Kumbuka imani huja kwa kusikia (**Warumi 10:17).** Tunapolisikia neno la Mungu na kuwa tayari kuleta mavuno, imani tunayohitaji tutapewa. Kumbuka tena Mungu amepima kwa kila mmoja imani tunayohitaji kufanya kazi katika neema yake katika mwili wa Kristo (**Warumi 12: 3-4).** Acha Mungu awahifadhi kwa neema yake katika nguvu za jina lake. ***"nilipokuwapo pamoja nao, mimi naliwalinda kwa jina lako ulilonipa"*** **Yohana 17:12a.** Mojawapo ya msingi ambao Mungu anataka kila muumini ajifundishe ni kuyajua mamlaka ya jina lake, jina la Bwana, juu ya ibilisi na juu ya kazi zote zake. Kila muumini anatakiwa kujua ya kwamba anaweza kupinga na kushinda hata mashambulizi ya kuogofya.

Yesu anatambua kwamba hata moja wa wale mitume thenashara alipotea ***"ili andiko litimie"*** **Yohana 17:12.** Jambo kuu tunajifundisha kutoka kwa ushuhuda wa Bwana ni kwamba kazi zetu ni kufanya 'mapenzi ya Baba', sio mapenzi yetu. Mara kwa mara, katika hudunma na maisha ya kanisa, ni kushambuliwa na wasemaji wa kuhamashisha, watetezi wa ukuaji wa kanisa na wengine ambao wanataka kutupa 'malengo ya dunia' na kwa hivyo tunajikuta kwa msukumo wa kuwavutia na kuweka watu wengi katika makanisa Yetu ama kuwa na makanisa mengi na kadhalika, ambapo Baba anataka tuyajue mapenzi yake na kuyafanya. Mwana wa Mungu alisema alikuwa amemaliza kazi ambayo Baba alimpa kwa kufaulu kuwainua mitume kumi na wawili – Mathiya alichukua nafasi ya Yuda (**Mdo 1:26).**

Furaha yangu kutimizwa ndani yao

Jambo la tano ambalo Mungu alisema kuhusu mitume ambao aliinua ni ***"ili wawe na furaha yangu imetimizwa ndani yao"*** **Yohana 17:13.** Kwa kuwa mitume walijua 'jina la Bwana' na walikuwa wamepokea 'maneno ambayo Yesu aliwapa kutoka kwa Baba', na kwa sababu sasa wanaweza 'kuuchukua utukufu wa Bwana ndani yao' na wakajua 'nguvu za kuhifadhi za Mungu "na ulinzi wa jina lake', 'walijawa na furaha yake'.Tutapataje kuijua furaha hii? Yesu alitupa jawabu katika **Yohana 16:24*: "hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu"***. Twatakiwa kumwomba Baba kwa jina lake (**Yohana 16:23).**

Ni utimilifu huu wa furaha ambao unakuja, kupitia kumjua Yesu, ambao unatuwezesha kustahimili mateso ambayo huja kupitia majaribu ambayo sisi sote tutapitia. Yakobo anasema ***"hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali"*** **Yakobo 1:2-3,** kwa kuwa majaribu ni ya kujaribu na kuosha imani yetu. Vivyo hivyo Petro anapanua mandhari hii akituhakikishia ya kwamba, 'mara tu imani yetu imethibitishwa, ***"tuna furaha isiyoneneka, yenye utukufu"*** **1Petro 1:7-8.** Yesu mwenyewe ***"aliustahimili msalaba, kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake"*** **Waebrania 12:2**. Neema ya kumpokea Yesu aliye Mtume, ambayo inaweza kuachiliwa kwetu kwa kuwapokea mitume ambao anatutumia, imejaa na inajumuisha. Kama matokeo tunaweza kutembea katika utimilifu wa kufanya wana ambayo inachilia neema ambayo tunahitaji kustahimili mateso inayoletwa na majaribio tunayo pata. Furaha yake inatimilika ndani yetu.

Neno linatupa ushindi ulimwenguni

"Mimi nimewapa neno lako; na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wao sii wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu" **Yohana 17:14.** Ni neno la Mungu ambalo linagawanya. Yesu alisema ***"sikuja kuleta amani, bali upanga"*** **Mathayo 10:34.** Wakati tunaongea ukweli wa neno, watu watatupenda ama watuchukie.

"Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu" **Yohana 17:15.** Yesu alitufundisha kuomba ***"utuokoe na yule mwovu"*** **Mathayo 6:13,** na katika **2 Wathesalonike 3:1-3** Paulo anaongea kuhusu hitaji la kukombolewa ***"kutokana na watu wasio haki"*** (dunia), na kisha anasema, ***"Bwana ni mwaminifu, atakaye wafanya imara na kuwalinda na yule mwovu".*** Hatujaitwa kupigana na shetani lakini kujinyenyekesha kwa Mungu na neno lake naye atatukomboa.

"***Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli***" **Yohana 17:17**. Neno la Mungu lina nguvu za kutakasa ndani yake. Ni neno likifanya kazi ndani yetu ambalo linatutenga kwa mapenzi ya Mungu. Tunahitaji kuendelea katika neno; tunahitaji kuendelea kuwa wanafunzi wa neno na kisha ***"tutaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itatuweka huru"*** **Yohana 8:31-32.** Ni katika ***"kulisafisha kwa maji katika neno"*** ambapo tunaoshwa na kutakaswa, ili tuhudhuliswe 'kwake kanisa tukufu' (**Waefeso 5:27).**

Kutumwa kama mitume

Matokeo ya Yesu akiisha kuwatayarisha na kuwaandaa watu ambao Mungu alimpa ni kwamba sasa anaweza kuwatuma katika ulimwengu kama mitume***: "kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni"*** **Yohana 17:18.** Neno hili 'tuma' ni neno la Kiyunani *'apostello'* ambalo ni kitendo cha mtume. Yesu alikuwa amekamilisha kazi ambayo Baba yake alikuwa amempa kuifanya. Alikuwa amejipatiana sana kwa miaka mitatu na nusu ya huduma yake katika kuwafundisha na kuwaandaa mitume. Katika **Yohana 17:4,** Yesu anatangaza wazi kuwa amekamilisha kazi ambayo Baba alikuwa amempa.

Kazi hiyo ilikuwa ni kuwainua mitume katika mahali pa ukomavu ambapo sasa walikuwa tayari kutumwa kama mitume kumwakilisha Yesu na Baba, na kuwezesha mapenzi yake yatendeke kupitia kuhubiri kwa injili na kujenga kanisa la Yesu Kristo.

Jukumu la Yesu kama mtume wa Mungu ilikuwa ni kujenga kanisa. Yesu alitangaza ***"nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda"*** **Mathayo 16:18**. Mitume tayari walikuwa wamechaguliwa wakati huu na Yesu haswa akawa amemwambia Petro ***"wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu"***. Petro, kama mtume, anaenda kusimamia nafasi kubwa katika msingi na kulijenga kanisa. Baadaye Paulo anasema kwamba, kama mtume alikuwa ***"mjenzi mwenye hekima".*** Paulo alikuwa na funguo. Alijua jinsi ya kujenga! Alijua cha kujenga! Kanisa linapaswa kujengwa, likue kufikia ukomavu, likiweza kuubeba utukufu wa Mungu katika Kristo, hivyo ni 'Kristo ndani Yetu'.

Yesu anawaombea waumini wote

Akisha dhibitisha na Baba kwamba wale watu ambao Baba alikuwa amempa walikuwa wameandaliwa na tayari kutumwa, Yesu kisha anawaombea ***"wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao (mitume)"*** **Yohana 17:20.** Ombi lake ni wale wote watakaofundishwa na mitume watakuwa "**umoja"**. Umoja huu ni umoja wa Yesu akiwa ndani ya Baba na Baba akiwa ndani ya

Yesu, "***kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako***" **Yohana 17:21.** Matokea ya waumini kuja katika umoja wa Uungu ni kwamba dunia iamini Mungu alimtuma Yesu **aya 21.**

Imani kwanza iliwakilishwa na mitume
na wale ambao walioliamini neno la mitume
walikuwa wawe umoja na kuendela katika umoja.

Baada ya kufufuka kwake, Yesu aliwatuma mitume kufanya wanafunzi kwa kuwafundisha maneno ambayo Yesu alikuwa amewapa (**Mathayo 28:20).** Ni wakati mitume wanatumwa na Yesu na wanapokelewa na waumini ambapo kanisa linaundwa kulingana na maneno ya Yesu. Kanisa ni mwili wake na ni lazima lije pamoja katika njia ambayo ameitenga kufanya kazi kikamilifu na kuonyesha maisha yake na utukufu wake, kama shahidi ulimwenguni kote.

Ili wakamilishwe katika umoja.

Yesu alisema alikuwa ametukuzwa katika mitume (**Yohana 17:10)**. Kisha anasema kwamba atatukuzwa katika wale wote watakaoamini (**aya 22).** Ni uhakika huu wa utukufu wa Kristo katika watakatifu ambao utawawezesha kuwa ***"umoja kama sisi tulivyo umoja: mimi ndani yao nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja"*** **Yohana 17:22-23.**

Lengo la Mungu la kanisa ni ukamilifu. Njia ya ukamilifu ni kupitia utukufu wa Mungu ukifunika na kujaza kanisa lote. Mungu ameahidi kivuli kama hicho kwa mabaki katika **Isaya 4:5-6.**

Yesu anaiweka wazi katika aya hizi ya kwamba
udhihilisho wa utukufu wa Mungu ndani yetu
ndio njia ambayo tunakuwa umoja.

Uthihirisho huu wa utukufu unajulikana kwa ufunuo na maarifa ambayo inashirikiswa na mitume ambao wameinuliwa, na kutayarishwa na kutumwa na Yesu. Matokeo yatakuwa ***"ulimwengu utajua kwamba Baba alimtuma Yesu"*** **na ulimwengu utajua kwamba Yesu *"amewapenda [waumini] kama wewe [baba] umenipenda mimi"*** **Yohana 17:23.**

Yesu anaendelea kuwaombea waumini wote. Ni kweli kwamba waumini wote wanaoishi leo wanaweza kupokea kuona na faraja kutoka kwa maombi ya Yesu. Ni kweli, kwamba katika miji mingi, wachungaji kutoka miji mingi inakuja pamoja katika umoja wa miungano na kwamba huo ni utendakazi wa maombi ya Yesu. Hata hivyo wengi wemekosea mazingira kamili ya ombi la Yesu kwa waumini wote ni kwamba wamekuja kumwamini Yesu kupitia mitume. Kuna ufunguo hapa kwetu, katika siku za mwisho, na ufunguo ni, wakati mitume wanarejeshwa na kupokelewa, kanisa litaufikia umoja.

Umoja ambao Yesu aliombea, na ambao wengi wanatarajia,
Unawezekana tu kupitia utukufu wa Mungu katika Kristo
Akifunuliwa katika waumini.

Yesu ako wazi: **utukufu unaleta na kuwezesha umoja.** Utukufu unafunuliwa kupitia kuhubiri na kufundisha hekima ya ndani ya Mungu kwa wale walio wakamilifu**.** "***Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala wale wanatawala dunia***

hii, wanaobatilika; bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa , ambayo Mungo aliazimu tangu milele, kwa utukufu wetu" **1Wakorintho 2:6-7.** Ni hekima, ufunuo wa siri, ambao Mungu anafunua tena nyakati zetu kupitia mitume. Umoja ambao watakatifu wanatakiwa kujua katika Kristo utafunuliwa kupitia kuhubiri kwa siri za utajiri usiojulikana wa Kristo ambao unawezesha wote kuona ***"ushirika ni nini [koinonia #2842] wa siri***" **Waefeso3:8-9.** Kuna ushirika wa ndani ambao ni **ushirika wa umoja.**

Mapenzi ya Bwana ni kwamba sisi tuwe naye***, "hao ulionipa nataka wawe pamoja nami popote nilipo, wapate na kuutazama utukufu wangu ulionipa; kwa maana ulinipenda kabla ya kuwekwa msingi ya ulimwengu"*** **Yohana 17:24.** Yesu hazungumzii kuhusu maisha pamoja naye mbinguni, lakini, anazungumzia ufunuo wa siri ambao Paulo anarejelea katika **Wakolosai 1:26-27*, "siri ile iliofichwa tangu zanani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake; ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu".***

Hatimaye, Yesu anatanga katika maombi yake kwamba wale ambao amewapokea kutoka kwa Baba wamekuja kujua ya kwamba Baba alimtuma Yesu **Yohana 17:25.**

Kumpokea kwetu Yesu ndio funguo
Za kuja kumjua Baba.
Huu ndio ufunuo wa kitume:
Kuja kumjua Baba kupitia Yesu,
Kwa kuwapokea mitume(mtume) ambao Yesu ametuma.
Yesu anasema, ni kwa kutangaza
Jina la Mungu, ambapo ufunuo wa upendo wa Mungu
unafunuliwa katika mitume na waumini.

UTUKUFU ukija kwa watakatifu
Ndio funguo za umoja
Wa watakatifu katika Kristo –
Ni hapo tu UTIMILIFU unafika.

Sura ya Tatu

NI KWA NINI TUNAHITAJI MITUME LEO

Tumahitaji urejesho wa mitume kuleta mafundisho imara ya msingi ya elimu ya Kristo (**Waebrania 6:1-20)**; kujulisha hekima ya Mungu kuhusu muundo wa kanisa, kuhusu kuwekwa kwa huduma na uchaguzi wa wazee kila mahali.

Mpaka tutakapofikia hekima hii ya ndani ya maarifa ya neno la Mungu hatuwezi kufahamu ama kuelewa ambacho Mungu anatenda duniani kupitia kanisa lake, wala vile tutaleta kanisa mahali pa ukomavu hapo vya kutosha kutembea katika ufunuo wa siri, hivyo kwa ufahamu tukishirikiana na Bwana anapojifunua kwetu kupitia kanisa lake.

Nyakati za Urejesho

Mungu ni Mungu wa urejesho. Kanuni za urejesho zimefundishwa vyema katika maandiko. Urejesho ni:

- Kuweka vyema muundo wa kwanza;
- Mambo yakiwa kama yalivyo kuwa mwanzo;
- Kuleta viumbe kama vilivyo kuwa katika hali yake ya mwanzo;
- Kurejesha kanisa kwa muundo wa kibiblia na mpangilio.

Petro alitangaza kwa wayahudi, wakati alipokuwa akihubiri katika hekaru baada ya yule kiwete kuponywa, ya kuwa tunaingia katika nyakati za urejedho***. "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani; ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu"*** **Mdo 3:19-21.**

Andiko hili linaonyesha kwamba kuna vitu fulani
ambavyo sharti zifanyike kabla ya kurudi kwa Yesu.
Yesu amepokewa mbinguni
"hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote".

Tunaishi katika ziku hizo za urejesho na hata vitu vyote vitakaporejeshwa ambazo lazima zirejeshwe kulingana na neno la Mungu, Yesu haji kulipokea kanisa kwake.

"Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa" **Waefeso 5:25-27.** Yesu anakuja kwa kanisa lililooshwa na damu, lililotakaswa, lililo safi lenye utukufu. Mpango wake wa kanisa ni kurejesha kanisa hata liwe na utukufu zaidi hata kuliko mwanzo.

"Utukufu wa mwisho wa nyumba hii utakuwa mkuu kuliko utukufu wake wa kwanza, asema BWANA wa majeshi" **Hagai 2:9.** Kanisa la kitabu cha matendo ndilo ka kwanza (hekalu). Lazima kanisa lirudi mwanzo; lazima lirudilie muundo wa Biblia, kwa muundo wa kitume kama ilivyo imarishwa na Yesu kupitia mitume wa kwanza. Kanisa litarejeshwa, ***"kama lilivyo kuwa mwanzo",*** Hata katika utukufu zaidi.

Viumbe

Katika **Mwanzo 1:26,** Mungu alisema ***"natufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakawatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitabaacho juu ya nchi".*** Mungu anakusudia kwa mwanadamu awe na utawala ya vitu vilivyoumbwa. Anataka tufanyishe kazi hayo mamlaka. Katika **Mariko 4:41,** baada ya Yesu kutuliza mawimbi, wanafunzi wake walisema ***"ni nani huyu, basi, hata upepo na bahari humtii?"*** Yesu alionyesha mamlaka, ambayo Mungu alikusudia mtu awe nayo, kupitia miujiza yake na uponyaji. Mungu atarejesha mamlaka ya utawala kwa wana wa watu kama wanavyo inuliwa katika uthihirisho wa kufanywa wana (**Warumi 8:19-21).**

Mungu alimwambia mke na mume ambao aliwaumba, "***zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi"*** **Mwanzo 1:28.** Mke na mme, walioubwa kwa mfano na sura ya Mungu walikuwa waijaze dunia na uzao wa kiungu, ambapo wakisongeza wema na utajiri ya shamba la Edeni kupitia dunia yote. Walikuwa waitiishe nchi: kutiisha ni msemo wa kijeshi ukimaanisha kuchukua uhukani. Lengo la Mungu kwa watu wake ni kwamba wamtiishe shetani na kutawala duniani.

Katika **Mwanzo 1:2** twasoma kwamba "nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilidi vya maji". Dunia ilikuwa tupu; kumaanisha kwamba ilikuwa ikaliwe. Kama tujuavyo kwamba Mungu aliumba uhai aina yote kujaza nchi ili isiwe tena tupu. Ilikuwa haina umbo lakini Roho Mtakatifu alikuwa akitembea juu ya vilidi na kazi yake ilikuwa kuleta umbo na ulinganifu, ikileta jambo lisilo na msingi liwe na msingi maridadi duara duara, kama tuijuavyo leo.

Kuna kanuni ya wema wa Mungu wa ajabu unaoonyeshwa hapa: panapo giza na utupu na kukosa kusudi, Roho wa Mungu huja '*kutamia'* (SC #7363), kama ndege akaliaye mayai yake ili kuleta kitu kipya, kitu maridadi.

Uumbaji Unafunuliwa

"Mungu akasema, ***"iwe nuru; ikawa nuru"*** **aya 3.** Nuru ilikuwepo wakati wote kwa sababu ni nuru ya Mungu, lakini sasa Mungu alikuwa anaachilia nuru katika himaya ya nyakati /nafasi/jambo ambayo alikuwa anaumba. Ambapo Mungu yuko kila mara pana nuru. Neno 'iwe' katika aya hii ni neno la kuruhusu kutenda jambo, lakini ni zaidi ya hayo, ilikuwa pia ni amri ya kuumba ya nguvu za ajabu ikileta matokeo ya kushangaza. Ghafla, katika siku ya kwanza ya kuumba, Mungu alikuwa ameleta sura kwa jambo ambalo lilikuwa tupu na bila sura ambayo ilikuwa imetokea kwanza.

"Mungu akasema, na liwe anga katikati ya maji, likayatenga maji na maji" ***aya 6.*** Hii inazungumzia kuhusu kutenganishwa kwa mbingu kutoka dunia. Mungu akaumba 'anga'. Kabla ya haya hakukuwa na anga, maji tu ndiyo yalikuwa yamezunguka dunia. Wakati Mungu aliumba anga, alitenganisha maji kutoka juu na chini bado hapakuwa na nchi kavu. Kisha Mungu akasababisha nchi kavu itokee. Wakati ilitokea Mungu akasema ***"Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake"*** **aya 11.** Uumbaji wa miti na mimea haikuwa ile ya mbegu kumea, lakini Mungu aliumba kila kitu katika ukomavu wote. Kwa hivyo miti iliyokomaa, ***"ambao mbegu zake zimo ndani yake",*** zilitokea kutoka kwa nchi.

"Kisha katika **aya 26,** "Mungu anasema, ***"Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu".*** Katika kuumba mme na mke, Mungu anafunua kusudi lake la milele, kusudi lake jipya kwa viumbe**.** Wakati Paulo anatufumdisha kuhusu ndoa katika **Waefeso 5**, anasema ***"Ninanena siri kubwa"*** **aya 32**. Alikuwa akinena kuhusu Kristo na kanisa. Wakati Mungu alimuumba mme

na mke na akawaambia wawe mmoja, alikuwa akitenda kitendo cha kinabii. Alitudhihirishia kusudi lake la milele, ambalo lipo kuwa na kanisa kamilifu, likiunganishwa kikamilifu na Kristo hata kama vile hawa alikuwa arejeshwe pia, hivyo na kanisa!

Mungu ni Mungu wa urejesho

Kama ilivyokuweko mwanzo

Mapenzi ya Mungu ni kila kitu kipate kurejeshwa 'kama ilivyokuwa tangu mwanzo'. Katika **Mathayo 19:4**, Yesu anazungumza kuhusu ndoa kwa mafarisayo waliokuwa wakimuuliza maswali kuhusu taraka. Akawakumbusha vile ilivyokuwa tangu mwanzo. Ndoa ni kati ya mme mmoja na mke mmoja. Hivi ndivyo ilivyokuwa tangu mwanzo, huu ndio mpango halisi wa Mungu.

Viumbe vyapaswa kurejeshwa kwa kuachiliwa kutoka laana iliyo letwa na dhambi za mwanadamu na kuwekwa huru na ***"wana wa Mungu***" na kuingia kwenye ***"Uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu"*** **Warumi 8:19-21.**

Yesu Anarejesha Kanisa Lake

Yesu alisema "***Nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitaweza kulishinda***" **Mathayo 16:18.** Yesu Kristo aliuweka msingi wa kanisa. Aliuweka kwa kuwatayarisha na kwa kuwachagua mitume kumi na wawili. Mungu anataka kurejesha kanisa kama ilivyokuwa pale mwisho. Kanisa la kwanza katika kitabu cha mitume haikuwa imeungwa na dini tofauti, ama taasisi. Hata kama kulikuwa na watu vikundi tofauti katika manyumba, walikuwa wangali sehemu ya kanisa la mjini. Paulo aliliandikia kanisa la Waefeso, kanisa la Korintho, na kadhalika. Yesu anakuja kwa kanisa lililokomaa, kama ilivyokuwa tangia mwanzo! Kanisa katika kila jiji walikuwa ni watu wamoja wakiwa na wazee waliojinyenyekeza kwa mtume. Yesu aliwachagua mitume kumi na wawili ambao angetumia kulijenga kanisa lake. Alimpa Petro jukumu fulani la kimsingi katika kuimarisha kanisa, kwa hivyo akaimarisha muundo wa mitume wengine wote. Mitume wote hupokea kutoka kwa Yesu huduma ambayo ni ya kimsingi katika kuunda ama kurejesha kanisa na hiyo ni ya muhimu katika kuleta kanisa katika ukomavu.

Kanuni za Urejesho

"Vivyo hivyo wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watukuwa wa mwisho" **Mathayo 20:16.** Msemo huu unaweza kutafsiriwa kiunabii kusema kanisa la siku za mwisho litakuwa kama kanisa la mwisho na kanisa la kwanza litadhihirishwa katika la mwisho. Kuna msemo ambao unatafuta kueleza ujuzi wa kihistoria wa urejesho katika historia ya kanisa; '**ukweli wa kwanza uliopotea ndio ukweli wa mwisho ambao unarejeshwa; ukweli wa mwisho uliopotea ndio ukweli wa kwanza uliorejeshwa'.** Ukweli wa kwanza uliopotea ni fundisho la kitume. Kihistoria, mapema sana baada ya kuandikwa kwa maandiko ya agano jipya, maasikofu kibinafsi waliinuka wakichukua mamlaka juu ya kanisa la mji bila kupokea tena mitume ambao Mungu ***"ameweka katika kanisa"*** **1Wakorintho 12:28.** Ni kwa siku za hapa punde ambapo tunashuhudia kurejeshwa kwa mafundisho na huduma ya mitume katika kanisa la siku za mwisho.

Ukweli na Huduma Zimerejeshwa

Ukweli wa mwisho ulipotea hadharani wakati wa historia ya ukristo ulikuwa ni wokovo kwa imani. Hii ndio ilikuwa kweli ya kwanza uliorejeshwa katika hadhara kupitia Martin Luther

katika mapema karne ya 16. Kutoka wakati wa Luther mpaka leo kumekuwa na urejesho mkubwa wa ukweli na huduma na karama katika maisha ya kanisa. Hii imetendeka kupitia ufufuo, kupitia viongozi waanzilishi ambao Kristo alichagua na kuinua kurejesha ukweli. Hatimaye, katika nusu ya pili ya karne ya ishirini huduma tano za Waefeso 4:11 zimerejeshwa kanisani. Matokeo ya haya ni kwamba kanisa leo imekaa kupokea sehemu kubwa ya urithi wake kama kazi ya urejesho inakamilika pakubwa kwa wale wenye masikio ya kusikia, macho ya kuona na mioyo ya kufahamu ufunuo unaofunguka wa siri za neno la Mungu. Siri hizi zinajulikana tena.

Urejesho wa Mitume

Kanisa la kwanza ***"lilikuwa limejengwa katika msingi wa mitume na manabii"*** **Waefeso 2:20.** Kujenga kanisa la mwisho na kuona likitenda kazi kikamilifu, tunahitaji urejesho wa mitume na manabii, na tunahitaji mitume na manabii wajulishe vya kutosha "***habari za madaraka ya siri, ambayo ilistirika katika Mungu aliye ambayeviumba vyote kupitia Kristo"*** **Waefeso 3:9**. Tunahitaji urejesho wa mitume kuleta msingi imara wakifundisha elimu ya msingi ya kanuni za Kristo (**Waebrania 6:1-2)** na kufanya ijulikane hekima ya Mungu kuhusu muundo wa kanisa, kuhusu kuwekwa kwa huduma na kuchaguliwa kwa wazee katika kila mahali.

Mitume huleta Ufunuo wa Siri

Katika **Waefeso 3:3,** mtume Paulo anasema "***kwa njia ya ufunuo alijulishw siri".*** Siri hii sasa ***"imefunuliwa na Roho Mtakatifu kwa mitume wake na manabii"*** **aya 5.** Kwa hivyo tunahitaji urejesho wa mitume na manabii ambao wanajua ufunuo wa siri kwa kanisa. Mpaka tufikie ufahamu huu wa ndani wa maarifa ya hekima neno la Mungu hatuwezi kufahamu na kuelewa kile Mungu anafanya duniani kupitia kanisa lake. Wala hatuelewi jinsi ya kuleta kanisa katika pahali hapo pa ukomavu kutembea katika ufahamu wa siri, hivyo tukishirikiana kwa uelewa na Bwana anapo jifunua kwa kanisa lake. Ufunuo huu ***"ambayo tangu zamani zote ilistirika katika Mungu aliye viumba vitu vyote"*** sasa umepewa mitume kupitia majira ya neema, "***ili sasa kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"*** **Waefeso 3:8, 10.**

Kuna ufunuo wa siri ambao unapewa mitume tu. Shukuru Mungu, anarejesha mitume leo na ufahanu wa hekima ya ndani ya Mungu inafundishwa, ikiwezesha kanisa kuufikia ukomavu. Hii ndio hekima ya waliokomaa; ***"ni hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu"*** **1 Wakorinto 2:7-8.**

Mitume wanamwakilisha Kristo

Mitume wanatumwa na Yesu wamwakilishe yeye na kumfunua kwa njia ya kipekee. Yesu hajayasema haya kwa muhuduma mwingine. ***"Awapokeaye ninyi, anipokea mimi, naye anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenituma"*** **Mathayo 10:40.** Yesu alitumia msemo kama huo katika **Mariko 9:37** na **Luka 9:48**, akiongea kuhusu kumpokea mtoto kwa jina lake. Katika kuyafanya hayo Yesu anahimiza umuhimu wa jinsi tunampokea yule aliyetutumia akimwakilisha. Huduma ya mitume ni ya kipee kwa jia hiyo. Neno mtume kihalisi linamaanisha 'aliyetumwa'. Huduma hii ya mitume haswa ni ya Yesu, mtume wa Mungu, na mitume ambao aliinua, ikihusisha wale alioinua baada ya kupaa kwake, haswa kumwakilisha yeye. Ambapo kanisa lote linatakiwa kuwa la kitume, hivyo ni, likimwakilisha Yesu duniani, kuna ufunuo wa ndani ambao unarejeshwa kanisani kupitia urejesho wa mitume. Pasina fundisho la mitume na ufunuo hatuna ufunuo kamili wa Yesu Kristo.

Tunampokea Mwana na Baba

Yesu allisema kwamba, tukimpokea mtume, tunampokea, lakini pia akasema tukimpokea, tunampokea aliyemtuma. Hii inamaanisha Yesu anasema tunaweza kumpokea mwana yesu, na Baba. Kuna ufunuo wa Mwana na ufunuo wa Baba unaotufikia kupitia kumpokea mtume. Kuna ufunuo wa Mungu ni nani na asiri yake halisi: Yeye ndiye Baba na pia Mwana na wao ni mmoja. Ufunuo huu wa Mungu wa ndani na wa kushangaza na wa kutosheresha unarejeshwa na mitume wanapotumwa kumwakilisha.

Neema na Utume

"Ambaye katika yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani, kwa ajili ya jina lake" **Warumi 1:5.** Andiko hili linaleta pamoja vipengele viwili vya nguvu ya kazi ya Mungu duniani kwa injili. Jambo kubwa la agano jipya ambalo ni la ajabu na kushangaza ni neema. Maandiko yanasema mara mbili katika **Waefeso 2** tumeokolewa kwa neema, **aya 5 na 8.** Neema hii ***"tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele"*** **2 Timotheo 1:9,** lakini haikuachiliwa kwetu mpaka Yesu Kristo alipofika duniani. Inaweza semwa kwamba kufanyika mwili kwa Mungu katika Yesu Kristo kimsingi kufunuliwa kwa neema ya Mungu ya milele katika majira ya dunia. Neema hii bila kutenganishwa inaunganishwa na utume. ***"Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo"*** **Waefeso 4:7**. Neema inaachiliwa kwa kila mshiriki wa mwili kupitia mitume na pia kwa huduma zingine katika **Waefeso 4.**

Neema

Ni uthihirisho wa neema hii kupitia **mwinjilisti** ambayo inatuokoa. Ni uthihirisho wa neema hii kupitia **mchungaji** ambaye analea na kutuimarisha katika imani ambayo inatuokoa. Ni kwa uthihirisho wa neema hii kupitia **mwalimu** ambayo inatupa msingi katika neno linalotuokoa**.** Ni kwa uthihirisho wa neema hii kupitia **nabii** ambayo inatuelekeza na kutuongoza kwa ufunuo wa ndani wa wokovu. Ni kwa uthihirisho wa neema hii kupitia **mtume** ambayo inatuleta katika utimilifu wa wokovu.

Kila mhuduma katika huduma tano, aliyepeanwa na Kristo ni kipawa cha neema ambayo inaachilia neema ya Mungu kwa washiriki wa mwili. Wandugu wengi wamebarikiwa na kuchangamka kushiriki katika matukio ya injili ya uinjilisti wakati **mwinjilisti** aliye na karama analetwa katika mji na nafsi zinazaliwa mara ya pili katika ufalme wa Mungu. Hakuna kitu kama neema ambayo mwinjilisti anatembelea na neema hiyo ni yakuambukiza. Sisi wote tunakuwa na uinjilisti wakati mwinjilisti anahudumu miongoni mwetu.

Wengi wanabarikiwa wakiwa sehemu ya ushirika ambao unaongozwa na mchungaji aliye na kipawa. Huduma ya **mchungaji** inaachilia neema spesheli kwa watu wa Mungu, ambapo wanajihisi wakiwa na usalama kupendwa katika ushirika.

Wengi wetu wanapata njaa ya neno la maarifa ya ndani ya neno la Mungu na wengine wetu tumebarikiwa kumpata **mwalimu** wa neno aliye na kipawa. Ambaye analeta uzima na nuru juu ya neno anapolifungua neno. Kipawa hiki kinashirikishwa kupitia nyenzo zilizoandikwa.
Nabii aliye na kipawa anatafutwa sana kwa kuwa kuna neema kubwa inayo achiliwa kwa wandugu wakati nabii miongoni mwao anahudumu neno la Mungu na kuleta mwelekeo na ufahamu kwa kanisa na kwa waumini binafsi.

Kila kipawa cha huduma kimepeanwa na Kristo kuhudumu neema katika mwili. Tukiwakosa **mitume** tunakosa sehemu muhimu ya neema ya Mungu ambayo amepeana kanisani mwake ya ***"kuwakamilisha watakatifu"*** **Waefeso 4:12.**

Utume

Neno utume ni ***apostole*** kutoka kwa kitendo ***apostello***, kutenga, kutuma; ***apostole*** inamaanisha kutuma, hivyo ni, haswa kutoka kwa *apostolate*, ikitafsiriwa utume. Neno hili linapatikana katika **Matendo 1: 25** katika ombi la kuuliza chaguo la Mungu kati ya Yusufu na Mathiya ***"ashike mahali katika huduma hii na utume huu, alioukosa Yuda***". Utume hapa unarejelea wito haswa na kuwekwa kama mtume wa Mwana- Kondoo wa mmoja ambaye alikuwa ameendana na Yesu na mitume wengine ***"kuanzia tangu ubatizo wa Yohana, hata siku ile alichukuliwa kwenda juu"*** **Mdo 1:22.** Huu ulikuwa ni utume maalum ukiwa na uhitimu spesheli.

Katika **1Wakorintho 9:2,** Paulo anasema waumini ***"ni muhuri ya utume wangu katika Bwana".*** Muhuri wa huduma ya utume wa mtu ni wandugu ambao wanaendelea katika imani na katika huduma kama tunda la utume fulani. Mtume anaamuriwa na tunda la huduma.
Kisha katika **Wagalatia 2:8,** Paulo anasema kwamba Kristo ***"aliyemwezesha Petro kuwa mtume wa waliotahiriwa ndiye aliyeniwezesha mimi kwenda kwa mataifa***". Hapa utume unazungumzia eneo la huduma, katika himaya ya jitihada. Ambapo hakuna yeyote aliye na eneo kubwa la utume leo kama Petro na Paulo, kuna maeneo wazi ya huduma kwa kila mtume ama kikundi cha mitume na hii inatakiwa kujulikana na kuungwa mkono pande zote mbili.

Wakati neema inaunganishwa na utume matokeo ni ***"mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani kwa ajili ya jina lake".*** Utume huu unazungumzia tume spesheli inayopeanwa na Kristo kwa mitume; inahusu jukumu fulani aliyowapa mitume. Utume ni wa kipekee na ndio huduma ya msingi inayopatianwa na Kristo kwa kulijenga kanisa. Ni kupitia mitume kimsingi analijenga kanisa aliyoongea juu yake katika **Mathayo 16:18,** na ni kupitia mitume ambapo kanisa inatayarishwa na neema na kuachiliwa kutimiza tume.

Mitume Wanahudumu Maisha ya Kupaa

"***Hivyo husema: 'Alipopaa juu aliteka mateka, akawapa wanadamu vipawa. Basi neno hilo, Alipaa, maana yake nini kama sio kusema kwamba yeye naye alishuka mpaka pande zilizo chini za nchi? Naye aliyeshuka ndiye yeye aliyepaa juu sana kupita mbingu zote, ili avijaza vitu vyote. Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu"*** **Waefeso 4:8-11.** Ni wazi kutoka kwa aya hizi kwamba huduma tano ni karama za kupaa. Zilipeanwa kanisani baada ya kupaa kwake Kristo. Hata mitume thenashara wa Mwana- Kondoo hawakupokea kipawa cha huduma ya mtume mpaka Roho Mtakatifu alipowashukiwa katika chumba cha juu. Walikuwa wamefundishwa na kutayarishwa kwa huduma na Yesu lakini karama ya huduma ya mtume ni karama ya kupaa ambayo Kristo alipeana baada ya ***"kupaa juu sana kupita mbingu zote***". Yohana mbatizaji alijua kwamba kila karama ya huduma iliyo kubalika hutoka Mbinguni. Alisema ***"hawezi mtu kupokea neno lo lote isipokuwa amepewa kutoka kwa Mungu"*** **Yohana 3:27.**

Karama za Huduma ni kwa Kuchaguliwa na Mungu

Wengine wanaongea kuhusu karama ya huduma tano ikiinuka kutoka wengi wa wazee katika mji. Kunaweza kuwa na karama ya huduma tano ya uongozi wa mji tayari lakini twatakiwa kuwa makini kujua kwamba kila mmoja katika huduma ajue wito wake na kuchaguliwa na Mungu katika Kristo. ***"Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu***" **1 Wakorintho12:28**. Kuna mpangilio wazi wa kuchaguliwa ambao umewekwa katika aya hii. Huduma hizi zote zinakuja pamoja katika baraza

la kitume kama rika. Hata hivyo, uongozi wa kanisa uliimarishwa katika kila mji katika maandiko na wazee waliochaguliwa /na kuwekwa wakfu na mitume katika kila mji. Kinachokosa katika miji mingi waleo ni wazee wa kila mji na ambapo pana wazee wa mji wanaoinuliwa, ukosefu wa mitume ambao ndio akina baba wa wazee. Ni uhusiano huu wa wazee ukiwa na akiwa na baba wa kitume aliye tumwa na Kristo ambayo inaleta wazee katika ufahamu wa uwana na katika mahali pa kuwa chini ya uangalizi na katika uhusiano wa kuwajibika.

Karama za huduma za Kristo zinakuja kutoka mbinguni, sio kutoka ulimwenguni. Nilipookoka mnamo mwaka wa 1994, nilijua nimeitwa na Kristo kuwa muhubiri. Kama nilivyoshiriki katika dibaji katika kitabu hiki, miaka yangu kwanza katika huduma ilikuwa na changa moto na kutimizwa kama nilivyo hudumu katika shule za kikristo, utawala wa kanisa, kuyachunga makanisa na uchungaji wa uinjilisti katika chuo kikuu. Lakini katika miaka hiyo kumi sikuelewa hakika wito wa huduma yangu; wala sikujua chaguo la Mungu kwangu. Ilikuwa ni mwaka wa 1994 ambapo nilialikwa katika baraza katika kanisa la mahali pamoja hapa Toowoomba ambapo nilitambua ya kuwa Kristo amenikirimia kuwa mwalimu. Ilikuwa ni udhihirisho wa karama ya upao iliopeanwa na Kristo katika kupaa kwake. Vivyo hivyo ni kristo aliyeniita mwisho wa mwaka wa 1997 kuanza kuandaliwa kwa huduma ya mtume. Ni ukweli mkuu kujua kwamba mmoja ameitwa na kupewa karama na Kristo kutumika katika huduma na kujua haswa karama ya huduma ambayo mutu amepokea.

Mitume ni Huduma ya Muhimu ya Msingi

"Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejegwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho" **Waefeso 2:19-22**. Maandiko haya yanatufundisha mengi kuhusu muundo wa ujenzi wa kanisa. Jengo lazima liwe na misingi. Msingi halisi ni Kristo (**1Wakorintho 3:11),** na jengo lote ni lazima lijengwe juu yake, hivyo ni juu ya ufunuo wa imani "***Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai"*** **Mathayo 16:16.** Yesu ameimarisha huduma ya mitume na manabii kama msingi ambao kanisa linajengwa. Ni huduma ya mitume na manabii, kupitia ufunuo ambao wamepewa ambayo inaleta mafundisho ya msingi wa imani. Kumbuka Yesu alitambua kwamba kukiri kwa imani ndani yake kama Kristo ilikuwa ni ufunuo kutoka mbinguni, na kisha Yesu akampa Petro msingi wa kiutume katika kulijenga kanisa lake. Katika siku zetu tunawahitaji mitume na manabii kuimarisha na kujenga kanisa juu ya msingi wa ufunuo wa imani katika Kristo Yesu.

Kristo Jiwe Kuu la Pembeni

Jiwe la pembeni linawekwa juu ya msingi ambao unawekwa kwanza. Hiyo inamaanisha kanisa ni lazima liimarishwe juu ya msingi wa huduma ya kitume na kinabii kabla ya jiwe kuu la pembeni liwekwe vyema. Jengo lote linaungamanishwa pamoja katika Kristo, jiwe kuu la pembeni. Jengo hilo, ambalo ni kanisa linakua kuwa hekalu takatifu: kanisa la ulimwengu kote, mwili mmoja (**Waefeso 4:4).** Hekalu hii ndio kanisa lote la Yesu Kristo lakini **aya 22** inaonyesha jambo lingine la 'kanisa la mahali pamoja', ambapo 'wewe', iwe katika Efeso, ama kangemi, ama mji katika taifa lingine, tunajengwa pamoja tuwe makao ya Mungu katika Roho. Tu washirika wa, ama mawe yaliyo hai ambayo yanafanya, hekalu la Mungu, lakini pia

tumeunganishwa pamoja katika Roho katika kanisa la mahali pamoja, kama sehemu ya kanisa la mahali pamoja la mji, ambapo tunapatana na Mungu katika Roho (**1Petro 2:5).**

Yesu aliwachagua Thenashara

Katika **Mdo 1** tunawaona tu mitume kumi na mmoja kwa sababu ya anguko la Yuda. Petro anaongozwa na Roho kuchagua wa thenashara katika ofisi kwa maana palitakiwa pawe na mitume kumi na wawili wa msingi. ***"Na ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili na katika hii misingi majina kumi na mawili ya wale mitume kumi na wawili wa Mwana-kondoo"*** **Ufunuo 21:14.** Wale kumi na wawili walikuwa ndio viongozi wa kanisa la kwanza (**Mdo 2:14, 6:2).**

Namba 12

Namba kumi na mbili inaonyesha serikali ya Mungu. Ni 3 mara 4. Namba 3 ni namba ya utimilifu wa Mungu, ikionyesha utimilifu wa Mungu katika Kristo. Pia ni namba ya shahidi mtimilifu na watu watatu wa utimilifu wa Mungu wote wanashuhudia kikamilifu kwa utimilifu wa Uungu. Namba 4 inaonyesha pande nne ama pepo nne, hivyo ikizunguka dunia yote. Kupitia mitume kumi na wawili 3x4, injili ya ufalme wa Mungu [ufunuo wa Uungu katika Kristo] itatanda kote duniani kupitia kuhubiri kwa injili na kuwafanya wanafunzi [tume kuu lililopewa mitume] (**Mariko 16:15, Mathayo 28:18-20).**

Walikuwa 3

Miongoni mwa 12 Yesu alichagua 3: Petro, Yakobo na Yohana (**Mariko 9:2, Luka 8:51).** Hawa watatu walikuwa wamebahatika kuwa na nafasi ya kuwa na Yesu katika nafasi spesheli. Walikuwa mashahidi wa matukio yasio ya kawaida, ikiwapo kule kugeuzwa. Wakati Yakobo, mtume wa Mwana- Kondoo, aliuawa na Herode nafasi yake ilichukuliwa na Yakobo, ndugu yake Yesu (**Wagalatia 2:9).** Hawa watatu waliitwa nguzo za kanisa la Yerusalemu na Paulo.

Miongoni mwa hizo nguzo tatu za kwanza palikuwa na 1, Petro**,** mwamba, yule ambaye haswa alitumwa na Kristo (**Mathayo 16:18-19).** Wale 12 walikuwa na uongozi katika Petro na kwa wale watatu walikuwa na kiongozi katika Yakobo (**Wagalatia 2:12).**

Paulo Alifanya Kazi na Mitume Wengine

Baadaye Paulo aliinuliwa kama mtume spesheli [mmoja haswa aliyetumwa na Kristo] na alionyesha uongozi wa nguvu wa huduma ya kitume. Tena katika 1 Bwana aliwekeza ndani yake kwa njia spesheli, ili adhihirishe ufunuo wa siri kwa kanisa. Petro alikuwa mtume kwa Wayahudi na Paulo alikuwa mtume kwa watu wa mataifa **Wagalatia 2:8.** Wakati Paulo amesimama peke yake kwa njia nyingi kama mtume alifanya kazi mwanzo karibu na Barnaba ambaye pia alikuwa mtume. Baadaye katika huduma ya Paulo alikuwa na mitume wengi kama wafanyi kazi pamoja naye akiwepo Timotheo na Silwano **1Wathesalonike 1:1, 2:6,** Androniko na Yunia **Warumi 16:7**, Tito na ndugu wengine, ***"wajumbe (mitume) wa makanisa***" **2Wakorintho 8:23** na wengine.

Mitume Wanatakiwa Kufanya Kazi Pamoja

Leo mitume wanaporejeshwa sio wazi kama Bwana ataenda kujidhihirisha kupitia wale mitume ambao waliagizwa mapema wakifanya kazi pamoja ama wakifanya kazi kando katika huduma wa kulileta kanisa katika ukamilifu. Kilicho wazi ni kwamba mitume wanatakiwa kufanya kazi pamoja na kwamba kuna mazungumzo mengi yaliyonyeshwa kwetu na mitume

katika maandiko, ikituonyesha uhakika wa mitume wakifanya kazi pamoja kama wajori ama kama wanaojua maeneo yao ya huduma lakini wakitoa mafundisho yao kwa viongozi wa maeneo mengine ya huduma na hapo pakiwa na kujitoa pande zote, kukubarika na kudhibitishwa

Kanisa Linajengwa Katika Fundisho la Mitume

Fundisho la mitume ni mafundisho ya Kristo. Katika tume Yesu aliwaambia mitume ***"na kuwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi"*** **Mathayo 28:20**. Kanisa la kwanza ***"walidumu katika fundisho la mitume"*** **Mdo 2:42.** Wanafunzi wa kwanza wapya (3000) walidumu kwa mafundisho ya mitume. Hivyo ndivyo walivyopata kujua kuhusu Yesu. Fundisho la mitume ni neno la injili nne za agano jipya. Ni mafundisho ya Paulo **Mdo 18:11**; ni agano jipya.

Mitume Wanatakiwa Kulijenga Kanisa

"Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliopewa mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na angalie jinsi anavyojenga juu yake" **1Wakorintho 3:10**. Mungu anafunua kwa mitume wake ramani, mipango yake, ili kanisa lijengwe. Musa peke yake alipokea ramani hii (muundo) katika agano la kale katika ujenzi wa hema. Paulo anasema kwamba alikuwa mjenzi mkuu mwenye hekima, akipokea kwa neema sehemu kubwa ya ufunuo wa kanisa la agano jipya, lakini inahitaji mitume leo wachukue joho ya kitume na kujenga kanisa kulingana na ufunuo.

Mitume na Manabii Wataona Babeli Ikianguka

"***Furahini juu yake (Babeli), enyi mbingu, nanyi watakatifu na mitume na manabii, kwa maana Mungu amehukumu hukumu yenu juu yake"*** **Ufunuo 18:20.** Mwisho mitume na manabii watakuwepo duniani kuona Babeli ikianguka. Kanisa la Yesu Kristo litakuwa limewekwa katika mpangilio; watakatifu wa aliye juu sana watakuwa wametayarishwa na wakifanya kazi vyema, ***"kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe"*** **Waefeso 4:16**. Babeli itaanguka kwa sababu ya hukumu ya Mungu itakayo tangazwa na kanisa. Kumbuka **Waefeso 3:10**, ***"ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho".***

Kanisa linaporejeshwa na kuimarishwa kama mwili wake ***"anayekamilika kwa vyote katika vyote"*** (ulimwengu wote) **Waefeso 1:23,** mamlaka ya Mungu itaachiliwa kupitia kanisa. Babiloni ikiakilisha yote ambayo sio ya kiungu na yanayopingana na Mungu itaanguka. Kumbuka Yesu aliahidi kwa kanisa lililoshinda nguvu za Yezebeli "***nitampa mamlaka juu ya mataifa, naye atawachunga kwa fimbo ya chuma kama vyombo vya mfinyanzi vipondavyo"*** **ufunuo 2:26-27.**

Tumepuuza mamlaka ya Yesu Kristo na, kwa sababu hatujakuwa na mitume, hatujaweza kupokea mamlaka Yake. mamlaka yake ni kamili: ***"mamlaka yote mbinguni na duniani***" **Mathayo 28:18**; Yeye ni ***"mkuu wa wafalme wa dunia"*** **Ufunuo 1:5**, na "***ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii"*** **Danieli 7:27**.

Mitume ni huduma ya muhimu:

- *Katika kulipanda kanisa,*
- *katika maisha na kuendelea*
- *kwa kanisa la Yesu Kristo.*

Mitume wanahitajika leo:

- *Kuweka kanisa katika mpangilio,*
- *Kurejesha msingi dhabiti,*
- *Kuwaweka wakfu wazee katika kila mahali,*
- *Kuleta ufunuo wa siri,*
- *Kuachilia neema ya Mungu,*
- *Kufanya ishara na maajabu makuu,*
- *Kuleta kanisa katika ukomavu.*

Sura Ya Nne

MITUME NI AKINA BABA

Mungu anatuahidi kwamba siku za mwisho atamtuma nabii
Eliya awarejeshe akina baba.

Hawa ni akina baba sio kwa jina au kwa cheo lakini akina baba walio na moyo wa watoto ambao watakua hata kufikia wana wakomavu, nao wakifanyika akina baba.

Mojawapo ya jukumu la msingi la mitume wanapoinuliwa na yesu leo ni kutoa ubaba kanisani. Mitume ni akina baba! Wana moyo wa baba kwa kanisa kwa maana wamechaguliwa na Yesu kuleta ufunuo wa baba kanisani. Katika mahusiano ya kitume, lengo la baba ni kuwalea watoto wawe vijana ambao watakua na kufikia ukomavu; kisha vijana waingie katika uwana kwa roho wa kufanywa wana. Mahali pa uwana ni uhusiano na baba wa mbinguni. Baba wa kitume amemaliza kazi yake.

Mungu ameahidi akina baba

Katika aya za kumalizia agano la kale, Mungu anasema ***"angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana"*** **Malaki 4:5-6.** Hii ni aya ya kushangaza, ikifunua moyo wa Mungu kwa watu wake. Hamu ya ndani ya Mungu na ilio wazi ni watoto wote wapate akina baba. Duniani kuna jaa ya akina baba wema hata katika jamii za kawaida. Hii imezidishwa katika mataifa ya magharibi kwa talaka za kiwango cha juu na watoto wamezaliwa na mama mmoja, lakini inaonekana katika tamaduni zote watoto wanateseka kwa ukosefu wa akina baba. Hata kwa kulinganisha hata pakiwa na baba mwema, watoto mara kwa mara wanakua wakikosa usalama na bila kujua kitambulisho cha kweli. Mungu anatuahidi kwamba, katika siku za mwisho, atamtuma nabii Eliya, awarejeshe akina baba. Hawa ni akina baba sio kwa jina, ama kwa cheo lakini ni akina baba wenye moyo wa watoto ambao watakua kwa kiwango cha wana wakomavu, na kisha wakafanyika akina baba.

Mungu anatuma Roho na Nguvu za Eliya

'Siku kuu na kuogofya' inayozungumziwa haijafika, na kabla ya siku hiyo, Mungu atamtuma nabii Eliya. Katika **Luka 1:16-17** malaika wa Bwana anatabiri kuja kwa Yohana mbatizaji, akisema "***na wengi katika Israeli atawarejesha kwa Bwana Mungu wao. Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya na nguvu zake, 'ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto', na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa".*** Kwa hivyo uthihirisho wa roho na nguvu za Eliya katika huduma ya Yohana mbatizaji ilikuwa na mambo matatu: 'kugeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, 'kuwatilia waasi akili za wenye haki' na 'kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa'. Hii ilikuwa ikionyesha huduma ya Yohana mbatizaji kutayarisha njia ya kuja kwa Bwana kwa kwanza. Lakini nguvu na Roho wa Eliya yuaja tena kabla ya 'siku ile ya BWANA kuu na kuogofya'. Hii itakuwa kabla ya kuja kwake mara ya pili. Wakati wa kuja kwake Bwana Yesu mara ya kwanza kulikuwa na furaha, na kwaya ya mbinguni ikiimba mbinguni **Luka 2:13-14**. Kwa njia nyingine, hii haikuwa siku ya 'kuogofya'. Kabla ya siku hiyo kuja, Mungu atawarejesha akina baba kanisani. Hawa ni akina baba wa kitume ambao wana moyo wa watu wa Mungu.

Akina baba ni nani?

Mtume Yohana anasema mara mbili ya kwamba akina baba ni wale ***"wanamjua yeye aliye tangu mwanzo"*** **1 Yohana 2:12-14.** Katika kifungu hiki akina baba wako katika mazingira ya ***"watoto wadogo"*** na ***"vijana".*** Matarajio ya Yohana ni kuwe na vizazi vitatu katika kila ushirika wa watu wa Mungu: watoto wandogo ambao wameokolewa tu wakipokea maziwa na kisha mkate wa neno la Mungu; vijana ambao wanaweza kupokea nyama ambao wana ushindi juu ya shetani na sasa wako tayari kushiriki neno kwa wengine; na akina baba ambao ni wale wamekomaa, katika maelezo wakitoa ubaba kwa watoto na pia vijana mpaka watakapofanyika wana waliokomaa.

Mitume ni akina baba

Katika siku hizi za urejesho wa kitume, Mungu anarejesha, kwanza, mitume ambao wanakuja kama akina baba katika mwili. Mojawapo wa jukumu la msingi la mitume wakiinuliwa na Yesu leo ni kutoa ubaba kanisani. Mitume ni akina baba! Wana moyo wa baba kwa kanisa kwa sababu wamechaguliwa na Yesu kuleta ufunuo wa baba kanisani. Yesu alisema kwa mitume wa kwanza ***"awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenituma"*** **Mathayo 10:40**. Huu ni ufunuo wa muhimu ambao umekuwa umekosa kwa maana hatujakuwa na mitume. Tumekuwa na wainjilisti ambao kwa nguvu wamehubiri injili ya wokovu wakituleta kumjua Yesu. Tumekuwa na huduma zingine zikitufundisha na kutuleta katika vipengele vingine vya neema na maarifa ya Bwana wetu Yesu Kristo na wa Roho Mtakatifu.

Lakini ambacho tumepungukiwa ni uhusiano wa ndani wa,
na maarifa ya, Mungu Baba.

Yesu anatuambia wazi kwamba ufunuo wa baba unakuja moja kwa moja tunapowapokea mitume wa kweli ambao wametumwa na Yesu Kristo.

Adamu baba wa kwanza

Katika agano la kale tumeletewa picha ya baba wakuu wengi. Ambapo huduma ya mitume haswa ni ya Agano Jipya, tuna mifano ya nguvu ya baba wa kitume katika agano la kale. Katika mwangaza huu mtume wa kwanza alikuwa ni Adamu na yeye ndiye baba wa wanadamu. Sisi sote kwa asiri, wana wa Adamu. Alikuwa awe baba wa kizazi cha kiungu lakini kifuniko cha utukufu wa Mungu kupitia baba wa wanadamu, Adam, kilivunjika alipoanguka kwa dhambi na Mungu hangerejesha kifuniko hicho kwa mda mfupi. Mungu alikusudia Adamu awe na mazao na aongezeke na aijaze dunia na watoto wa kiungu **Mwanzo 1:28**, lakini Adamu alianguka. Kabla ya kuokolewa tulikuwa wana wa Adamu ambaye alikuwa ni mwenye dhambi na kwa kuwa tulikuwa chini ya kivuli hicho kilichovunjika sisi sote tumezaliwa tukiwa wenye dhambi.

Nuhu baba wa kitume

Kizazi cha Kiungu kupitia Sethi mpaka Nuhu kinaonyesha uhusiano wa baba na mwana. Kila baba alikuwa akimpitishia mzaliwa wake wa kwanza urithi. Ambapo machache yanajulikana ya baba zetu, muundo umewekwa na kiongozi wa kitume aliyefuata katika maandiko ni Nuhu. Nuhu alitumiwa na Mungu kujenga 'Safina ya wokovu' katika kizazi chake na kuleta ukombozi kwa jamii yake, akisha kuhubiri wokovu wa Mungu kwa watu wote. Kisha Nuhu akafanyika kuwa baba wa watu wote. Lakini licha ya kuchaguliwa kwake na kusimama kwake mbele ya Mungu, alikuwa angali mwenye dhambi na hakuweza kukipata kizazi cha kiungu.

Ibrahimu baba wa kweli

Kwa kama mda wa miaka 2000 baada ya Adamu, Mungu alimwinua baba mwingine Ibrahimu. Aliitwa na Mungu aliyebadirisha jina lake kutoka Abramu, ambayo inamaanisha 'baba aliyeinuliwa' kwa Ibrahimu, ambayo inamaanisha 'baba wa wengi' (**Mwanzo 17:5).** Mungu alimchagua mtu huyu katika kujua kwake kwa mbele ya kuwa atatawala nyumba yake vyema na kuwa atawafundisha wana wake kufanya haki na hukumu (**Mwanzo 18:19)**. Alikuwa baba kwa nyumba yake na akawafundisha katika njia za Mungu. Ibrahimu alijulikana kama baba wa imani na sisi ni watoto wake kupitia imani katika Yesu Kristo (**Warumi 4:16)**. Mungu alimpa Ibrahimu ahadi ambayo, kupitia yeye, kila jamii ya dunia itabarikiwa, (**Mwanzo 12:3).** Mungu alikuwa akiweka badala mtume aliyeanguka, Adamu, na yule aliyemchagua Ibrahimu. Kama waumini, tunaye baba katika Ibrahimu. Baraka, zilizoahidiwa kupitia Ibrahimu kwa kizazi chote, hazingewafikia mara moja. Mpaka Yesu alipokuja, ilikuwa imewekwa kwa jamii moja ndogo, wana wa Israeli. Isaaka ni mbegu ya Ibrahimu na kupitia yeye akaja Yakobo. Yakobo ndiye baba wa kabila kumi na mbili za Isaraeli.

Musa Baba wa Taifa.

Baada ya miaka 400, Mungu alimwinua musa ambaye alifanyika baba wa kitume kwa wana wa Israeli. Kupitia Musa, Mungu aliruhusu taifa moja ya watu kuja chini ya kivuri cha kitume ambacho kiliwatenganisha na mataifa mengine yote ambao walikuwa wangali katika kivuli kilichoanguka cha Adamu. Biblia inasema katika (**1 Wakoritho 10:1-2)** yakuwa wana wa Israeli walibatizwa wote katika Musa. Mungu aliwapa sheria na akawafanya kuwa taifa. Walikuwa na 'baba' ;walikuwa chini ya kivuli cha uongozi wa mtu wa Mungu, na walikuwa na kitambulisho; walijitambua. Mpaka siku ya leo dini ya Wayahudi imewekwa kwenye msingi wa sheria za Musa na Wayahudi wangali wanajitaburisha na yeye hhaswa kwa sehemu. Hata hivyo kitaburisho hiki kilikuwa cha mda na hakikuachiliwa Baraka iliyuahidiwa kupitia Ibrahimu kufikia mataifa yote.

Wazo la Kufunika

Kuhusu wazo la kufunika, sio kivuri cha mwanadamu kama ifikiriavyo. Tunapoongea kuhusu Musa akileta kufunika cha kitume kwa watu wa Mungu, ni Mungu akifanya kazi kupitia Musa, kwa utukufu wake, kuwafunika watu wake. Kufunika hiki kinakuja kupitia kuhubiri na kufundisha sahihi kwa neno ambalo Mungu anapatiana. Katika Agano la Kale, ni sheria zilipatianwa kupitia Musa; katika Agano jipya, ni injili ya Bwana wetu Yesu Kristo. Hii haibadiriki! Katika Agano la kale Mungu alikua akiwaita watu wamrudie Mungu kwa neno lililonenwa na Musa; na pia kiunabii ikielekea kwa Agano jipya ambalo litakuja. Katika Agano jipya, kanisa ***"liliendelea kudumu katika fundisho la mitume",*** na Paulo na waandishi wengine wa nyaraka**,** sawa na manabii wa Agano la Kale, wanawaita watu wa Mungu waendelee kwa mafundisho na ufunuo ulioletwa na Bwana Yesu, zote mbili aliyofundisha kwa mitume wa mwana kondoo na, kisha kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu, kwa mitume walioinuliwa baadaye.

Yesu Kristo ni Mtume wa Mungu

Kupitia Yeye Baraka za Ibrahimu zinawafikia wote.

Kuna picha nyingi za kitume kote katika Agano la Kale, lakini picha ya kitume muhimu katika fundisho letu ni Yesu mwenyewe. Ni kupitia Kristo ambapo Baraka ambazo ziliahidiwa Ibrahimu zinaachiliwa kwa wote. Musa angepeana kivuri kwa Wayahudi tu. Kupitia Kristo, ambacho baba wetu Adamu alipoteza kinarejeshwa kwa vizazi vya wanadamu vyote.

Baraka za Ibrahimu ni ahadi ya Roho, ***"ili kwamba Baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani"*** **Wagalatia3:14**. Baraka ya Roho haingekuja mpaka Yesu aje. Ni kupitia Kristo ambapo tunapokea urithi wetu. ***"Kwa kuwa ninyi nyote, mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu",*** na ***"kama ninyi ni wa Kristo, basi , mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi"*** **Wagalatia 3:26,29**. Wakati tunazaliwa mara ya pili tunafanyika wana wa Mungu na urithi ni wetu; lakini wakati tunaingia katika 'uwana' [katika hali ya kufanywa wana] hapo ndipo hakika tunarithi.

Yesu, Mtume wa Mungu, ni Baba Yetu

Yesu ndiye mtume aliyetumwa na Mungu (**Yohana 20:21).** Yeye ni mtume wetu: ***"mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu Yesu"*** **Waebrania 3:1.** Yesu anawakilisha kikamilifu na kumdhihirisha Baba kwetu. Katika Yeye tunakuja kumjua Baba. Yesu anaoyesha ama anazungumzia Mungu kama Baba zaidi ya mara 170 katika injili. Alifanyika 'baba kwa 'watoto' kupitia injili. Anasema, ***"mimi nipo hapa na watoto niliopewa na baba Mungu"*** **Waebrania 2:13.** Yesu ni Baba Yetu. Yeye anawaongoza wana wengi katika utukufu (**Waebrania 2:10)**. Anayafanya haya kwa kutuleta katika ufunuo kamili wa ujumbe wa kitume. Tukimpokea mtume aliyetuma, tunampokea Yeye, na katika kupokea Yeye tunampokea Baba. Alikuwa Mwana kwa Baba yake na ametupatiana kwa Baba. Sisi ni ndugu wa Yesu kwa njia moja lakini, katika uhakika, katika nyumba ya Mungu, Yesu ndiye Baba wetu wa kitume na kupitia Yeye, tunakuja kumjua Mungu kama Baba yetu. Kisha akawachagua mitume kuwa baba katika kanisa ili kuwapitia tunakuja kumjua Yesu na katika yeye, tunakuja kumjua Baba.

Yesu Aliwainua wale Kumi na Wawili wawe Akina Baba wa Kanisa.

Moja ya mitazamo ya huduma ya Yesu ilikuwa ni kuwainua mitume kumi na wawili ambao walikuwa wawe huduma ya msingi na uongozi wa kanisa. Walikuwa ndio baba wa kitume kupitia wale ambao Yesu alizaa kanisa (**1Wakorintho 4:15, Wagalatia 4:19)**. Daima hawa ni huduma ya msingi ya kanisa la milele. Katika siku hizi za mwisho Yesu mara tena anapatiana mitume kwa kanisa lake na jambo kuu la huduma ya kitume ni kwamba mitume walete ubaba kanisani.

Sisi sote tunahitaji 'Baba'

Kila binadamu anahitaji baba. Bila 'akina baba' kuna ukosefu wa amani na neema. Badala kuna kunga'ng'ana ili kujidhibitisha. Kuwa na 'baba' ambaye anapenda bila masharti inaleta amani na usalama na hakika inatuachilia kwa mwito wa Mungu ambapo tunakuja kujitambua. Uthibitisho na kukubalika ambako tunatafuta huja kwetu kutoka kwa Mungu Baba yetu, lakini mara nyingi inatiririka kikamilifu kwetu kupitia baba wa kiroho. Tunahitaji kujua sisis ni wa jamii ya Mungu na huko 'kujua' huja kupitia baba wa kiroho. Kumpokea mtume ni kumpokea Yesu na Baba (**Mathayo 10:40).** Tunapopewa ama kutumiwa mtume na Bwana, na kumpokea huyo, kitu hutendeka. Neema ya Mungu inaachiliwa kutuleta katika ujuzi kamili wa uwana.

Kwa kipindi cha majuma na miezi katika mwisho wa 2002 baadhi yetu katika SHILOH walikuja katika ujuzi wa kutambulika wa ubaba wa kiroho na uwana. Kwa wengine ilikuwa ni ujuzi ulioleta mabadiliko ya maisha; kwa wengine ilikuwa ni mabadiliko ya taratibu, kutambua kwamba mtu amefikia mahali pa ajabu pa usalama na pa neema inayoonekana. Kuufikia uhakika wa uwana, kwa kumpokea baba wa kiroho (mtume) ambaye kupitia Kristo anaachilia neema ya

kufanyika wana, inatuleta katika ufahamu na uhusiano wa ndani na Baba wa mbinguni. Tokea wakati huo, ujumbe wa kufanyika wana na uhakika wa baba wa kiroho umesonga kupitia sisi na wengi wamepata kuingia katika kufanyika wana.

Hivi karibuni, niliongoza kikundi kutembelea kanisa kadhaa za nyumbani lakini huduma kuu ilikuwa ni kwa kanisa moja la nyumbani mpya katika mji mamia ya kilomita kusini ya mji wetu. Tulikuwa kwa kikundi hiki cha watu mara moja tu kabla na wakaanza kukutanika kama kanisa la nyumbani kama matokeo ya kutembelewa huko. Katika kupanga kurudi kwetu tulikuwa tumependekeza waandae semina ya umma kutangaza ujumbe wa kitume. Hata hivyo walituzungumzia na kusema 'twahitaji baba yetu aje na kusema nasi'. Baada ya kuwa na watu hawa kwa siku mbili, tulitambua kwamba Mungu alikuwa akifanya kazi ya ajabu miongoni mwao, akiwaleta katika uhusiano wa usalama nasi na miongoni mwao na kuwapa maono, kusudi na neema ya kuendelea walisema kwangu 'tulijua kwamba baba yetu alipokuja Baba yake angekuja pia' watu hawa wana ufunuo wa ajabu kwa maana walijua kumpokea mtume.

Ufunuo wa Uwana

Ufunuo huu wa Yesu na Baba ambao huja kupitia mitume, unaleta kwa waumini uhakika wa uwana. Mtume wa kweli anatumwa na Kristo na nguvu za urejesho wa Eliya kurejesha ***"mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana"*** **Malaki 4:6**. Uwana inahusu kutembea katika ukomavu. Ni sawa na kupokea roho wa kufanywa wana ambapo tunafikia uhusiano halisi na Baba;

- Sio kama mtoto amjuae baba kama mtoto,
- Sio uhusiano ambao kijana anao kama mtumishi kwa baba,
- Bali uhusiano ambao mwana aliyekomaa anapata na baba.

Yesu ndiye Mwana Aliye Kielelezo

Yesu alihusiana na aliongea kuhusu Baba Yake kila wakati. Hata kama baru baru wa miaka kumi na miwili, alisema ***"hamkujua ya kuwa imenipasa kuwemo katika nyumba ya Baba yangu?"*** **Luka 2:49**. Katika ubatizo wake, Mungu aliongea kutoka mbinguni akimtambua Yesu, ***"wewe ndiwe mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe"*** **Luka 3:22.** Katika **Waebrania 1:5,** uhusiano wa kiungu wa Yesu na Baba yake imetangazwa wazi ikinukuliwa kutoka kwa maandiko ya kinabii ya Agano la Kale. ***"Ndiwe mwanangu, mimi leo nimekuzaa; na tena; mimi nitakuwa Baba yake, naye atakuwa Mwanangu".*** Mungu alitoa ***"Mwana wake wa pekee"*** kwetu (**Yohana 3:16).** Katika maisha yake kama Mwana wa Adamu Yesu alituonyesha jinsi ya kuhusiana na Mungu kama Baba yetu.

Ufunuo wa Baba na Mwana

Mwana wa kweli anatoshana na baba yake

Katika kitabu cha Yohana, Yesu anaeleza uhusiano wake kwa Baba. Baada ya Yesu kuponya mtu katika kisima cha Bethzatha na huyu mtu akawaambia Wayahudi ni Yesu aliyemfanya mzima, wayahudi walitaka kumwua kwa kuponya siku ya sabato (**Yohana 5:1-13)**. Yesu aliwajibu akisema ***"Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi"*** **Yohana 15:17**. Mwana anafanya kila ambacho anamwona Baba akifanya. Maandiko yanaendelea kusema kwamba ***"basi kwa sababu hiyo Wayahudi walizidi kutaka kumwua, kwa kuwa hakuivuja sabato tu, bali pamoja na hayo alimwita Mungu Baba yake, akijifanya sawa na Mungu"*** **aya 18.** Mwana aliyekomaa ni sawa na baba.

Katika uhusiano wa kitume lengo la baba
ni kuwalea watoto wawe vijana wanaokua kwa umri wa ukomavu;
kisha vijana wanaingia katika uwana kwa roho wa kufanyika mwana.
Mahali hapa pa uwana ni uhusiano na Baba wa mbinguni.
Baba wa kiroho amekamilisha kazi yake.

Mwana wa kweli anafanya kazi ya Baba

Kisha Yesu akasema "***mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote atendayo yeye, ndiyo atendayo Mwana vile vile"*** **Yohana 15:19.** Katika Aprili 2004, nikiketi kwa kitanda changu katika hoteli yangu Rwamagana, katika mji wa mkoa wa Rwanda, katikati ya kuondoka kwa nguvu katika huduma ya kitume, nilimsikia Bwana akisema kwangu 'kuanzia leo utakuwa ukitenda kile tu unaona nikitenda'. Hii inasikika ikiwa nyepesi nan i hivyo! Ni ukweli mkuu kuingia katika pumziko na kutenda tu yale ambayo anasema. Kwa wakati ambapo Paulo alimtuma Timotheo kule Korintho kama "***mwana mpendwa na mwaminifu",*** alijuwa kwamba Timotheo atamwakilisha yeye, sio kama mtumishi lakini kama mwana, mwana aliyekomaa akitoshana na baba kwa vile anaweza kufanya kazi zile amwona baba yake akifanya. Kwa njia ile ile, sasa kwa ujasiri ninaweza kuelekeza viongozi ambao wanauliza habari za huduma yetu katika tuvuti yetu kwa mitume katika Afrika ambao ni wana. Katika kufanya hayo ninaweza kusema, 'Mtume huyu wa Kenya atawakilisha huduma ya kitume ya Kristo', vya kutoshsa na kweli kwa yuke kiongozi anayetafuta.

Kuna kazi kubwa kwa mwana.

"Kwa kuwa mwana ampenda baba, naye humwonyesha yote ayatendayo menyewe; hata na kazi kubwa zaidi kuliko hizo atamwonyesha; ili ninyi mpate kustaajabu" **Yohana 5:20**. Moja wapo ya ufunuo wa ambao tunasoma kutembea kama wana ni kwamba 'Baba ananipenda'.

Ananipenda kama mwana Wake, mmoja wa wale Aliowachagua,
na amenichagua haswa kwa "kazi kubwa".

Kumbuka, Yesu alituambia baadaye katika injili ya Yohana kwamba tutafanya kazi kubwa alipoenda kwa Baba (**Yohana 14:12).** Kazi hizi kuu sasa zinatendeka. Katika huduma yetu tumewaona wengi wakiwa na ujuzi wa kugeuzwa wanaposikia ufunuo wa kitume na kupokea Roho wa kufanywa wana. Kushuhudia mhuduma wa ujuzi wa miaka mingi akiwa amebadilishwa mbele ya macho ya watu ni 'kazi kubwa'. Kutembea katika neema ya utume na ufunuo inatufanya kumshukuru Mungu daima. Kama Daudi katika **1 Mambo ya nyakati 17:16,** ni nasema kwa Mungu ***"mimi ni nani, Ee BWANA Mungu, na nyumba yangu ni nini? hata umenileta hata hapa?"*** Kama Daudi, kila mmoja wetu ni mwana wa Mungu aliyechaguliwa na Mungu anatuita kutembea katika uwana, kuzitenda kazi kuu.

Baba anamshuhudia Mwana - Yohana 5:31-39

Nimesema mapema kwamba Yesu ni Baba yetu. Hata kama Baba alivyomshuhudia Yesu kama Mwana, sasa ni Yesu anawashuhudia wana. Wana wa kweli wanamwakilisha Baba. Tunamwakilisha Yesu. Wakati haya ni maalum katika huduma ya mtume, kama Roho na nguvu za Eliya zinarejeshwa watakatifu wote wataingia katika uwana na watadhihilishwa kama wana duniani (**Warumi 8:19)**. Wana wanamwakilisha Baba na Baba kwa Roho wake, anawashuhudia wana. Bwana atatushuhudia kama tunapohubiri na kufundisha maandiko kwa uaminifu. Ni kweli

kwamba tukibaki kuwa waaminifu, kuzungumza neno la Mungu pekee, kisha neno litafanyika mwili tena na litaonekana na watu wote. ***"Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauli langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake" Yohana 14:10.*** Yesu alisema ***"aliyeniona mimi amemwona Baba"*** **Yohana 14:9.** Mwana anashuhudia Baba na Baba anashuhudia Mwana.

Utukufu wa Baba unastahili kuonekana ndani ya Kristo aliye ndani yetu!

Ufunuo wa Baba na Mwana ukitumika

Umoja wa kweli ni kuwa mmoja na Yesu na Baba. Njia ya kipee ya haya kutendeka ni kuwapokea Mitume ambao amewatuma. Kumbuka ***"Awapokeaye ninyi, anipokeya mimi; naye anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenituma"*** **Mathato 10:40**. Mungu alituumba kwa sura yake mwenyewe kulingana na mfano wake mwenyewe (**Mwanzo 1:26),** na mfano huo unafunuliwa kuwa Mungu kama Baba na Mungu kama Mwana; Mungu ni Baba kwa Mwana na Mwana kwa Baba. Mungu analeta kanisa lake katika ufunuo huo: Anaturejesha kwa sura yake na mfano wake. Kwa hivyo anawainua akina baba wa kitume na kuachilia watoto wake katika ujuzi wa kufanywa wana, kwa hivyo wakituleta sisi wote katika uhusiano wa karibu na Mungu.

MUNGU ANAMTUMA ELIYA!

Roho na nguvu za Eliya zimerejeshwa
na zinaachiliwa.

Mitume wanainuliwa

'Neema na Utume' inapokelewa tena
Kutoka kwa Mungu Baba kupitia Kristo.

Hii ni kuwaachilia watoto wa Mungu
Katika uhusiano wa kitume.

Baba wa kitume wamerejeshwa

Wengi wanaufikia ujuzi huu
Wa neema na utume,
Kufunuliwa kama 'wana'.

Sura ya Tano

MTUME NI NINI?

Jambo kuu la kufanyika mtume ni kupokea mwito wa Mungu. Mungu humwita mtu awe mtume; Mungu anamwinua mtu, kwa ujumla baada ya mafunzo na maandalizi, na kumtuma mtu huyo kufanya kazi ya mtume.

Mtume ni aliyeitwa na Kristo na kupewa kipimo kikubwa cha neema na upako na Baba kuleta ufunuo na uhakika wa mapenzi na upendo wa Baba kwa kanisa.

Mitume, wale wakumi na wawili, na wale waliopeanwa kama kipawa cha upao wao ni huduma ya msingi ambayo kanisa la kitume la Yesu Kristo linajengwa.
Kwa hivyo kanisa la siku za mwisho litajengwa tena ju ya msingi wa huduma ya mitume.

Hata kama ilivyokuwa katika mwanzo wa kanisa, ndivyo itakavyokuwa katika kanisa la siku za mwisho – kutakuwa na mitume wengi walioitwa na Bwana.

Mtume ni *"aliyetumwa" ,* mjumbe maalum, yule aliyetumwa kwa jukumu fulani ama wajibu, aliyetumwa na ujumbe; rasmi kamishna wa Kristo [strongs concordance #652]. Halisi, mtume ni aliyetumwa.

Mtume ni aliyetumwa kwa niaba ya mwingine akiwa na mamlaka
ya aliyemtuma atimize kwa kufaulu ambalo ametumwa,
na kikamilifu amwakilishe na afanye ajulikane aliyemtuma.

Jambo kubwa katika kuwa mtume ni kupokea wito kutoka kwa Mungu. Mungu anaita mtu kuwa mtume; Mungu anamuinua huyo mtu, kwa ujumla baada ya miaka mingi ya mafundisho na maandalizi, na kumtuma mtu huyo kufanya kazi ya huduma ya mtume. Paulo mtume alitangaza aliwekwa ametengwa kutoka tumboni mwa mama yake kwa kusudi la Mungu (**Wagalatia 1:15).** Katika wakati wa uongofu wake, Mungu alimfunulia mwanafunzi Anania ya kuwa palikuwa na wito wa kitume wa nguvu katika maisha ya Paulo (**Mdo 9-15-16).** Ilikuwa ni baada ya miaka mingi baadaye, wakati Paulo [Sauli] alikuwa akihudumu katika kikundi cha uongozi wa kanisa la Antiokia, ambapo Roho Mtakatifu alifunua kwamba sasa ulikuwa wakati wa Paulo na Barnaba kuwekwa wakfu katika huduma ya mtume (**Mdo 13-1-3).**

Wengine wanasema kwamba kuna **vipengele vitatu** vimewekwa vya mtume. Hebu tuviangalie vipengele hivyo:

'Yule ambaye amepata kukutana na Yesu aliyefufuka'. Hiyo ina maana gani? Paulo mtume hakumwona Yesu katika mwili lakini alikuwa na ujuzi wa kukutana na yeye uso kwa uso na Bwana aliyefufuka katika kwa njia ya kwenda Demesiki ambayo kwa ghafla ilibadirisha maisha yake. Stefano, mfia imani wa kwanza, alikuwa na ujuzi wa kukutana na Yesu moja kwa moja na Yesu alipopigwa na mawe. Ushuhuda wangu ni kwamba wito wa kitume unahitaji kuwa na msingi wa kukutana na Bwana kuliko wazi ili yule aliyeitwa kama mtume asiwe na mashaka kwamba mwito wake ni kutoka kwa Kristo. Kuma mengi ya kunga'ng'ania ya huduma ya

mtume, kanisani na kwa wahuduma wengine, na kiroho kutoka katika himaya ya roho kutoka kwa nguvu za giza. Nilishiriki, katika utangulizi wa kitabu hiki, ya kuwa nilimwona Bwana na amenituma kwa huduma ya mtume. Huu umekuwa ni ushuhuda wa msingi wa nguvu na nimefaulu kusimama katika mataifa mengi, mbele ya mamlaka na nguvu, na mbele ya umati mkuu na mndogo wa viongozi na kutangaza ya kuwa mimi ni mtume wa Yesu Kristo.

'Ambaye anapanda makanisa'. Katika maandiko sio mitume tu wanapanda makanisa. Katika **Matendo 8**, Filipo alipanda kanisa la Samaria lakini kwa mapema mitume walihusishwa ili waweke kanisa katika mpangilio. Katika **Matendo 11**, baadhi ya wanafunzi walilipanda kanisa la Antiokia lakini, mitume waliokuwa Yerusalemu walipata kusikia haya, walimtuma Barnaba kusaidia kama mtume mjumbe katika uongozi wa kanisa. Pengine inaeleweka vyema kusema mtume ndiye mjenzi mkuu wa kanisa, akiweka msingi na kuweka kanisa katika mpangilio ili kila kanisa la pahali pamoja lifanye kazi na kupata mazao. Ili kanisa lipandwe vyema kunatakiwa na kuhusika kwa mitume na manabii kwa kuwa huduma hizi mbili zinaleta mafundisho na maagizo yanayohitajika ili kanisa lipate kunjengwa vyema (**Waefeso 2:19:22)**.

'Yule ambaye anafanya kazi katika huduma na ishara, maajabu na miujiza'. Kila huduma ya upao inaweza kutarajia kufanya kazi kwa ishara na maajabu. Kwa hakika, kila muumini wa kweli, ambayo kimaandiko inamaanisha muumini wa kitume, anaweza kutarajia kuona ishara na miujiza (**Mariko 16:17-18).** Wito wa mtume inatakiwa kudhibitishwa na Bwana kwa njia hii, haswa, ***"maajabu mengi na ishara zlitendwa kupitia mitume"*** **Mdo 2:43**. ***"Kweli ishara za mitume zilitendwa katikati yenu, katika saburi yote, kwa ishara na maajabu na miujiza***" (**2 Wakorintho 12:12).** Elewa saburi ni tabia ya muhimu ya mtume. Mimi ninashuhudia ya kuwa Mungu anapeana ishara za kutambulika kupitia huduma ya mtume, na ninashuhudia kwamba saburi ndio ufunguo bora ya kujifundisha na kukua ndani yake.

[Nukuu tatu za aina ya giza zimetoka kwa Marvin Vincent zimechukuliwa kutoka kwa Neno Utajiri juu ya 'mitume' katika Spirit Filled Life Bible, kwenye 1 Wakorintho 12:28. maoni mengine ni yangu]

Bwana Huwaita Watu kwa Majina Wawe Mitume

Katika **Mathayo 10,** tunasoma kuhusu kuitwa kwa mitume wa kwanza na Bwana Yesu Kristo. Wito wa kwanza tunaopokea ni wa kumfuata Yesu; kisha panatokea uchaguzi katika huduma spesheli. Kutoka kwa wengi ambao wanamfua Yesu, Mungu aliwaita wale kumi na wawili kuwa mitume wake. Katika **aya 2-4**, Yesu anawataja wale ambao walikuwa wawe mitume wake. Aliwaita kwa majina yao. Walichaguliwa na Yesu baada ya usiku uliotumiwa kwa maombi akizungumza na Baba yake (**Luka 6:12-13).** Wote Luka na Mariko pia wananakili majina ya wale kumi na wawili. Kuna kama mitume **22** waliotajwa katika Agano Jipya na mitume wengine wanatajwa. Ni ya kupendeza kutambua kuwa hakuna wachungaji waliotajwa katika Agano Jipya; walikuwako manabii wachache sana na waalimu waliiotajwa na mwinjilisti mmoja tu. Hata kama ilivyokuwa katika mwanzo wa kanisa, hivyo ndivyo itakavokuwa katika kanisa la mwisho – kutakuwa na mitume wengi wameitwa na Bwana.

Katika siku hizi Mungu amenitayarisha, na huduma hii, kwa uwezo wa kutambua na kutuma mitume. Tunafanya kazi katika maeneo haya kwa umakinifu sana.

Huduma ya mitume sio kitu ambacho tunatamani kwa hiari ama tamaa,
lakini ni kuitikia kwa mwito ulio wazi
na uchaguzi wa Mungu.

Mitume wanatiwa nguvu na Bwana

"Akawaita wanafunzi wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina" (**Mathayo 10:1).** Ishara za mtume, zilizopeanwa na Yesu, ni nguvu juu ya roho chafu na uweza wa kuzitoa, na uwezo wa kuwaponya wagonjwa. Tambua kwamba Yesu amepeana mamlaka ya kuponya "***magonjwa yote na udhaifu"***. Tunatakiwa kuomba na ujasiri kwa kila mtu mgonjwa tukiwa na ujasiri katika mamlaka ya neno.

Ushuhuda wa ishara na maajabu

Ushuhuda wa huduma yetu ni kama ifuatavyo: kutoka mwaka wa 1995-1998, sisi kama kikundi cha huduma tuliona ishara nyingi sana na miujiza kila tulipoenda Australia na ng'ambo. Kimsingi tulikuwa **huduma ya usafiri ya kufundisha** katika siku hizo. Kutoka 1999, majira yalibadilika na Bwana akatuweka 'kwa majificho' kujifundisha huduma ya mitume tukianzia na msingi. Hata hivyo kuanzia mwisho wa 2002, Bwana ameinua huduma hii katika mamlaka ya kitume. Kama matokeo, lengo letu na himizo sio kwa ishara na maajabu ila hari kila mara Bwana hutenda ishara kubwa na maajabu, akidhibitisha neno tulinenalo.

Kwa mfano februali 2003, nilipelekwa kwa kanisa la kijijini Yangon, Myanmar. Wakati wa mikutano ya jioni niliulizwa kuwaombea vijana watatu ndugu, wote wakiwa wanaugua 'saratani ya damu'. Kijana mkubwa alikuwa ameugua. Nilikuwa sina kikudi wakati huo na nikaomba kwa imani kulingana na **Mariko 16:18** ***"wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya".*** Nikarudi Yangon mwezi wa tisa mwaka huo na watenda kazi wawili wakristo kutoka kwa kanisa la kijiji hicho wakaja kukutana nami katika mji kuniambia kwamba wale vijana watatu walipata kuponywa kikamilifu.

Mnamo Septeba 2005 nilikuwa na kikundi Pakstani na, katika jioni moja, nilikuwa mnenaji katika injili ya hadhara katika hema kubwa ambayo ilikuwa imewekwa kwa mikutano fulani. Mamia ya watu walihudhuria mikutano ya usiku na mara tu tulipofika kwa jukwaa, tulitambua mwanamke aliyekuwa mna pepo akivutia umakini mwingi katikati mwa umati. Kikundi changu kikaona haya na kikaanza kuomba na kufanya maombezi na zile tabia za kipepo zikakoma nikaweza kuhudumu. Mwisho wa mkutano kulikuwa na mwaliko wa kuwaombea wagonjwa na wasaidizi wakaanza kumleta yule mwanamke aliyekuwa na pepo. Wakati wa mkutano, Mungu alikuwa ameweka ushawishi ndani yangu kwamba huyu mwanamke atawekwa huru. Hata hivyo, nikawaagiza wasaidizi kumpeleka mwanamke nyuma ya umati kwa kuwa ile tabia ya kipepo ilikuwa imeonekana tena kwa kuwa pepo alinuia kuvuta umakini wa watu na kuingilia uponyaji wa wengine.

Tulipotoka kwa mkutano, mara mojo nilimwendea yule mwanamke aliyekuwa amepagawa na aliwekwa huru haraka sana kwa urahisi kwa kumfunga pepo ndani yake, kwa jina la Yesu, na kumuacha mwanamke huyu akubaliane nami nikiliitia jina la Yesu na kuamuru amtoke. Yule pepo akatoka; tukamsimamisha yule mwanamke kwa miguu na tukamwombea ajazwe na Roho Mtakatifu na akaongea na lugha ya mbinguni. Yule mwanamke alikuwa amepagawa tangu utotoni. Watu, na haswa wachungaji wa mtaa waliokuwa nasi walishangaa. Wachungaji walisema 'hatujaliona jambo kama hili! Huu ndio muujiza mkuu tulioona!

Mitume Wanatumwa kwa Vikundi Vya Watu Spesheli.

Mitume wanatumwa na Bwana. Yesu aliwapa mitume maagizo maalum: watawaendea watu gani, na wataenda wapi. ***"Katika njia ta mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia ya kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya***

Waisraeli" (*Mathayo 10: 5-6).** Paulo pia wazi alitumwa haswa kwa mji ama maeneo. Katika **Mdo 16:6** Paulo alisema ***"walizuiliwa wakikatazwa na Roho Mtakatifu, wasilihubiri lile neno katika Asia (Mkoa wa Rumi)". kisha Paulo akaelekezwa na Bwana kuelekea Makedonia kuhubiri injili kule **aya 10.**

Myanmar

Mapema 1997 nilienda na mchungaji mwingine Myanmar na, tukiwa pale Bwana akaiweka wazi kwangu kwamba nitarudi kwa taifa hio nikivileta vikundi vya wahuduma. Nilirudi Myanmar kwa mara ya nne mapema 1999 na kazi ya kuonekana ikawa ikifunguka kwetu. Vikundi vingine kutoka kwa huduma yetu walikuwa wameenda Myanmar vilevile. Nilijua kutoka miaka yangu ya kwanza katika ujuzi wa ukristo ya kuwa nitakuwa nikihubiri Asia na hii sasa inatimizwa. Sikuwa nimefikilia kwenda Afrika, nikifikilia ya kwamba mataifa ya Uropa watawajibika kuyasaidia makanisa ya Afrika. Hata hivyo, nikiwa Myanmar katika mwaka wa 1999, mwaliko ukanifikia kupitia ujume wa faksi na Bwana akanena nami akiniambia wazi nitaenda Afrika.

Afrika

Kutumwa kwa huduma yangu na Bwana Afrika imekuwa maalum sana. Ikidhibitishwa kwa njia nyingi, na sasa kazi Kenya imekuwa ni jambo letu la msingi ya kazi yetu ya kitume na tunaona mazao ya kudumu. Mitume wengi wameinuliwa Kenya na hata katika Mwaka wa 2006, huduma za kitume zimetoka Kenya. Huduma za kitume zimekuwa kwa Kambi ya wakimbizi ambayo iko Magharibi ya Tanzania na Dar Es Sa-laam, mji mkuu wa Tanzania. Vikundi vimekuwa kwa mji na vijiji katika Sudani kusini. Mtume wa Kenya, George Muteti mara kwa mara anatembelea mataifa manne ya Afrika ya kati, akihuduma katika mji mkuu wa Burudi, Rwanda, Uganda na katika mji mingine na jiji kama vile Goma, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Kuna wana wengine wa kitume ambao wanahudumu kwa nguvu Kenya na katika Mataifa mengine ya Afrika.

Utendaji wa Huduma ya Kitume

Mitume walikuwa wafanye nini?

Walikuwa "***wahubiri, wakisema, 'Ufalme wa mbinguni umekaribia'. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo…" (*Mathayo 10:7-8).** Mojawapo wa jambo kuu ya urejesho ambalo Mungu anahimiza katika kanisa katika siku hizi ni 'kutambua tena ufalme wa Mungu' na kwamba injili ni 'injili ya ufalme wa Mungu [ama ufalme wa mbinguni]'. Karne ya ishirini ilikuwa ni ya uinjilisti wa kisasa, ilioanzia katika mwisho wa karne ya kumi na tisa kwa kuinuliwa kwa Charles Spurgeon katika Uingereza, na pia Amerika, D.L. Moody.

Ni Moody aliyekuwa baba wa uinjilisti wa Karne ya ishirini. Ni Moody aliyeanzisha mialiko ya madhabahu ambapo waliopotea wangekuja kwa wokovu wakisema 'ombi la mwenye dhambi' na kufanywa nishauriwa. Hii ilifanyika njia ya uinjilisti wa huduma zote zilizokuwa zikivuna nafsi. Himizo katika uinjilisti huu ilikuwa wokovu wa nafsi, na kwa njia nyingi, mtazamo ambao sio wa kimaandiko ulikuwa 'kwenda mbinguni' badala ya kuhubiri maagizo kama maneno ya Yesu mwenyewe wakati alipoanza kuihubiri injili ya ufalme wa Mungu, ***"wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuamini injili" (*Mariko 1:14-15).**

Kisha katika **Yohana 3**, Yesu anamueleza Nikodemo jinsi ya kuingia katika ufalme, "Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu" (**3, 5).**

Watu huokolewa ili waingie ufalme wa Mungu sasa,
sio wawe na uhakika wa kwenda mbinguni wakati watakapokufa.

Walikuwa wafanye huduma kwa njia gani?

Walitumwa na Bwana na wakatii maagizo yake (**Mathayo 10:9-15).** Katika tukio hili, Bwana aliwatuma "wala msichukue dhahabu, wala fedha, wala pesa mishipini mwenu", wala kanzu mbili, akiwahakikishia, kwamba watalishwa na kuangaliwa. Katika chakula cha mwisho, Yesu aliwakumbusha wanafunzi habari za wakati aliwatuma bila chochote, kisha akawaambia, katika nuru ya mateso yake yaliyokaribia na kifo, sasa wangehitaji mifuko, na mkoba na upanga (**Luka 22:35-36).** Kutoka kwa vifungo hivi viwili vya maandiko tunajifundisha kwamba Bwana ana njia zake za kushugulika akipatiana haswa kwa kila misheni ambayo anawatuma watumishi wake.

Kuanzia mwanzo wa huduma yetu mwaka wa 1998, tumejua kutoka kwa 'rhema' [neno lililo huishwa] kutoka kwa Bwana huduma yetu itakuwa ya 'kutumwa, salama na itashugulikiwa'.

Kwa miaka Bwana ametufundisha:
kila misheni ya Mungu inaruhusa yake
na anaishugulikia. Mungu ana raslimali ambayo hatujui,
na ana uweza wa kushugulika.

Ushuhuda wa kushugulika kwa Mungu

Wakati mwingine tumetoka Australia na kikundi tukisafiri kwa gari tukiwa na pesa kidogo za mafuta na kadhalika. Na tunapata kushugulikiwa katika mahitaji yote, mara kwa mara tukirudi nyumbani na pesa za kutusaidia katoka huduma. Wakati tunashawishika kwamba Mungu ametutuma kwa misheni kwa mataifa, mara kwa mara washiriki wa kikundi chetu nikiwepo, hatuna fedha mikononi za kusaidia kwa safari**.** Tunahitajika kumtumainia Bwana kikamilifu ili apatiana. Ni zoezi letu, mpaka sasa, kujilipia safari zetu tunapo enda nga'mbo kwa kuwa mwisho wetu huwa ni kwa mataifa ambayo yanakuwa. Hii inamaanisha kwamba, kwa wakati mwingine, tunahitaji pesa za ziada ili tusaidie kuendelea kwa kongamano na washa katika taifa linalotupokea, na pia kukimu mahitaji yetu makazi na usafiri. Hata hivyo, hali hii inabadilika, wakati wandugu katika mataifa wanazidi kuwa wa kitume katika fundisho na utendaji. Hivi karibuni itawezekana kuwatembelea hawa wandugu na waweze kushugulikia mahitaji ya muhuduma aliyewatembelea. Jambo ni kwamba tunatakiwa kumuuliza Bwana na kuondoka kwa mapenzi yake na kwa ujasiri wa kushugulika kwake, kama utakuwa na mkoba wa pesa ama la.

Katika huduma yetu, tunazo shuhuda nyingi za kupeana kwa Mungu za kutushugulikia hapa Australia na kwa safari nyingi katika mataifa. Miaka kadha nyuma, nilipangiwa niende Afrika na kikundi. Nilikuwa nina uhakika kwamba mipango yetu ilikuwa ni kwa mapenzi ya Mungu, lakini, siku mbili kabla tiketi zetu zilipwe, nilikuwa sina pesa kabisa. Nilimtafuta Bwana akanijibu akaniambia 'kopa pesa za kulipia ndege kwa kuwa pesa za safari ya Afrika zinakuja'. Nikamwendea mtu ambaye nilijua atanipa pesa na ajabu Mungu alikuwa amewazungumzia jambo hili. Nikalipa tiketi yangu na nikawa nilihitaji dora elfu moja kwa gharama zote kwa jumla za safari. Siku iliyofuata mtu akaja kwa ofisi na akaongea na mmoja wa watenda kazi nami kwamba urithi umewafikia kwa njia ya nyumba ambayo ilitakiwa kuuzwa. Yule mtu akasema, 'nitatoa fungu katika mauzo yake na umwambie Paulo anaweza kutumia baadhi ya hizo pesa kwa misheni ya Afrika'. Majuma kadha yakapita na haikuwa mpaka siku ya mwisho

ya kufanya kazi kabla ya twende Afrika ambapo mtu huyu alileta fungu la kumi kwetu. Unaweza kufikiri kulikuwa ni kipindi cha changamoto kungonjea mpaka dakika ya mwisho kulipia ndeni yangu na kuwa na pesa za kusafiri lakini Bwana alipatiana!

Mitume watateswa

Mateso yatakuja watu wakiingia kikamilifu katika huduma kwa ajili ya Bwana, hata kutoka kwa jamii. Mitume walikuwa watarajie mteso lakini wasiogope kwa kuwa Roho Mtakatifu atawaambia la kusema (**Mathayo 10:16-20).** Kama huduma ya kitume, tumepitia pingamizi za kweli hapa Australia na katika baadhi ya mataifa ya nga'mbo, kutoka kwa viongozi wengine wa kanisa kwa kuwa tumetoka kufanya kazi ya kitume. Nimeshaitwa mbele ya 'baraza' zaidi ya mara moja na nikazingiziwa kwa kuwapotosha watu kwa mafundisho yangu na matendo. Nimeshatishwa na baadhi ya wahuduma wakaonywa kuhusu huduma yetu, sio kwa sababu ya makosa ya kimaandiko kuhusu fundisho ama matendo katika huduma, lakini ni kwa sababu huduma ya kitume inawapa wengine changa moto katika fundisho na utendaji.

Mitume wanatakiwa kuyatoa maisha yao - Mathayo 10:27-31.

Mitume wanatarajiwa kuhubiri wazi mambo ambayo Yesu anawafunulia. Hii inaweza kulazimu maisha ya mtume. Mtume lazima awe na ushujaa, kwa ujasiri akitangaza kusudi yote ya Mungu. Katika kanisa la wakati huu hii inahusisha kuweka wazi makosa ya 'fundisho la ufanisi' ambayo imeharibu wahuduma wengi na kufanya waumini wengi wawe maskini; inahusisha kutangaza ukweli wa biblia kuhusu dhambi ya ushogo ambayo baadhi ya dini zimetangaza kwamba sio dhambi; inahusisha mafundisho wazi kutoka kwa maandiko kuhusu kuja kwa Yesu mara ya pili na hitaji la kanisa kujiandaa kwa ***"kuvumilia mpaka mwisho"*** **(Mathato 24:13).**

Mitume wanatakiwa kumkiri Kristo Mathayo 10:32-33

Tambua kwamba andiko hili limetumiwa vibaya na wainjilisti wakimuuliza mkristo mpya kuja mbele ya mkutano kukiri Yesu kwa hadhara. Ni mitume ambao wanatakiwa kumkiri Yesu wazi. Kama mtu akifanya haya, Yesu ameahidi kukiri majina yao mbele ya Baba. Kikiri wazi kwa Kristo kutaleta migawanyiko. Nyumba zitagawanyika, lakini hii ni sehemu ya gharama ya kutimiza wito (**aya 34-39)**. Yesu alisema 'wala mtu asiyechukua msalaba wake akanifuata hanistahili' (**aya 38).**

Anayempokea mtume anampokea Bwana

Kuna dhawabu kwa wale wanampokea mtume. Yesu alisema, akinena na mitume, ***"awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenituma***" (**Mathayo 10:40)**. Ukimpokea mtume unampokea Bwana.

Hapa kuna siri: tunapompokea mtume wa kweli wa Yesu Kristo
tunapokea ufunuo wa ndani wa Yesu na Baba; Mwana na Baba!
Ufunuo wa Mungu unajulikana kwa kanisa kwa undani kupitia mitume.

Mtume wa kweli anatiwa nguvu na Kristo kuhudumu ***"Utume"*** kupitia neema. Paulo anasema ***"ambaye katika yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani kwa ajili ya jina lake"*** (**Warumi 1:5).** Mtume sio tu muhuduma mwingine wa huduma tano. Mtume ni yule anaitwa na Kristo na kupewa neema kuu na upako na Baba kuleta

ufunuo na uhakika wa mapenzi ya Mungu na ya upendo wa Baba kanisani. Ni ujuzi wetu kwamba, wakati tunampokea mtume wa Yesu Kristo kwa uhakika tunapokea majaliwa makubwa ya neema ya Mungu ambayo haiwezi kulinganishwa na jambo lolote ambalo lilipokelewa awali. Mmoja anapotii fundisho la mitume, kunakuja ufunuo wa ndani wa Yesu Kristo na Baba. Fundisho la mitume mwanzo linaweza kufundishwa na mitume ambao Yesu anarejesha kanisani leo. Kupitia mitume, Yesu anarejesha fundisho la kitume na ufunuo wa siri. Hata hivyo fundisho la mitume linapofundishwa wahuduma wote wanaanza kufanya kazi na upako wa kitume na ufunuo na kuanza kufundisha fundisho la kitume wenyewe. Fundisho la mitume, kwa urahisi ni kufundisha maandiko kwa usahihi.

Mitume wa Mwana Kondoo ndio misingi

Mitume walikuwa na Yesu kwa mda kabla awataje. Walikua tayari wamefundishwa na Yesu. Aliwajua. Katika Yerusalemu mpya kuta za mji zimejengwa juu ya misingi ya mitume kumi na wawili wa Mwana Kondoo (**Ufunuo 21:14)**. Kuna mitume kumi na wawili tu wa Mwana Kondoo. Katika **Mdo 1:15-26,** tunasoma kuchaguliwa badala ya Yuda; kuhitimu kwa badala huyo: Mmoja ambaye alikuwa na Yesu tokea ubatizo wake na Yohana mpaka siku ya kupaa kwake (**aya21-22).**

Kanisa: Limejengwa katika Msingi wa Mitume

Kanisa linajengwa juu ya misingi ya mitume na manabii (**Waefeso 2:20*).*** Mitume, wale kumi na wawili na wale ambao wamepatianwa kama karama za upao ni huduma za msingi ambayo juu yake kanisa la Bwana Yesu Kristo linajengwa. Kwa hivyo, kanisa la siku za mwisho tena litajengwa juu ya huduma ya msingi ya mitume. Mitume wa siku za mwisho pia wanatakiwa kufanya kazi ya huduma kulileta kanisa katika ukomavu. Wakati kanisa linabaki chini ya utawala wa maaskofu na wachungaji haliwezi, kwa maelezo kuufikia ukomavu kamili. Hii ni kwa sababu kanisa linahitaji huduma zote tano zikifanya kazi kuachilia neema inayohitajika kwa kanisa likue hadi ukomavu.

Hii haijawahusu viongozi wengi kwa kuwa hawaamini kwamba kanisa limewekewa kuja kwa ukomavu wa utukufu katika kujiandaa kwa kuja kwa Bwana. Badala wanaamini na kufundisha kwamba kanisa ‘litanyakuliwa’ kutoka ulimwengu huu katika hali yake ya kutokomaa. Kwa hivyo nia ni: pata watu waokoke na uwaangalie vyema iwezekanavyo katika jengo la kanisa kisasa mpaka Yesu aje alinyakue kanisa.

Funguo za ufalme wa mbinguni

Katika **Mathayo 16:18-19**, Yesu alitangaza wazi atalijenga kanisa katika kukiri kwa imani ndani yake. Kwa maana Petro alikuwa na ufunuo huu, amechaguliwa kama muundo awe mtume wa msingi wa kanisa. Yesu alimpa mtume Petro funguo za ufalme. Mahali pengine wazi katika maandiko panapoongea kuhusu funguo ni ‘ufunguo wa Daudi’, ikitajwa kwanza katika **Isaya 22:22** na kisha katika **Ufunuo 3:7.** Yesu anatambulika kama Yule aliye na funguo wa Daudi. Ni ya busara kuamini kwamba Yesu alikuwa akipatiana kwa mitume kitu cha asiri ya ufunguo wa Daudi.

Petro anazitumia funguo

Katika Yerusalemu - mdo 2:17-41

Petro ndiye aliyechaguliwa na Mungu asimame na wale kumi na mmoja na kuhubiri siku ya Pentekosti kwa matokeo kwamba Wayahudi 3000 waliachiliwa katika ufalme. Katika siku

hiyo Petro alizitumia funguo kufungua mlango wa ufalme wa mbinguni kwa wale wayahudi 3000.

Katika Samaria – Mdo 8:14-17

Baada ya Filipo kuhubiri Samaria kama mwinjilisti aliyefaulu kwa ishara na maajabu, wake na waume pamoja waliamini na kubatizwa lakini walikuwa hawajapokea Roho Mtakatifu. Kanisa katika Yerusalemu lilimtuma Petro na Yohana, wale mitume wawili viongozi, ambao waliwawekea mikono ili wapokee Roho Mtakatifu. Petro alitimiza tume lake kwa kuzitumia funguo kuachilia ubatizo wa Roho Mtakatifu kule Samaria.

Kule Kaisaria – Mdo 10:30-46

Petro alienda kwa nyumba ya Kornelio, mtu wa mataifa, kushiriki injili, akizitumia funguo, alimhubiri Yesu kwao na Mungu akaachilia Roho Mtakatifu kwao. Kisha akawabatiza katika maji. Petro akafungua ufalme wa Mungu kwa mataifa.

Petro alitumika kama mtume wa msingi kwa njia tatu spesheli katika kitabu cha mitume kulitimiza tume. Katika **Mdo 1:8,** Yesu aliwaamurisha mitume kwamba, mara tu wamepokea nguvu za Roho Mtakatifu, walikuwa wahubiri katika maeneo matatu makubwa: kwa Wayahudi Yerusalemu na Judea, kwa Wasamaria na watu wa mataifa.

Paulo mtume alikuwa na funguo hizo hizo.

Paulo kwanza aliitwa kwa huduma ya kitume wakati Anania alitumwa kumponya, na aone kwamba amejazwa na Roho Mtakatifu na amebatizwa kwa maji. Katika **Mdo 9:15-16,** tunasoma kuhusu tume alilopewa Paulo na Yesu kupitia Anania, ***"huyu ni chombo kiteule kwangu, alichukue jina langu mbele ya mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli***". Paulo alizipokea funguo wakati aliwekwa wakfu kuwa mtume. Katika **Mdo 13:1-4,** Paulo amatumwa kama mtume na Roho Mtakatifu afanye kazi ya huduma ya mtume. Kabla ya hayo anaitwa mwalimu. Tayari anatabuliwa kuwa na kipawa cha upao cha walimu. Kanisa lilikutana pamoja 'wakahudumu mbele za Bwana kwa kufunga na kuomba'; naye Roho Mtakatifu akawazungumzia, ***"Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliowaitia".*** Manabii wengine na waalimu wakawawekea mikono na wakawaachilia.

Katika **Mdo 14:1-4,** Paulo na Barnaba wanaanza kufanya kazi kama mitume, wakihubiria na kuwafundisha Wayahudi na watu wa Mataifa sawa, wakipata waumini wapya na wakipata upinzani mkubwa. Na katika **aya 3** tunasoma kwamba Bwana ***"aliyeshuhudia neno la neema yake akiwajalia ishara na maajabu yatendeke kwa mikono yao".***

Katika **Mdo 19:1-7**, tunaona Paulo akitumia funguo za ufalme wa mbinguni kulipanda kanisa la Efeso. Paulo alitumiaje funguo kule Efeso? Aliwahubiria Kristo. Walibatizwa kwa jina La Yesu na wakapokea Roho Mtkatifu; walinena kwa ndimi na wakatabiri. Hawa watu kumi na wawili walifanyika mawe ya msingi ya kanisa la Efeso.

Mitume katika kitabu cha Matendo ya mitume.

Petro akifanya kazi ya uinjilisti.

Katika **Mdo 2:38,** 'Kisha Petro akawaambia, ***"tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"'***. Petro anatumia funguo: akiwaita watu watubu, wabatizwe kwa jina la Yesu na kupokea Roho Mtakatifu. Kwa miaka kadha mungu amenielekeza kuzingatia mikutano ya semina za uongozi kuwaleta viongozi wa kanisa katika ufunuo wa kitume. Hata hivyo wakati wa safari yangu Pakstan 2005, niliulizwa kuzungumza katika mikutano kadha ya krusedi. Nilikuwa

sijafanya kazi ya uinjilisti kwa njia hii kwa miaka mingi. Sasa, kama mtume mwenye ujuzi katika huduma ya kitume, nilipata kwamba nilikuwa na neema kubwa na hekima na ufahamu kuleta injili kwa njia ambayo waliopotea waliokoka, na kuwa hitaji la ubatizo wa maji uliwakilishwa , yakuwa waumini walipata kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na kwamba kulikuwa na chakula kwa kila mtu katika kuhubiri kwa neno. Nilipata mamlaka makuu nikiwa ninafahamu Bwana amenipa ***"funguo za ufalme wa mbinguni"***

Mitume wakiachilia Roho Mtakatifu

"Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu wakawapelekea Petro na Yohana, ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu" **Mdo 8:14-15**. Mtume anatumiwa kuwachilia Roho Mtakatifu.

Miaka kadhaa iliyopita mimi na kikundi tuliulizwa kuhubiri siku chache mwisho wa shule ya mda mfupi (majuma 6) katikati mwa Myanmar. Wanafunzi walikuwa wamefundishwa kikamilifu lakini Mungu alitutumia kuwachilia nguvu za Roho Mtakatifu ***"kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao"*** **(Mdo 8:16).** Baadhi ya hao wanafunzi waliondoka kwa huduma ya nguvu kutoka kwa shule hiyo na tungali tuna mawasiliano nao hata sasa.

Wito wa Paulo

Bwana alisema kwa Anania***, "nenda tu; kwa maana huyu ni chombo kiteule kwangu, alichukue jina langu mbele ya Mataifa, na Wafalme na wana wa Israeli. Maana nitamwonyesha yalivyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili ya jina Langu"*** **Mdo 9:15-16.** Paulo, mtume, alikuwa ameitwa na kutumwa na Yesu, na hii ilidhibitishwa na Roho Mtakatifu katika **Mdo 13:2**. Wakati mwito wa Paulo ulikuwa wa kipekee pia ni kweli kwamba Paulo ni mtume 'kielelezo' kwa sisi wote ambao wameitwa kwa huduma ya kitume. Kwa kuwa Paulo hakuwa mmoja wa wale mitume kumi na wawili wa mwana kondoo, anatuonyesha jinsi mitume wanaitwa leo.

Kanisa la kwanza lililoimarishwa katika Mataifa

Katika **Mdo 10:1-44,** Petro alitumwa na Bwana kwa nyumba ya Korinerio, kwa mtu wa mataifa. Alimhubiri Yesu, Roho Mtakatifu akashuka na akawabatiza waumini wapya. Petro mtume analianzisha kanisa katika 'nyumba'. Tumepata kujua kwa miaka minane ambayo imepita kwamba Bwana ametuelekeza kuanzisha kanisa kwa nyumba. Mara kwa mara katika huduma yetu Australia, ambapo tumejipatiana katika kupanda kanisa nyumbani, tumeweza kuhudumu wokovu, ikihusisha ubatizo wa maji na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tumefanya ubatizo katika bafu ya kuoga, katika bahari ikiwa karibu katika mito, bahari na mabwawa na mabwawa ya kuogelea ya kibinafsi na umma.

Tumeandika kuhusu kanisa la nyumbani mahali kwingine na tunahitaji kuandika zaidi kwa sababu kanisa la kibiblia ni ambalo linakutana kutoka nyumba kwa nyumba. Ni ujuzi wetu kwamba mikutano midogo nyumbani ndio mahali kamili pa kutayarisha kwa kuleta watakatifu kuwa wahuduma ambapo kila mshirika anaweza kufanya kazi katika ushirika wa nyumbani, sio tena 'mkaazi'.

Faida ya kanisa la nyumbani zitakuwa dhahiri wakati nyakati ambazo tunaishi ndani mwake zinaleta mateso na adha ambayo hayawezi kuepukika ya siku za mwisho. Hata katika wakati huu, sauti ya manabii inaanza kusikika, ikiagiza kanisa kwamba wakati wa kuteseka utafikia kanisa duniani kote na kwamba kanisa la magharibi limetayarishwa vibaya kwa mwisho kama huo.

Ni Roho Mtakatifu ambaye Anapaka na Kutuma

"Wakiisha kupelekwa na Roho Mtakatifu" **Mdo 13:4.** Paulo na Barnaba walitumwa kufanya kazi ya huduma ya mtume na Roho Mtakatifu. Kanisa lote linatakiwa kuwa la kitume. Wengi wamefikiri kwa miongo ya hivi karibuni kwamba wamishenari ndio mitume wa kisasa. Hakuna shaka ya kwamba wengi ambao wameenda kwa uwanja wa kimisheni wameitwa na kutumwa na Bwana. Hata hivyo, mazao ya kazi nyingi ya kimishenari imekuwa ni kuimarishwa kwa makanisa ya kidini katika kila taifa duniani. Kwa hivyo, kazi ya kimishenari haijakuwa hakika ya kitume, lakini ya kidini katika tabia.

Tena leo, tunaona Roho Mtakatifu
akipaka na kuwatuma mitume.

Mojawapo wa alama ya huduma yangu binafsi kama mtume imekuwa ni uwezo kwa Roho Mtakatifu kutambua na kupaka mitume. Hii ilianza katika safari Yetu ya Marchi/Aprili 2003 Kenya. Katika safari hii, tulipofundisha katika mikutano na seminari watu wachache waliitikia haswa kwa neno ambalo lilikuwa likieleza urejesho wa mitume na, kupitia mitume urejesho wa akina baba. Kwa wakati Bwana alituonyesha 'upako wa Samweli' juu ya wale ambao walikuwa wameitwa kuwa mitume. Tulifamu kwamba hata kama vile Samueli alimpaka Daudi kuwa mfalme miaka mingi kabla ya awe mfalme, tulikuwa tukipaka watu ambao wameitwa kuwa mitume, tukijua kwamba huduma itainuka kwa wakati. Tokea wakati huo Mungu amezidi kuinua mitume kupitia sisi, AFrika na Asia, na ni wazi ni kazi ya Roho Mtakatifu.

Mitume wanapanda na kuimarisha, na kuchagua wazee

"Hata walipokwisha kuihubiri Injili katika mji ule, na kupata wanafunzi wengi, wakarejea mpaka Listra na Ikonio na Antiokia, wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile Imani, na ya kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi. Na walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila kanisa, na kuomba na pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini" **Mdo 14:21-23.** Mitume wana uweza wa kubabanua wale ambao wanainuliwa katika uongozi.

Fundisho la Mitume huimarisha kanisa

Katika **Mdo 18:1-8,** Paulo alitembelea Korintho na tunaona kazi ya kitume ikiendelea: kanisa linainuliwa, kazi ya uinjiisti inatendeka na neno la Mungu linafundishwa. Huu ulikuwa ni msingi wa kanisa lenye nguvu likiinuliwa katika Korintho, ambayo iliondoka kwa ishara na maajabu. Kazi ya mitume leo kwa jumla sio katika uinjilisti, kwa maana kazi ya uinjilisti imefanyika mahali kwingi na kanisa limeimarika kwa njia fulani. Hata hivyo, kazi ya mitume leo sana sana ni kufundisha neno, fundisho la mitume, kuweka kanisa katika mpangilio.

Kuchagua viongozi

Katika safari Kenya mwaka 2006, nilialikwa kuzungumza kwa semina ya siku moja, jumamosi katika kikundi cha kitume kinachoongozwa na mtume George muteti. Kisha jumapili asubuhi, nikapata nafasi ya kuhudumu katika mkutano ambapo kanisa kadha za nyumbani zilikuwa zimekutanika. George amekuwa akifanya kazi kama mtume kwa miaka michache na alikuwa amewafundisha baadhi ya wanafunzi ambao walikuwa tayari kwa huduma. Ilikuwa ni wakati wa kushangaza: nilimuweka wakfu George kama mtume, nikiwa nimemtuma miaka miwili ambayo ilikuwa imepita; niliwaweka wakfu wachungaji wawili, ambao walikuwa

wakifanya kazi katika kanisa la mtaa katika kikundi hiki cha kitume; niliwatuma watu kama kumi na wanane waume kwa wake kwa huduma tofauti, ikihusiha uchungaji, kufundisha, shemazi, wazee, waabuduji na waombezi wakiunabii.

Kuweka kanisa katika mpangilio

Katika mkutano wa jumapili, nilipata nafasi kuweka mambo kadha wa kadha katika mpangilio, ikihusisha meza ya Bwana, fungu na sadaka; pia kulisaidia kanisa kuongozwa na Roho katika ibada na katika huduma ya karama za Roho Mtakatifu. Nilifundisha neno kuhusu kurejeshwa kamili kwa wanawake katika huduma. George na mimi tulikuwa tukijua wakati Mungu alikuwa anaamrisha na kuwezesha kazi ya ajabu ya kuimarisha na kutia nguvu kikundi hiki cha kitume katika mpangilio wa kitume. Kuweka kanisa katika mpangilio ilihusisha kuweka wakfu na kutuma viongozi. Kutoka wakati huo, nimekuwa nikipokea ushuhuda kutoka kwa George kuhusu mabadiliko kutoka utendaji kazi kwa huduma yake – kuongezeka kwa mamlaka na uelewa wa huduma ya mtume – na kuachiliwa kwa huduma katika maisha ya wale niliowatuma.

Kanisa katika Kambi ya Wakimbizi

Miaka kadha iliyopita, wachungaji wawili kutoka kwa kambi ya wakimbizi wakongomani iliyo magharibi mwa Tanzania walituzungumzia kupitia tovuti yetu. Walikuwa wakiniomba niwatembelee lakini hio haikuonekana ikiwezekana. Hata hivyo mnamo Septeba 2005, mtume Peter Akeki kutoka Kakamega Magharibi ya Kenya, akiandamana na mchungaji, walisafiri kwa kambi hiyo kwa niaba yangu na wapendwa kule walifurahia mno. Kama matokea ya kutembea huku, Peter alirudi Novemba 2005 na akafanya simina ya siku nne katika kambi ya viongozi wa kikristo. Wachungaji na wahuduma, wakihusisha wakuu wa vyuo vya biblia, wakihudhuria semina, mwisho wa siku ya nne Peter aliuliza kama kuna swali lolote, swali lililotokea tu lilikuwa ‘tutapata haya lini tena?’ kuna watu 56000 na wamekuwa pale kwa miaka tisa.

Baada ya semina, wachungaji ambao walikuiwa wakiwasiliana nami wakaniandikia ripoti na ninainukuu: “*kambi imepata ufufuo kuhusu neno ya huduma na urejesho wa kanisa. Rasmi tunataka ujue kwamba sisi tungali watoto na hatujui kitu kuhusu neno la Mungu ijapokuwa sisi ni wachungaji na viongozi wa kanisa, kwa sababu ufahamu wetu ungali chini.*

Tunaamini kwamba Mungu ametukubalisha tuwe wakimbizi kwa kusudi. Hii inatuwezesha kufanyika wanafunzi, kutoka kwa uwanafunzi hata kwa watumishi na kisha wana. Hebu tukiri kwamba kanisa DRC limepoteza mpango ambao sasa tunatafuta. Wamishenari waliotukoloni hawakuhubiri injili wakitangaza ufalme wa Mungu katika uwazi wake. Hata hivyo jambo tu ambalo linaweza kurejesha mambo yote ni kanisa kutumia mafundisho ya kitume ambayo yana nguvu za kiroho na kuhamashishwa na Roho Mtakatifu”

Kwa maombi ya viongozi katika kambi, Peter alirudi kufanya semina Machi 2006 na, pia kwa ombi la viongozi na kozi spesheli ya mafundisho imewekwa. Kozi hii inahusisha miongozo tisa (hizi ni miongozo ya kufundisha ambazo zimetolewa na Revival Ministries Australia. Na muhtasari wa kozi unaweza kupatikana katika kiabatisho cha kitabu hiki). Kozi itamalizika mwisho wa mwezi wa Noveba na Peter atarudi Julai na Kisha Noveba kwa semina zingine na kwa kuwafunzu wanafunzi waliohitimu mwisho wa Noveba .

Muundo wa Waefeso

Katika **Mdo 19:1-7**, misingi ya imani ilikuwa inawekwa katika maisha ya watu kumi na wawili na kupitia hao kanisa lilipandwa Efeso. Katika miezi ya mwanzo wa huduma ya Paulo Efeso, aliimarisha kituo cha mafundisho ya kitume katika shule ya Tirano akifundisha huko kila siku**.** ***"Mambo haya yakaendelea kwa mda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani"*** **aya 10**. Huu ndio mfano wa kwanza wazi wa shule ya mafundisho ya kitume, ambapo mtume aliendelea kufundisha neno, akifundisha wahuduma wengi na kuwatuma nje wakati wa shule kufanya uinjilisti katika mkoa wote wa Asia. Huduma ya Paulo Efeso ilikuwa na sifa za ishara kuu na maajabu lakini, hata zaidi sana ***"neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu"*** **aya 20.**

Kanisa Efeso lilikua kuwa kanisa lenye nguvu ya kitume na uinjilisti likiwa na karama zote za huduma zikifanya kazi. Katika **Waefeso 4:11,** huduma tano zimewakiliswa wazi na kusudi ya huduma tano imeonyeshwa katika **aya 12-16.** Kanisa la Efeso ndio muundo wa kanisa katika maandiko. Tuna habari nyingi kuhusu kanisa hili kuliko lingine na ni katika waraka wa Efeso ambapo Paulo anajulisha sana kuhusu ufahamu wake wa siri ya kanisa, hivyo ni, kufikia kujua asiri yake ya kweli. Katika siku hizi za mwisho, Bwana mara tena analiinua kanisa lake duniani na ni kulingana na muundo wa maandiko.

Sehemu ya muhimu ya huduma ya kitume

ni kujulisha tena muundo

ambao umefunuliwa katika maandiko

kulingana na vile kanisa

lazima liimarishwe na lijengwe.

Sura ya Sita

TABIA ZA HUDUMA YA KITUME

Tunatambua kwamba Yesu hakuchagua manabii kumi na wawili, wainjilisti kumi na wawili, wachungaji kumi na wawili ama waalimu kumi na wawili; kwa kukukusudia Aliinua huduma mpya na akawekeza kwa huduma hiyo upekee wa huduma yake ya utume.

Kazi ya msingi ya Yesu kama mtume wa Mungu ilikuwa kuwainua mitume na ni kupitia tu huduma ya mitume ambapo kanisa mwishowe litajengwa kulingana na muundo wa maandiko.

Kabla ya Yesu kupaa, Alitoa mamlaka yake kwa mitume na, kupitia hao, kwa kanisa lote. Maandiko hayajui kuhusu makanisa ambayo hayafuati mamlaka ya kitume. Kwa hivyo ni ya busara kusema kwamba kanisa la Agano jipya ni ya kitume.

Mtume anatakiwa kuishi maisha ambayo ni kielelezo kwa wengine. Yeye anatakiwa kuwa na uwezo wa kusema 'nifuate kama vile mimi ninamfuata Yesu.'

Yesu aliwachagua mitume kumi na wawili

Katika sura hii, tutafanya somo fupi ya Agano Jipya kuona tabia za huduma ya mtume. Huduma ya mtume ni ya kipekee kwa Agano Jipya. Wakati sasa tunaweza kuangalia nyuma kwa Agano la kale na kuona mfano wa kiongozi wa kitume na kujifundisha mengi kuhusu mitume kwa kufanya haya. Yesu haswa alitumwa duniani kama mtume wa Mungu na, kama mtume, Huduma yake, ilikuwa kuwainua wale kumi na wawili waliochaguliwa katika huduma ya utume. Tunaona kwamba Yesu hakuchagua manabii kumi na wawili, wainjilisti kumi na wawili, wachungaji kumi na wawili ama waalimu kumi na wawili; kwa kukusudia aliinua huduma mpya na akawekeza katika huduma hiyo upekee wa huduma Yake Mwenyewe.

Mafundisho ya kukoma ni ya uongo

Agano Jipya lote ni ufunuo wa Yesu Kristo na kanisa Lake. Biblia yote ni neno la Mungu na Agano Jipya linaleta utimilifu wa yale yoye yaliyonenwa katika agano la kale. Agano Jipya ni hati ya kitume na 'msingi' wa fundisho la biblia na utendaji kanisani leo. Kwa bahati baya, tumepitia karne za 'fundisho la kukoma' ambalo linasisitiza hakuna mitume leo. Walimu kama hao wanadai kwamba hakuna ubatizo wa Roho Mtakatifu leo, hakuna uponyaji, hakuna miujiza, hakuna kukemea mapepo na kadhalika. Hata hivyo, hata miongoni mwa wale wamekubali urejesho wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuna wengi ambao hawakubali urejesho kamili wa karama za huduma tano katika **Waefeso 4:11** zaidi hata miongoni mwa wale wanakubali kwa njia fulani urejesho wa karama za huduma tano, kuna ukosefu wa kuelewa na kukubali mitume kama ilivyo fundishwa wazi katika Agano Jipya ila hali, Jambo la Yesu la msingi, kama mtume wa Mungu, ilikuwa kuwainua mitume na ni kwa huduma ya mitume tu ambapo kanisa litanjengwa kulingana na muundo wa maandiko.

Katika **Yohana 17:4-19**, Yesu anahusiana na Baba yake kuhusu kazi ya kitume ambayo Baba alikuwa amempa. Kumbuka katika **Waebrania 3:1** twatakiwa kutafakari ***"Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu".*** Kazi ya Yesu ya kitume ilikamilika (**Yohana 17:4**)

na kazi hiyo ilikuwa kuwainua mitume kumi na wawili, akiwaleta hao wanafunzi mahali ambapo walikuwa tayari kutumwa kama mitume (**Yohana 17:18).**

Zifuatazo ni tabia za huduma ya mitume zilizotolewa katika maandiko:

Mitume wanaitwa kwa jina na wanatumwa na Bwana

Katika **Mariko 3:13**, Yesu alienda juu mlimani na akawaita 'wale aliowataka'. Katika **aya 14-15** ***"akaweka watu kumi na wawili wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, tena wawe na amri ya kutoa pepo*****".** Kisha akawataja kumi na wawili (**aya 17-19).**

Hao wa kwanza kumi na wawili (Mathiya akichukuwa nafasi ya Yuda) ndio mitume kumi na wawili wa mwana kondoo (**Ufunuo 21:14).** Hata hivyo, katika Agano Jipya angalao mitume wengine kumi na mmoja wanatajwa na wengine wengi wanatajwa. Leo, Bwana anaita na kuchagua mitume. Ni kwa Roho Mtakatifu ambapo Bwana anafanya hivi. Katika **Mdo 13:1-4** Roho Mtakatifu anawatambua Sauli na Barnaba kutengwa na kutumwa kama mitume. Hawa ndio wawili wa kwanza miongoni mwa mitume wa karama ya upao walioitwa na majina wawe mitume.

> [mitume waliotajwa katika Agano jipya: 12 katika **Mathayo 10:2-4**; Mathiya katika **Mdo 1:26;** Paulo na Baranaba katika **Mdo 13:2/14:14***;* Androniko na Yunia Katika **Warumi 16:7** na mitume wengine ambao wanajulikana; Apolo katika **1Wakorintho 1:12, 4:5-6,** Tito katika **2 Wakorintho 8:23***;* Yakobo katika **Wagalatia 1:19**; Epafrodito katika **Wafilipi 2:25;** Siliwano na Timotheo **1Wathesalonike 1:1, 2:6;** wandugu wengine wanne wa Bwana **1 Wakorintho 9:5; Mariko 6:3]**

Mitume wanatumika kupanda makanisa na kuweka misingi

Yerusalemu – katika **Mdo 2,** Petro mtume anaweka misingi ya kanisa katika siku ya Pentekosti. Aliwaambia watu ***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu".*** Elewa Petro anarejelea misingi tatu kati ya minne ya kwanza iliioorodheshwa katika **Waebrania 6:1-2.** Haya ndiyo mafunzo ya kwanza ama ya msingi ya Kristo ambayo kanisa lazima lijengwe juu yake kabla ya kuenenda katika ukomavu. Msingi wa pili katika orodha umekosa, 'Imani kwa Mungu'; msingi huu tayari umekwisha wekwa kwa sababu wasikizaji siku ya pentekosti walikuwa wakifanya kazi katika Imani kwa neno ambalo walilisikia.

Samaria – katika **Mdo 8**, mitume Petro na Yohana wanatumwa Samaria ambapo Filipo alikuwa akihubiri. Waliwaombea waumini wapya kwamba wapokee Roho Mtakatifu **aya 15** kupitia kuwekea mikono **aya 17.** Filipo alikuwa tayari amekwisha weka misingi mitatu ya kwanza ya toba, imani na ubatizo.

Kaisaria – misingi ilikuwa imewekwa katika **Mdo 10** wakati Petro alihudumu neno katika nyumba ya Kornelio. Alimhubiri Yesu kwa watu wa mataifa, Roho Mtakatifu akaja na Petro akawaamuru wabatizwe. Kanisa lilipandwa.

Efeso – katika **Mdo 19:1-7,** mtume Paulo alitumiwa kuimarisha kanisa katika Efeso. Wanafunzi walibatizwa katika jina la Bwana Yesu kwa maana waliamini mahubiri ya Paulo kumhusu Kristo. Wanafunzi hawa walikuwa wafuasi wa Yohana tayari lakini walitubu [kubadilisha mawazo yao] na wakamwamini Yesu. Kisha Paulo 'akawawekea mikono, Roho Mtakatifu akawashukia, na wakanena kwa lugha na kutabili' **aya 6**.

Kuangalia misingi

Sehemu kubwa ya mtume leo ni kuangalia misingi kwa sababu, katika sehemu nyingi, kanisa tayari limepandwa, lakini pasina kutambua vyema kwa muundo wa kitume na utendaji wa maandiko. Kwa hivyo waumini wengi hawajawekwa vyema katika imani.

Mtume Peter Akeck wa Magharibi ya Kenya alikuwa ameulizwa ahubiri katika ibada ya asubuhi jumapili na mchungaji ambaye alikuwa amemsikia akihubiri katika semina. Kanisa la mtaa lilikuwa kusanyiko ya watu kama 120 wazima. Peter akaandika kwa barua pepe mnamo Februari 15:2006, "*Roho aliniongoza kushiriki mambo ya msingi sana kutoka* **Mdo 2:36-42.** *Kanisa lote likashangaa kwa ufunuo wa ajabu katika aya hizo ambazo wamezipitia tu kwa haraka. Mwisho wa ujumbe, zaidi ya watu hamsini walikuwa tayari kwa ubatizo, wasitake kwenda nyumbani kuleta mavazi ya kubadirisha. Ushawishi ulioletwa na ufunuo wa ubatizo ni nini, aliwazidi na kwa mara ya kwanza katika maisha yangu, niliyapeleka watu zaidi ya hamsini kwa mto – umbali wa kilomita mbili – na kuwabatiza. Wote – wanawake wakongwe, wanaume, mabinti wachanga na vijana – walifurahi mno, walienda nyumbani wakitiririka maji.*

Hii ilikuwa ni baada ya zaidi ya watu 100 wazima kukubari kwamba walikuwa hawajajazwa na Roho Mtakatifu na nikawaombea kwa kuwawekea mikono na kama watu 80 walijazwa kwa ajabu na wakanene kwa lugha na wakamtukuza Mungu". Mtume anaweka msingi katika mpangilio.

Mitume wanapatiwa nguvu na Yesu za kuponya kutakasa, kuwafufua wafu na kutoa mapepo.

Katika **Mathayo 10,** yesu alituma wale kumi na wawili na akawaamuru katika **aya 8** ***"pozeni wagojwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo"*** hii imerudiwa katika **Mariko 3:15**, ambapo Yesu aliwapa mitume ***"nguvu za kuponya magojwa na kutoa mapepo".*** Hii ni sehemu ya tume kuu ambayo ilipewa mtume kabla ya Yesu kupaa mbinguni, ***"na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kuvisha hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagojwa nao watapata afya"*** **Mariko 16:17-18.** Nguvu za kuwaponya wagonjwa na kutoa mapepo kisha inapewa waumini wote: Kanisa lote, hatimaye, linatakiwa kuwa la kitume.

Huduma ya mtume ina sifa za ishara na maajabu. Katika **Warumi 15:18-19,** Paulo anaandikia kanisa katika Rumi, ***"maana sitathubutu kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yangu, Mataifa wapate kutii, kwa neno au kwa tendo kwa nguvu za ishara na maajabu, katika nguvu za Roho Mtakatifu; hata ikawa tangu Yerusalemu, na kando kando yake, mpaka Ililiko nimekwisha kuihubiri injili ya Kristo kwa utimilifu".*** Injili bila nguvu sio injili kabisa. Kumbuka ya kwamba Paulo, katika **1Wakorintho 2:1-5,** anashuhudia nguvu za Mungu ambazo zilionyeshwa na Roho Mtakatifu katika Korintho.

Mitume wanatumiwa na Mungu kuachilia Roho Mtakatifu

Katika **Mdo 8**, Filipo alienda Samaria na akamhubiri Kristo kwa watu. Wengi wakaitikia, wakaamini na wakabatizwa. ***"Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea RohoMtakatifu"*** **Mdo 8:14-17.** Katika **Mdo 10,** Petro waliwahubiria mataifa katika nyumba ya Kornelio. ***"Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno"*** **aya 44.**

Katika **Mdo 19,** Paulo akaja Efeso na akakutana na kikundi cha wanafunzi na akawauliza kama walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu. Wakajibu ***"hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia"*** **aya 2.** Paulo akawafungulia maandiko na kisha ***"akaweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri"*** **aya 6.** Sio tu mitume ambao wanaweza kuachilia kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa mfano mwanafunzi Anania alimwekea Sauli mikono ili apate kujazwa na Roho Mtakatifu (**Mdo 9:17).** Nilikuwa tu na miezi michache ndani ya Bwana wakati nilimwekea muumini mpya mikono na wakajazwa.

Mitume wana mamlaka kutoka kwa Yesu ya kufunga na kufungua.

"Nami nimekupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni, na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni" **Mathayo 16:19.** Jesu kwanza alizipatiana funguo za ufalme kwa Petro mtume. Tumeandika kuhusu funguo hizi mahali pengine. Katika mazingira ya kufunga na kufungua ni lazima tutambue kwamba hakuna pahali palipotanjwa pa kupigana ama kujaribu kufunga, mamlaka ama nguvu. Yaliotajwa ni katika ufalme wa Mungu na Petro alizitumia funguo hizi kikamilifu kwa kumhubiri Yesu Kristo na kuamuru ubatizo, ikihusisha kupokea karama ya Roho Mtakatifu. Haya ndiyo mazingira ya msingi ya kufahamu funguo hizi na nguvu za kufunga na kufungua. Ya pili, na ingine pekee, wakati ambapo kufunga na kufungua kumetajwa katika **Mathayo 18:18**; hapo mazingira ni ya urudi wa kanisa – kupambana na ndugu ambaye amekataa kutubu dhambi.

Kabla ya Yesu kupaa, alipatiana mamlaka yake kwa mitume na kupitia hao kwa kanisa lote. Maandiko hayajui kuhusu makanisa ambayo hayatembei na mamlaka ya kitume. Kwa hivyo ni ya busara kusema kwamba kanisa la Agano Jipya ni la kitume. ***"Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia, 'nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani"'*** **Mathayo 28:18** na mamlaka hayo inapatikana na kudhihirishwa kwa kanisa la Yesu Kristo. Haya ndiyo mamlaka ya kufunga na kufungua, kufungua mlango kwa ufalme wa Mungu ili watu waingie, wasifungwe na dhambi tena.

Mitume wana mamlaka kusamehe dhambi ama kutosamehe dhambi.

Yohana 20:23 - Wengine wanaweza kuona hii kama kutumia mamlaka 'kufunga na kufungua' na huu ni ufahamu mwema.

Baada ya kufufuka, Yesu alikuja kwa wanafunzi wake, ***"akawavuvia, akawaambia, 'pokeeni Roho Mtakatifu"'***. Katika kuwapatia wanafunzi wake Roho Mtakatifu, Yesu kisha anawaambia kwamba wana mamlaka ***"kuondoa dhambi",*** hivyo ni kusamehe dhambi. Hii ni jambo la nguvu sana ambalo Yesu aliwapa wahuduma wake: hata kama vile alikuwa na mamlaka ya kusamehe dhambi duniani, mitume sasa walikuwa na nguvu za kusamehe dhambi, albeit,/ hata kama ni kupitia injili. Mara kwa mara kusamehewa kwa dhambi ni funguo kwa mtu akipokea uponyaji wake. Kama mtu atabaki bila kutubu, kama Simioni mchawi alivyofanya katika **Mdo 8,** kisha huyu mtu anabaki amefungwa ama akibaki na dhambi zake.

Katika tukio moja, kijana mmoja alikuja kwa mkutano mmoja wa hadhara. Alikuwa na msimamo katika dini ya kikatoleki. Alikuja mbele baada ya mkutano wa maombi. Nikamuelezea kuhusu kazaliwa mara ya pili na nikamuuliza kama naweza kumuongoza katika maombi na kukiri. Alikubali. Kwa tukofanya ombi la wenye dhambi na kumuuliza Yesu aje katika maisha yake. Hakuna kitu kilitendeka. Roho Mtakatifu akanisukuma kuvunja nguvu ya dhambi katika maisha yake. Nikafanya hayo na nikamuongoza ombi la wenye dhambi tena na akahisi Yesu akija katika Maisha yake. Huu ni mfano wa nguvu ambazo Yesu ametupa za kuondoa dhambi.

Mitume wameitwa kwa maombi na huduma ya neno.

Katika **Mdo 6:1-4,** kuliinuka manung'uniko ya Wayahudi wa Kiyunani juu ya Webrania kwa sababu ya wajene wao walisahauliwa katika huduma ya kila siku. Mitume wakaamua kuwachagua watu saba ambao wangeangalia mahitaji haya. Petro akaiweka wazi kwamba huduma kuu ya mitume ilikuwa ni kuhubiri na kufundisha neno la Mungu. Alisema, ***"na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile neno"*** **aya 2-4.** Hapa hakika tumepewa mwangaza kwa asiri ya kweli ya huduma: kwanza muhuduma ni lazima atumie mda akiendelea katika maombi; kutoka kwa maombi hutokea huduma ya neno. Ushuhuda wangu binafsi inadhibitisha haya: kwa miaka huwa ninatumia wakati kwa maombi nikiwa na biblia imefunguka mikononi, nikiomba maandiko na kwa bidii nikimtafuta Bwana. Katika wakati wa maombi Bwana angenipa ufunuo na ufahamu ambayo ningehubiri. Mpaka wakati huu huduma yetu imeimarika kimaombi ikiwa na nyakati zilizotengwa za maombi na nyakati zingine kwa wito wa maombi ya ghafra.

Mitume wanawainua wengine kufanya kazi ya huduma.

Katika **Mtendo 6:1-7**, wengine saba wanainuliwa kusaidia na kazi; wametumwa kwa kuwekewa mikono. Matokeo ya huduma ya kuongezeka ni ***"Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana".***Uongozi wa kweli wa kitume unaweza kufanya maamuzi ya kiungu na maamuzi ya kiungu inaachilia ufifio wa ziada. Usimamizi wa uongozi imetamatishwa na Paulo wakati alimuagiza Tito ***"Ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji"*** **Tito 1:5.** Makanisa mengi wanaweka msingi na mipangilio ya kufanya vitu, ikihusisha kuchagua uongozi katika viwango vya idara na dini. Ni nadra sana kupata makanisa yakifanya kazi katika mpangilio wa kimaandiko na wazee ambao wamewekwa na mtume. Lazima pawe na kuongezeka kwa viongozi na ni mitume ambao wanaanzisha hii na kuiongoza.

Mitume wanatunza, kulisha na kuchunga kundi.

Petro, mtume, alitumwa na Yesu kwa huduma ya mchungaji. Katika **Yohana 21:15-17** ***Yesu*** alimuagiza Petro ***"lisha wana- kondoo wangu", "chunga kondoo zangu",*** na tena "***lisha kondoo zangu".*** Mitume wote watakuwa na moyo kwa kondoo kama akina baba na wataweza kuwafundisha wachungaji ***"litunzeni kundi lote la Mungu"*** **Mdo 20:28**

Mitume wanahudumu kwa hadhara na kutoka nyumba kwa nyumba

Matendo2:42-47. Kanisa la kwanza walifundishwa 'fundisho la mitume' na walidumu kila siku kwa moyo moja katika hekalu na kumega mkate kutoka nyumba kwa nyumba. Mitume wa kwanza walifundisha neno kutoka nyumba kwa nyumba. Kanisa la kwanza kimsingi walikutana katika nyumba. Mitume na, baadaye manabii na wengine katika huduma tano, walifanya kazi nyingi za huduma zao katika kanisa la nyumbani.

Katika **Matendo 20:20,** Paulo akiongea na wazee wa kanisa la Efeso, akiwakumbusha jinsi alitangaza injili kwao na 'kufundisha kwa hadhara na kutoka nyumba kwa nyuma'. Kwa bahati baya, wahuduma wengi leo wanajiinua na hawaelewi asiri kamili ya kanisa, ambayo ni mikutano ya mashirika katika vikundi vidogo wakikutana manyumbani. Wahuduma kama hao wanatafuta makundi na sadaka nono badala ya kujikuza katika kazi ya huduma, ***"kwa hiari, si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo, wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya kielelezo kwa lile kundi" 1Petro 5:2b-3***. Baadhi ya mikutano ya nguvu ambayo tumekuwa nayo imekuwa kwa nyumba. Wakati mwingine hapa Australia tunasafiri kwa kijiji ama mashambani na wandugu wanakusanyika kwa nyumba moja, wengine wakileta

Karavani na hema walale ndani. Tunaendelea kwa ushirika kwa siku mbili ama tatu ama zaidi, na watu huja kutoka kwa mitaa vile vile.

Mitume wanafundisha neno; wakilitangaza kusudi lote la Mungu.

Neno lao ni kama amri, ***"mpate kuyakumbuka yale maneno yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu na ile amri ya Bwana na Mwokozi iliyoletwa na mitume wenu"*** **2 Petro 3:2.** Paulo kama mtume alikuwa na uwezo wa kusema ***"sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu"*** **Mdo 20:27**. Yakobo mtume alilitangaza kusudi la Mungu kwa baraza la Yerusalem. ***"Mitume na wazee wakakusanyika wapate kulifikiri neno hilo"*** **Mdo 15:6**, tena katika **aya 13-21** Yakobo akalinena neno la Mungu 'kama lilivyoandikwa' kutoka kitabu cha Amosi. Hekima hii ya Roho Mtakatifu ilitatua hari ambayo baraza ilikuwa ikipitia.

"Bali kama vile tulivyopata kibali kwa Mungu tuwekewe amana injili, ndivyo tunenavyo; sio kama wapendezao wanadamu, bali wampendezao Mungu anayetupima mioyo yetu" **1 Wathesalonike 2:4.** Mitume wameaminiwa kusudi lote la Mungu. Kwa kuwa mitume wameaminiwa na ujumbe wa Injili kwa njia spesheli, hapo mtume anaongea ukweli wa neno kama mtume, wazee (wahuduma) na wandugu wanatakiwa kulishika kwa makini. Neno la Mitume halitakuwa kila mara ***"kama la kuwafurahisha wanadamu".***

Katika **Waebrania 6:1-2,** misingi sita imeorodheshwa ambayo lazima ifundishwe kabla kanisa kuenenda katika ukomavu. Mtume anatakiwa kuliita kanisa lilejeree msingi, kuhakikisha kwamba imewekwa vyema. Isipokuwa misingi iwekwe vyema, Mungu hawezi kuachilia undani mkuu wa neno lake kwa waumimi.

Katika tume lililopatianwa na Yesu (**Mathayo 28:20*)*** mitume wameamurishwa ***"kuwafundisha kuyashika yote niliowaamuru nyinyi".*** Mitume walifundisha ***"fundisho la mitume"*** **(Mdo 2:42)**. Fundisho la mitume lilikuwa ni neno la msingi ambalo kanisa linajengwa juu yake na iko hivyo hata siku ya leo''. Kama sheria ya Musa ilivyowaongoza maisha ya kanisa la Kale, fundisho la mitume, ni kile kinaongoza maisha ya kanisa la Agano Jipya.

Mtume Paulo alifundisha Korintho***: ''akakaa huko muda wa mwaka na miezi sita akifundisha kati yao neno la Mungu***" **Mdo 18:11**. Katika Efeso, Paulo, ***"akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja jina lake Tirano. Mambo haya yakaendelea kwa mda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana wayahudi kwa wayunani***" **Mdo 19:9-10.** Katika Rumi***, "akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimuendea akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi asikatazwe na mtu"*** **Mdo 28:30-31.**

Paulo alimfundisha Timotheo na akamuagiza awafundishe wengine, ***"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahindi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine"*** **2 Timotheo 2:2**.

Tangia mwanzo wa huduma yetu ya Revival Ministries Australia mnamo mwaka wa 1998 Januari, tulipata maono ya kuwa na kituo cha kufundisha cha kitume, mfano wake ukiwa ni mtume Paulo katika Efeso katika **Mdo 19**. Mungu amewezesha haya yatimie na tumekuwa tukifanya shule za muda mdogo Australia na ng'ambo kwa miaka mingi. Sasa tuko katika hali ya kuanzisha nafasi nyingi za kufundisha.

Mitume wanawaweka wazee wakfu

Mitume waliyatembelea makanisa katika miji tofauti **Mdo 14:21**; kisha ***"walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila kanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika***

***mikono ya Bwana waliyemwamini"* aya 23.** Paulo alimtuma Tito kuwachagua wazee, ***"kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru"* Tito 1:5.** Paulo, kama mtume, alikuwa miongoni mwa wazee waliomweka Timotheo wakfu (**1Timotheo 4:14)** na Paulo anasema haswa alikuwa ameachilia karama kwa Timotheo kupitia kuwekewa mikono. Tunaweza kuwazia kwamba kuachiliwa huku kwa kipawa kulifanyika wakati Paulo alimwekea timotheo mikono wakiwa na wazee. Ni Tabia nzuri kwa kila uongozi wa kanisa la mtaa {Wachungaji/wazee} kumuuliza mzee ambaye wanahusiana na ambaye wanafuata utume wake, awe sehemu ya shughuli za kuwaweka wahuduma waliochaguliwa wakfu.

Mitume wanatakiwa kustahimili katika mateso na dhiki

Mathayo 10:5-15 inaorodhesha maagizo ambayo Yesu alitoa kwa wale kumi na wawili kabla ya kuwatuma, kisha katika **aya 16-26,** Yesu anawaonya kwamba mateso yanakuja. Katika **2 Wakorintho 11:23-28,** Paulo anaorodhesa mateso ambayo amestahimili kama mtume. Yesu anaonya katika **Luka 21:16** ***"nanyi mtasalitiwa na wazazi wenu, na ndugu zenu, na jamaa zenu, na rafiki zenu, nao watawavisha baadhi yenu".*** Maonyo haya yanarudiwa katika **Mariko 13:9-13**. Yesu alikuwa amekataliwa na kuteswa. Aliwaambia wanafunzi wake, ***"mtumwa si mkubwa kuliko Bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi"* (Yohana 15:20).** Mitume katika kanisa la kwanza waliyapitia mateso haya **Mdo 4:1-22.** Petro na Yohana walishikwa na kuwekwa gerezani, na wakaamuriwa kutokuhubiri kwa jina la Yesu. Paulo alitarajia mateso na akatamatisha katika **1Wakorintho 4:9** ***"maana na dhani ya kuwa Mungu ametutoa sisi mitume mwisho, kama watu waliohukumiwa wauwawe; kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu".*** Mateso yamehakikishwa lakini tabia bora inayohitajika ni uvumilivu. ***"Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tama; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi"* 2 Wakorintho 4:8-9.**

Mitume wana kushugulika na kubeba mzigo wa makanisa

***"Katika taabu na masubufu; katika kukesha mara nyimgi; katika njaa na kiu; katika kufunga mara nyingi; katika baridi na kuwa uchi. Bagahairi ya mambo ya nje, yako yanijiayo kila siku, ndio maangalizi ya makanisa yote"* 2 Wakorintho 11:27-28.** Paulo anasema mzigo wake mkubwa sio mambo mazito ambayo alikuwa amepitia lakini ni mzigo wa makanisa. Mtume ni kama mzazi akiwaangalia watoto wake. Kwa barua zake ni dhahiri kwamba Paulo alibeba mzigo wa makanisa yote aliokuwa ameyatembelea. ***"Tazama, hii ni mara ya tatu ya mimi kuwa tayari kuja kwenu, wala sitawalemea. Maana sizitafuti vitu vyenu, bali nawatafuta ninyi; maana haiwapasi watoto kuweka akiba kwa wazazi, bali wazazi kwa watoto"* 2Wakorintho 12:14.** Akiwaandikia Wagalatia, Paulo alionyesha mzigo wake wa ndani kama baba kwao wakue mpaka ukomavu ***"vitoto vyangu ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu"* Wagalatia 4:19**

Mtume anapatiana vyote kwa watakatifu katika makanisa

Hii inafuatisha hatua iliyotangulia. Mtume Paulo anasema kwa Wakorintho katika **2Wakorintho 12:15***, "nami kwa furaha nyingi nitatapanya, tena nitatapanywa kwa ajili ya roho zenu. Je! Kadiri nizidivyo kuwapenda sana, ninapungukiwa kupendwa".* Hata kama Paulo alijihisi kana kwamba Wakorintho hawakufurahia yale ambayo alikuwa ametenda na alikuwa akiwatendea, maisha yake yalikuwa yametolewa kwa ajili yao. Mhuduma wa kweli wa

Kristo ameandalika kuteseka ili kwamba aweze kuhudumu kikamilifu katika mwili. Paulo anasema katika **Wakolosai 1:24** ***"sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajiri yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyo pungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake".***

Mtume anayafanya yote kwa ajili ya kujenga

"Mwadhani hata sasa ya kuwa tunajiudhuru kwenu! Mbele za Mungu twanena katika Kristo. Na hayo yote, wapenzi, ni kwa ajili ya kuwajenga ninyi" **2Wakorintho 12:19.** Kazi ya huduma ni "***kuujenga mwili wa Yesu Kristo"*** mpaka mwili ukue ufikie utimilifu (**Waefeso 4:12-16).** Mtume na wahuduma wote wa karama za huduma tano, wanatakiwa kujipatiana ***"kwa kazi ya huduma".*** Kazi ya huduma haijakamilika mpaka mwili wa Kristo umefikia ukomavu kama iliyofundishwa wazi katika aya hizi katika Waefeso. Kila kitu chatakiwa kufanywa kwa neno na matendo kwa kujenga kanisa, watu wa Mungu (**1Wathesalonike 5:11).**

Kristo anajionyesha kwa nguvu kwa huduma ya mtume

"kwa kuwa mnatafuta dalili ya Kristo, asemaye ndani yangu, ambaye si dhaifu kwenu, bali ana uweza ndani yenu" **2 Waakorintho 13:3.** Huduma ya mtume haswa ni kumwakilisha Kristo. Neema nyingi inapatikana kwa mtume kuwakilisha na kudhihirisha uhakika wa Kristo. Hata hivyo hii pia inahusisha mamlaka ambayo inapatikana katika hukumu kama ilivyokuwa katika **Mdo 5** na Anania na Safira. Paulo alisema kwamba alipenda kuhudumu ***"kwa upole na utaratibu wa Kristo"*** lakini pia alionyesha kwamba ikihitajika angekuwa na ujasiri katika Bwana dhidi ya wale waliomhukumu ***"kuenenda kwa jinsi ya mwili"*** **2 Wakorintho 10:1-2**, na ya kwamba ***"sitahurumia waliotenda dhambi"*** **2 Wakorintho 13:2.**

Mtume anaishi na kuhudumu kwa nguvu za Mungu

Paulo alijua alikuwa ategemee nguvu za Roho Mtakatifu. ***"Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima. Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa. Na nilikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi. Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za Nguvu, ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu bali katika nguvu za Mungu"*** **1Wakorintho 2:1-5.** Paulo alitegemea nguvu za Mungu zilizokuwa ndani yake,***"maana, alisulibiwa katika udhaifu, lakini anaishi kwa nguvu za Mungu. Maana sisi nasi tu dhaifu katika yeye; lakini tutaishi pamoja naye kwa uweza wa Mungu ulio kwenu"*** **2 Wakorintho 13:4**. Wale walioitwa kwa huduma ya mtume lazima wajue 'kifo cha nafsi zao' na wawe na ujuzi unaoendelea na unaokuwa wa nguvu za Mungu zikifanya kazi ndani yao na kupitia wao.

Mtume anajua neema, upendo na ushirika wa Mungu

Paulo anaweza kushiriki neema ya Bwana, upendo wa Mungu na ushirika wa Roho Mtakatifu na watakatifu (**2 Wakorintho 13:14).** Kwa maana mtume anajua udani wa uhusiano na Mungu katika Kristo, anaweza kuhudumu na, hivyo, kuwaleta watakatifu katika uhakika huo. Tunaelewa katika nyaraka za Paulo na Petro zinaanza na huduma ya "***neema kwenu na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo",*** na mara inamalizia kwa jambo linalofanana la huduma ya neema. Kwa miaka tumezimia kuruka aya za utangulizi kwa nyaraka ila hali pana huduma ya ajabu ya kupokezwa kutoka kwa mtume hadi kwa watakatifu ya neema

na amani. Zaidi, mtume anaweza kuleta watakatifu katika upendo wa ndani wa Mungu na kudhihirisha kutembea kwa ndani na Roho Mtakatifu.

Mtume anajua na kutumia siraha za vita

"Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; maana silaha za vita vyetu si za mwili, mbali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome; tukiangusha mawazo na kila kitu kilicho inuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira imapate kumtii Kristo; tena tukiwa tayari kupatiliza maasi yote, kutii kwenu kutakapo timia" **2wakorintho 10:3-6.** Mtume lazima awe na uweza kuonyesha, watakatifu mwenendo wa kumtii Kristo. Ni wakati tu kutii kwetu kutakapokamilika ambapo tunaweza kuadhibu kutotii kwote. Kuadhibu kwa kutotii ni kupitia usahihi na mahubiri ya neno yenye nguvu za Roho Mtakatifu na kuongoza maombi katika kweli na uhakika wa neno. Katika maandiko haya katika Wakorinto, Paulo haonyeshi vita vya kiroho katika maeneo ya mbinguni kinyume cha 'mamlaka na nguvu' lakini anaonyesha kufanywa upya kikamilifu mawazo kwa kuangusha mawazo, ubaguzi, maoni na maeneo ya kiburi cha ubinafsi ambacho kinatuzuia kutembea katika utiifu wa neno la Mungu.

Mitume hawatakikani kulinganishwa na kila mmoja, ama kujilinganisha na wengine

"Kwa kuwa hatuthubutu kujihesabu pamoja na baadhi yao wanaojisifu wenyewe wala kujilinganisha nao; mbali wao wenyewe wakijipima na nafsi zao na nafsi zao, na wakijilinganisha nafsi zao na nafsi zao, hawana akili" **2 Wakorintho 10:12.** Kila muhuduma wa kweli lazima awe na ufahamu wa kweli wa yeye ni nani ndani ya Kristo na ni nini wamechaguliwa kufanya. Kila muhudumu atakuwa wa kipekee katika huduma zao katika kutii mwito wa Kristo. Hakika, kila mtume na kila mtakatifu anastahili kuja kwa ujuzi wa, na kutembea katika, uwana. Ni neema hii ya kufanyika mwana ambayo inaleta usalama na ufahamu mwema wa kitambulisho cha mtu. Neema ya uwana inahusika na kutakuwa na usalama kwa miaka mingi.

Mitume wanajua maeneo ya huduma ambayo Mungu amewaamulia

"Lakini sisi hatutajisifu zaidi ya kadiri yetu; bali kwa kadiri ya kipimo tulichopimiwa na Mungu, yaani, kadiri ya kufika hata kwenu" **2Wakorintho 10:13.** Mwanzoni Yesu aliwatuma wale kumi na wawili kwa kondoo waliopotea wa Israeli, akiwaamuru ***"katika njia ya mataifa msiende, wala katika mji wowote wa wasamaria msiingie"*** **Mathayo 10:5-6.** Paulo alikuwa amechaguliwa kimsingi kuwaendea watu wa mataifa (**Wagalatia 2:8).** Wakati wa utendaji kazi wa huduma yake, kama Yesu, Paulo alikaza kuhubiri injili katika miji mingine. Siamini kwamba kuna 'mipaka' ya kitume kama vile wengine wanadai lakini kuna maeneo wazi ya huduma ambayo Bwana anawahagua mitume watumike ndani yake. Nimeelewa kwamba njia ya kitume ni kubaki mnyenyekevu na kuachia Bwana afunue na adhibitishe eneo la huduma.

Mitume wanawezesha injili wakienda nchi zilizo mbele

Paulo anajua ameitwa ***"kuihubiri injili katika nchi zilizo mbele kupita nchi zenu, tusijisifu katika kipimo cha mtu mwingine kwa mambo yaliyo kwisha kutengenezwa"*** **2 Wakorintho10:14-16**. Mtume ni mwanzilishi na ni lazima aruhusiwe kuongoza njia kwa himaya jipya za huduma. Mtume anatakiwa kutii amri ambayo Yesu alipeana katika **Mathayo 28:19-20, *na*** kutoa uongozi kwa kutimiza tume, "***mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi".***

Kwa wepesi kuhubiri injili kwa njia ya kiuinjilisti haitimizi tume kuu. Mtume wanawezesha kanisa la mtaa na wahuduma wake kufanya ‘wanafunzi’.

Mtume anaweza kutumika kufichua mitume wa uongo

Paulo alifanyiza mazoezi kubabanua huku ***“maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo”*** **2 Wakorintho 11: 13.** Yesu anapongeza ***“malaika wa kanisa liliko Efeso”,*** kwa kuwa ***“umewajaribu wale wajiitao mitume nao sio, ukawaona kuwa waongo”*** **Ufunuo 2:1-2**. Malaika wa Kanisa anaweza kuonekana kama ‘mjumbe’ [maana halisi ya malaika]. Ni ya kupendeza kwamba King James Bible inatafsiri neno la Kiyunani *apostolos* mara mbili katika biblia kama mjumbe (**2Wakorintho 8:23** na **Wafilipi 2:25).** Ina maana kwamba viongozi wa makanisa katika **ufunuo 2 na 3** wangekuwa mitume.

Kama ilivyo na noti ya sarafu, mtu hutambua noti bandia kwa kuwa na ufahamu wa noti halisi; hata hivyo, aliye mtume wa kweli anaweza kubabanua asiye. Makosa ambayo viongozi wengi wa wachungaji na maaskofu wanafanya ni kwamba, pasina kujua mitume wa kweli, wanawakataa mitume wote kama ni wa uongo.

Mtume anapata msaada wa kifedha kutoka kwa makanisa mengi

Mtume Paulo anaeleza kwamba alipokea mshahara kutoka kwa makanisa mengine ili aweze kuhubiri injili ‘bila malipo’ kwa kanisa la Korinto **(2Wakorintho 11-7-9**). Mitume wana haki ya kusaidiwa. Paulo anajadili wale wanahubiri injili, wanastahili kusaidiwa, vile vile kama na wanaotoa huduma wana haki ya kupokea ujira wao***. “Hamjui ya kuwa wale wazifanyazo kazi za hekaluni, hula katika vitu vya hekalu, na wale wahudumiao madhabahu, hua na fungu lao katika vitu vya madhabahu? Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio injili wapate liziki kwa hiyo injili”*** **(1Wakorintho 9-13-14).**

Katika kanisa la leo mapato ya kanisa fungu la kumi na matoleo inaonekana kuwa kwenye uthibiti wa mchungaji wa mtaa. Katika hali zingine, ni askofu muangalizi wa makanisa kadhaa anaye dhibiti pesa za makanisa yote. Katika hali zote mbili zinapungukiwa na muundo wa maandiko. Katika hali zote mbili hakuna sehemu ya mitume na wakati mitume wanarejeshwa, kuna pingamizi ya kutoa msaada wa fedha kwao. Mfano wa kanisa la kwanza ilikuwa ni kuleta pesa na kuziweka ***“chini ya miguu mitume”*** **Mdo 4:35**. Katika hali yangu, Mungu imeinua mahali pa msaada kupitia baadhi ya kanisa ya nyumbani na mashirika ambao wanasaidia huduma ya kitume iliyo SHILOH.

“Wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyo hitaji” **Mdo 4:35.** Kanisa la kwanza “walishiriki vitu vyote”. Wakati walitaka kupatiana vilivyo zidi walizileta kwa mitume na wakatafuta ushauri na uthibitisho wa uongozi jinsi ya kugawa zawadi. ***“Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo”*** **1Wakorintho 16:1.**

Bwana huwashikilia mitume wake

Paulo aliona kwamba kuna wale ambao walimuacha, ambao walitafuta kumdhuru na wale waliompinga. “Lakini Bwana alisimama nami akanitia nguvu, ili kwa kazi yangu ule ujumbe utangazwe kwa utimilifu, hata wasikie mataifa yote. Na nikaokolewa kutoka kinywa cha simba. Bwana ataniokoa na kila neno mbaya, na kunihifadhi hadi nifike ufalme wake mbinguni (**2Timotheo 4:17-18).** Wakati wa safari ya kitume ya kwanza ya Paulo, Yohana Mariko aliwaacha mitume akarudi kutoka kwa safari. Wakati ulipofika wa safari ya pili, na Barnaba

akataka kumchukua Yohana Mariko naye, Paulo alikataa. Hata hivyo, baadaye katika huduma ya Paulo, Mariko alikuwa mfanyi kazi na Paulo aliye heshimika. Katika Wakolosai Dema ni mfanyi kazi pamoja na Paulo **(4:14)** lakini katika **2Timotheo 4:10** amemuacha Paulo ***"akiupenda ulimwengu huu wa sasa".*** Nimeyapitia mambo kama haya na wafanyi kazi ambao wametuacha na, kwa shukrani, tumepata kuona wengine wakirejeshwa kwetu.

Mitume ni lazima wawe na nidhanu ya mwili

"Bali na utesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa" **1 Wakorintho 9:27.** Paulo pia anasema ***"mtu akighafirika katika kosa lo lote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe"*** **Wagalatia 6:1**. Mitume hujizuia katika mambo yote. ***"Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika"*** **1Wakorintho 9:25.** Wanastahili kuwa na kiasi***. "Tena msilewe kwa mvinyo, ambapo mna ufisadi; bali mjazwe Roho"*** **Waefeso 5:18.**

Mtume anatakiwa awe kiongozi ambaye anaweza kufuatwa na wengine

"Ndugu zangu, mnifuate mimi, mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi" **Wafili 3:17**. Paulo anasema 'fuata mfano wangu'. Mtume anatakiwa kuishi maisha ambayo ni mfano kwa wengine. Yeye lazima awe na uwezo wa kusema 'nifuate mimi kama vile ninamfuata Kristo'. Miaka kadha iliyopita katika shule yetu ya mafundisho niliombwa nipeane fundisho kuhusu uongozi. Sikuwa nimefanya hivyo mwanzo. Nilikuwa kwa semina za uongozi na nilikuwa nimeshangaa kuona mafundisho yalikuwa yamewekwa katika kanuni za kufaulu kwa kibiashara sio katika maandiko. Nikachukua sehemu na, kwa mara ya kwanza katika maisha yangu nikatambua kwamba ni lazima niweze kusema kwa viongozi: 'mnifuate kama vile ninamfuata Kristo!' Niliweza kishiriki hayo, kama yeyote alitaka kujua jinsi ya kuomba kikamilifu, ningewaonyesha jinsi ya kuomba; kama mtu angetaka kujua muundo wa maandiko wa kutoa fedha, ningewaonyesha kupitia kutoa kwangu; kama mtu angependa kujua jinsi ya kuhubiri, ningewafundisha; kama mtu akiamini ni lazima aende kwa mataifa ningewapeleka. Nikaelewa kwamba Mungu alikuwa amenileta mahali ambapo ningeongoza kwa mfano. Paulo anasema ***"basi, nawasihi mnifuate mimi"*** **(1Wakorintho 4:16).** Katika shule ya mataifa hivi karibuni, idadi ya viongozi ambao walikuja kutoka kwa mataifa walishuhudia hadharani kwa kujipatiana kwa kiwango cha juu na kujipatiana kulikoonekana katika maisha ya viongozi hapa SHILOH.

Maisha ya mtume ni lazima yawe mfano wa neema

"Ambaye katika yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani, kwa ajili ya jina lake" **Warumi 1:5.** Neema hupokelewa kupitia Yesu Kristo na neema ambayo inaachiliwa kupitia huduma ya mtume ambayo ndiyo alama ya mtume. Kila mmoja wetu amepokea neema lakini kuna neema ya mtume kutembea ndani yake na kuhudumia mwili. Maisha ya mtume inatakiwa kuonyesha neema iliyo pokelewa. Paulo anatangaza kwamba alipokea ***"habari ya uwakili wa neema ya Mungu niliyopewa"*** kuwajulisha ufunuo wa siri na ***"kuwahubiri mataifa utajiri wake Kristo usiopimika"*** **Waefeso 3:2-3, 8.**

Huduma ya mtume inaweza kuhusisha huduma zote tano

Huduma ya kitume iliyokomaa inaonyesha tabia zote za huduma zingine***. "Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; wengine kuwa wachungaji na waalimu"*** **Waefeso 4:11**. Paulo alionyesha kuchanga huko kwa huduma: ***"nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe muhubiri na mtume, nasema kweli, sisemi uongo, mwalimu wa mataifa katika imani na kweli"*** **1Timotheo 2:7.** Paulo alihubiri injili kama mwinjilisti; akafundisha neno na akahudumu kama mtume. Anasema haswa alikuwa amechaguliwa kwa huduma tatu. Tunajua kutoka kwa maandiko ya Paulo kwamba alikuwa na ufahamu mkubwa sana wa kinabii katika neno la Mungu na pia twaelewa kwamba alikuwa na moyo wa uchungaji wa wandugu waliokuwa wakifanya kazi karibu naye.

Tamati

Mtu anaposoma agano jipya, akitafuta kuelewa mitume ni akina nani na wanafanya nini, mmoja anapata maelezo mengi. Mengi ya mafundisho ya Yesu imeelekezwa kwa mitume. Maandiko mengi ya Paulo ni kushiriki kuhusu huduma ya mtume. Agano jipya limeandikwa na mitume ama na watendakazi pamoja naye wa karibu kama habari ya Luka. Kitabu cha Matendo ni matendo ya mitume.

Bwana Yesu, Kichwa cha kanisa anarejesha karama ya huduma ya mtume kanisani ulimwenguni kote. 'Kuwekwa kwa kanisa katika mpangilio' kwa mwisho inafanyika ili Bwana apate kuachilia ufifio wa siku za mwisho katika kila taifa. Mto wa Mungu utatiririka, lakini haitawezekana mpaka misingi imewekwa vizuri na kwa nguvu, kulingana na neno la Mungu na sio kulingana na utamaduni wa kidini. Wakati wale wanafunzi mia na ishirini walikutana katika chumba cha juu baada ya kupaa kwa Yesu mbinguni, biblia inasema***, "Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali"*** **Mdo 1:14.** Kutokana na maombi ya kujipatiana, Petro aliongozwa kubadirisha Yuda, Mtume aliyeasi ambaye alikuwa amejiua kwa wakati huu. Mara tu mitume wa msingi walipokuwa wemewekwa, kisha siku ya pentekosti ***"ilitimia kikamilifu!"*** Bwana alikuwa akiweka kanisa katika mpangilio kupokea kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kusiko kwa kawaida.

Na ni nani alikuwa akiwekwa katika mpangilio?
Mitume, huduma ya msingi katika kanisa.
Bwana anatuonyesha kwamba mitume
Wamewekwa kanisani;
Ndio wa kwanza! ***(1Wakorinto 12:28).***
Ndio huduma ya msingi ambayo
Wote wengine wanjengwa.
Mitume ni lazima wapokelewe,
Kwa maana wakati kanisa linampokea mtume
Wanampokea Yesu Masihi
Na kwa kumpokea yeye watampokea Baba Mungu!
Mathayo 10:40.

Sura ya Saba

FUNDISHO LA MITUME NI NINI?

Injili halisi kama zilivyoandikwa ni fundisho la mitume

Mtume wa kweli ni Yule ajaye kwa jina la Bwana, ambaye haji kwa njia ya dini, ambaye haji akiwakilisha sememu ya kanisa ama kikundi fulani lakini anakuja na moyo wa kweli wa Yesu kwa watu wake na kwa mwili wake. Kupitia mafundisho ya mitume, Yesu anafunuliwa.

Kunatakiwa kuwa na ingalawa vizazi vitatu vilivyo hamashishwa, walimu waliofundishwa wakifanya kazi katika mwili wa Kristo: mitume ambao wanatoa kwa wahuduma wengine; kisha wahuduma ambao wanafundisha na kutoa kwa watu waaminifu; watu waaminifu ambao wanafundisha wengine.

Kama tukifundisha kukamilika kwa kanisa, kuandalika kwa kanisa lenye utukufu, kama tukihubiri neema ya Mungu ili watu wastahimili katika dhiki na kuinuliwa ndani yake, kisha tutakuwa tukihubiri na kufundisha neno la Mungu kwa usahihi na kutangaza kusudi lote la Mungu.

Injili Nne

Mfano wa kwanza wa fundisho la mitume katika Agano Jipya ni ushuhuda wa waandishi wa injili nne. Mathayo na Yohana walikuwa ni mitume wa Mwana Kondoo na wanashiriki moja kwa moja ujuzi wao na Yesu. Ambapo hakuna ushahidi wa kutosha kana kwamba Luka na Mariko walikuwa mitume [pengine walikuwa] katika huduma ya kanisa, wote wawili walifanya kazi karibu sana na mitume kwa kipindi kirefu na wakapitisha fundisho na ushuhuda. Injili halisi, kama ilivyo andikwa kimsingi ni fundisho la kitume. Zinahusisha mafundisho halisi ya Bwana Yesu na ushuhuda wa matendo yake.

Injili ya Mariko

"Mwanzo wa injili ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu" Mariko 1:1. Injili ya Mariko ni ushuhuda tosha wa kushangaza wa maisha na huduma ya Bwana Yesu. Injili ni habari njema ambayo inahusisha ahadi ya wokovu na kutimizwa katika uhai,kifo, kufufuka na kupaa kwa Bwana Yesu Kristo.

Injili ya Yohana

Yohana aliandika injili yake kama shahidi wa kuona. Anatuambia ni kwa nini aliandika injili: ***"lakini hizi zimeandikwa; ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake"*** **Yohana 20:31.** Yohana aliandika injili hii ili watu wapate kuamini na kuokoka. Fundisho la mitume ni kuhubiri Yesu aliye Kristo (**Mdo 5:42)** kwa kusudi la wasikizaji waje kwa maarifa ya wokovu wa Mungu.

Injili ya Luka

Katika kutanguliza injili yake, Luka anapatiana ufahamu muhimu wa asili ya fundisho la kitume. Anaandika ***"kwa kuwa watu wengi wametia mikono kutunga kwa taratibu habari za mambo yale yalitimizwa katikati yetu, kama walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo, nimeona vyema mimi nami, kwa***

kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Thiofilo mtukufu, upate kujua hakika ya mambo yale uliyofundishwa" **Luka 1:1-4.**

Kuna mambo manne kwa aya hizi ambayo yanaeleza fundisho la kitume ni nini:

- **Kutunga kwa utaratibu**
  Fundisho la kitume, kama ilivyoelezwa katika injili ya Luka, ni kutunga kwa utaratibu wazi (hadithi) ya maisha, fundisho na huduma ya Bwana Yesu.
- **Imepatianwa na mashahidi wenye kuyaona**
  Injili ilifikiswa na mashahidi wenye kuyaona [mitume wa Mwana Kondoo] na wahuduma wa neno [mitume ambao walikuwa naye, ikihusisha pia mitume waliopatikana baada ya kupaa kwake].
- **Usahihi wa mambo**
  Luka amepata usahihi wa mambo kutoka kwa ushuhuda wa mitume. Kumbuka, Luka ni mtu wa mataifa aliyefanyika mwanafunzi wa Paulo miaka kadha baada ya kufa na kufufuka kwa Yesu.
- **Kujua hakika ya mambo haya**
  Baada ya kuagizwa, Luka anaweza kuandika kwa taratibu ili mwingine 'ajue uhakika wa mambo hayo' ambayo Luka amepata kujua kutokana na kupokea fundisho la kitume.

Katika **1Yohana 1:1-4,** Yohana anaongea kwa njia iliyo sawa na hiyo: ushuhuda wa Yesu unashirikiwa na mitume, mashahidi walioona na wahuduma wa neno, ili kwamba sisi, wasikizaji, tupate kufikia uzima wa milele ambao ni ushirika ***"na Baba na Mwana wake Yesu Kristo".***

Injili ya Mathayo

Injili ya Mathayo, miongoni mwa vitu vingine, inaonyesha kutimizwa kwa unabii wa Agano la Kale katika maisha na huduma ya Yesu Kristo. Utafsiri wa Agano la Kale ni mtazamo muhimu wa fundisho la kitume. Kitabu cha Waebrania kinaonyesha mtazamo huu wa fundisho la kitume kwa undani kama tafsiri kamili [ikionyesha kutimizwa] wa kivuli na mifano ya Agano la Kale. Kuelewa Waebrania mtu anatakiwa awe na ufahamu unaofanya kazi vyema wa Agano la Kale.

Yesu hakuja kutangua sheria, lakini kuitimiza. Alitangaza ya kwamba sheria itatimizwa. Yesu anataka tufundishe neno la Mungu kutoka Agano la Kale kiunabii.

Fundisho la kitume inawapatia watu wa Mungu ufahamu wa sheria na amri,
ya manabii na nyaraka, kuwawezesha wote waone na wafahamu
kutimizwa kwake ndani ya Kristo
(Mathayo 5:17-19).

Tunahitaji kuwa na ufunuo wa Kristo na kanisa lake katika Agano la Kale ili tuweze kufundisha utimizo wa kinabii katika Agano Jipya***. "Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe"*** **Luka 24:27**. Yesu alidhibitisha kwa mitume wake ***"hayo ndiyo maneno Yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi. Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko"*** **Luka 24:44-45.**

Fundisho la kitume ni lazima lipitishwe

***"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakao faa kuwafundisha na wengine"* 2 Timotjeo 2:2**. Paulo anatupatia ufahamu unaofanana na huo wa vile fundisho la kitume linatakiwa kupokelewa na kupitishwa kwa wengine. Mtume, ambaye ni shahidi wa kuona [Paulo anasema alikuwa amemwona Bwana] na muhuduma wa neno [Petro alisema mitume ni lazima wajipatiane ***"Kwa huduma ya neno* Mdo 6:4]** anafundisha na kutayarisha wengine kuwa wahuduma [sio wote walio mitume; hii inahusisha huduma zote tano]. Wahuduma ambao wamepokea kutoka kwa mitume wanatakiwa kupitisha fundisho la mitume kwa watu waaminifu [hakuna mtu mume wala mtu mke] ambaye atawafundisha wengine. Kunatakikana kuwa na ingalao vizazi vitatu vilivyo hamashishwa, walimu walioandaliwa wakifanya kazi katika mwili wa Kristo:

- **Mitume** ambao wanafunza na kutoa kwa wahuduma wengine;
- **Wahuduma** ambao wanafunza na kutoa kwa watu waaminifu;
- **Watu waaminifu** ambao wanafundisha wengine.

Fundisho la mitume katika kitabu cha Matendo

"Wakawa wakidumu katika fudisho la mitume, na katika ushirika, na katika kumega mkate na katika kusali"* Mdo 2:42.** Mambo manne ambayo wallidummu ndani yake hakika ndizo ***'kazi za kwanza' za kanisa la kwanza. Katika **Ufunuo 2**, Yesu anaandikia kanisa lililoko katika Efeso na katika **aya 4** Ansema, ***"Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza".*** Katika **aya 5** anaendelea kusema, ***"Basi, kumbuka ni wapi ulianguka; ukatubu, ukafanye matendo ya kwanza. Lakini usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu".*** Kanisa hili lilikuwa limeuacha upendo wake wa kwanza na lilikuwa likiambiwa na Yesu lipate kutubu na kufanya kazi zake za kwanza tena. Ili tupate kujua kazi za kwanza zilikuwa zipi, twatakiwa kuangalia tabia za kanisa la kwanza.

Kanisa la kwanza lilihusisha wale waumini 120 [wakiwepo mitume 12 wa mwana kondoo], ambao Roho Mtakatifu alipata kushukia siku ya Pentekosti na watu 3000 ambao walikuwa wameamini na wakabatizwa siku hiyo. Waumini hawa walidumu katika mambo manne yaliyoorotheshwa katika **Mdo 2:42*:*** fundisho la mitume, ushirika, kumega mkate na maombi. Waliendelea katika ushirika wa fundisho la mitume, ushirika wa kumega mkate pamoja, na ushirika wa maombi ya pamoja; walipodumu katika ushirika, kulikuwa na 'kujali na kushirikiana' kwa njia kuu miongoni mwa waumini **(Mdo 2:44-45).**

Kama tutaendelea kudumu katika mambo haya manne, matokeo ya kuendelea yatakuwa kwamba tutakuwa na upendo na Yesu na hatutapoteza upendo huo. Utaongezeka kila mara tunaposhiriki meza ya Bwana; kila mara tunapokuja pamoja kwa maombi na kuabudu; kila mara tunapokutanika kwa ushirika uliojaa imani, ambao unajali na kushiriki, ukijali mahitaji ya kila mmoja, na kila mara tunaposhiriki fundisho la mitume, ambayo ni mafundisho ya neno la Mungu [fundisho ambalo limepitishwa kikamilifu na mitume]. Aya hii haswa inasema ***"fundisho la mitume",*** sio tu fundisho la neno. Neno la Mungu limekuwa limefundishwa kwa kiwango tangu wakati wa Matengenezo katika karne ya 16**,** lakini nadra kumekuwa na mtume wa kufundisha neno kwa karne za hapa karibuni. Kwa hivyo tunatakiwa kufahamu 'fundisho la mitume ni nini'?

Ufunuo unapatianwa kwa Mitume na Manabii

Kimsingi, Agano lote Jipya ni fundisho la mitume lakini ufunuo wa neno la Mungu inapeanwa haswa kwa mitume na manabii **(Waefeso 3:5).** Katika siku hizi, tunahitaji mitume wainuliwe

wakiwa na upako wa kufundisha neno. Maandiko yanaweza kufundishwa na wachungaji, waalimu na wainjilisti, lakini ufunuo mkubwa unapatianwa kwa mitume na manabii. Ni kwa uwakili spesheli wa neema ambapo mitume na manabii wanaweza kuleta ufahamu wa siri**.** ***"ikiwa mmesikia habari za uwakili wa neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu"*** **Waefeso 3:2.** Paulo, kama mtume, alikuwa amepokea uwakili wa neema. Utenda kazi wa neema hiyo ni katika **aya 4** ***"kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri Kristo***". Bwana mwenyewe huwafunulia mitume na manabii siri. [Siri hii pia inaonyeshwa katika **1Wakorintho 2:6-16 na Wakolosai 1:24-29].** Paulo alikuwa na ufahamu wa siri ya Kristo na alifundisha na akashiriki ufahamu huo. Kila mshirika wa mwili kisha anapokea neema kwa kupokea fundisho la kitume ***"siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine kama walivyo funuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho"*** **waefeso 3:5.** Siri hii ilikuwa haijafunuliwa Ibrahimu ama watu wengine wa Mungu katika Agano la Kale. Watu hawa wa Agano la kale hawawezi kuja katika utimilifu mpaka Yesu ainue kanisa lake **(Waebrania 11:40).**

Siri ni nini?

Siri ni umoja katika Kristo

"Ya kwamba mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya injili" **Waefeso 3:6.** Ni injili tu ambayo inaweza kuwaweka Wayahudi na watu wa Mataifa katika umoja **Waefeso 2:14-18.** Yesu ndiye amani Yetu na amefanya hawa wawili kuwa mmoja, akiumba mtu mmoja kutoka kwa wawili. Mungu anataka 'mtu mmoja mpaya'; yeye anaona tu mtu mmoja mpya! Ukuta wa kutenganisha umeondolewa.

Paulo anonyesha siri hii zaidi katika **Warumi 11** akiongea kuhusu mzaituni ambao unawawakilisha watu wa Mungu. Kuna mzaituni mmoja tu wa kweli. Mti wa kweli ulikua kupitia Mungu akichagua baba zetu, Ibrahimu, Isaaka na Yakobo. Mzizi ni Masihi, Yesu. Anasema ***"mimi ndimi niliyeshina na mzao wa Daudi"*** **Ufunuo 22:16.** Anasema ***"yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko"*** **Yohana 8:58**. Yesu pia alijitabulisha kama "***Mzabibu wa kweli"*** na washirika wa kanisa ndio matawi (**Yohana 15:1-8).** Huyu mtu mmoja mpya, mwili wa Kristo, mzaituni na mzabibu zote zinaongea kuhusu Agano Jipya ***"Israeli wa Mungu"*** **Wagalatia 6:16.**

Wakati Kristo alikuja katika mwili, ni mabaki tu ya Waisraeli walimpokea na kuingia katika haki ndani ya Kristo (**Warumi 11:5-7)**. Wengine walikatwa kama matawi yaliyokufa na mataifa waaminio wakawekwa kwenye mzaituni wa kweli kupitia imani (**aya 17).** Hata hivyo, Paulo anaendelea kutufunulia kwamba, kwa sababu ya "akina baba", Mungu atafanya kazi kubwa ya mwisho ya ukombozi miongoni mwa wale Israeli halisi ambao wamepofuka kwa injili kwa sababu ya kutoamini kwao (**aya 25-28).** Matokeo yatakuwa gani? Wayahudi na mataifa kwa furaha wakikua pamoja katika haki katika huo mti wa mzeituni mmoja!

Siri ni kanisa "bibi Arusi"

Katika **Waefeso 5:23-33**, Paulo anaelezea kuhusu siri ya kanisa bibi arusi katika hali ya ndoa na uhusiano katika ndoa kati ya mume na mke. Katika kutamatisha, anasema ***"Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa".*** Katika **Ufunuo 21:9-11**, Yohana anaonyeshwa katika Roho ***"Bibi – arusi, mke wa Mwana kondoo"***. Kanisa ni bibi arusi katika maandalizi ya ndoa na mke wa Mwana kondoo. Yesu mwenyewe ***"Analitakasa na kulisafisa kwa maji katika neno apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote***

kama hayo, bali liwe takatifu lisilo na mawaa" **Waefeso 5:26-27.** Kanisa hili ambalo yesu anaenda kujiletea litakuwa tukufu. Katika asili huwa tunajua kwamba bibi arusi atapatianwa kwa siku ya arusi yake jitihada zote zikifanywa za kumrembesha na ili kila kitu kitendeke kusababisha siku ya arusi iwe kamilifu iwezekanavyo.

Kanisa linatakiwa kuwa limeungamanishwa kikamilifu kwa Mungu: ***"lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye"*** **1Wakorintho 6:17**. Hii ni ndoa ya kiroho, kuunganishwa kikamilifu. Sisi ni ***"viungo vya mwili wake"*** **Waefeso 5:30**. Hivi ndivyo Adamu alivyosema alipomwona Hawa na akamwita 'mwanamke' **(Mwanzo 2:23).**

Siri ni neema ya Mungu

Paulo anasema alifanyika muhuduma ***"kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa kwa kadiri ya utendaji wa uweza wake"*** **Waefeso 3:7.** Matokeo ya neema hiyo ilikuwa ***"kuwahubiri mataifa utajiri wake Kristo usiopimika"*** **aya 8.** Mungu ***"ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele, na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile injili; ambayo kwa ajili ya hiyo naliwekwa niwe mhubiri na mtume na mwalimu"*** **2Timotheo 1:9-11**. Neema hii ilipeanwa kabla ya nyakati.

Siri ya neema ya Mungu ni kwamba Paulo, wa tohara, amechaguliwa kama mwalimu wa mataifa. Neema ndio nguvu za kuwezesha, ikiwezesha mapenzi yake kutendeka. (Ikimuwezesha Mfarisayo wa Wafarisayo kuwa mtume kwa watu wa mataifa)

Ushirika wa siri

Paulo anasema alipewa neema ***"kuwahubiri mataifa utajiri wake Kristo usiopimika; na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote"*** **Waefeso 3:9**. Kuna ushirika wa siri ambao Mungu anataka tuone na tujue. Neno la ushirika ni *koinonia* SC#2842 na, katika mazingira ya ushirika wa siri, inazungumzia ushirika wa ndani na Mungu na miongoni mwa wandugu ambao wameufikia ukomavu. Paulo anatuambia kwamba hekima ya ndani ya Mungu, siri, ni kwa waliokomaa **(1Wakorintho 2:6-7).** Ninaelewa kwamba kiwango hiki cha ukomavu ni cha neema ambapo Roho Wa Mungu anatuweka kama wana katika Kristo, katika uhusiano na Baba kama wana na katika uhusiano wa mmoja na mwingine ulio wa ndani kuliko lo lote ambalo tulilijua hapo mwanzo. Ukomavu ni kutembea huko na Mungu katika Kristo ambako tunaita uwana, ***"bali mlipokea roho ya kufanywa wana"*** **Warumi 8:15**. Tunashuhudia kwamba ushirika ambao tunafurahia kama wana pamoja una utajiri ni wa ndani na unatuleta katika ujuzi wakuwa tumeunganishwa pamoja katika mwili, tukitembea katika ufunuo wa undani na utele wa mwili wa Kristo.

Sehemu ingine ya ufunuo wa siri ni ***"kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumrisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia. Naam, katika yeye huyo"*** **Waefeso 1:10**. Hii inazungumzia kuja pamoja kwa watakatifu ambao wako mbinguni na Yesu na ambao wanakuja pamoja naye, na watakatifu walio takaswa duniani, walio tayari kwa kuja kwa Bwana **(1wathesalonika 4:13-17).** Utakuwa ushirika wa namna gani!

Kuhamisha mamlaka na nguvu

Paulo anasema matokeo ya kanisa kuja kujua ushirika wa siri ni ***"ili sasa kwa njia ya kanisa hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika***

ulimwengu wa roho" **Waefeso 3:10.** Wakati kanisa linakuja katika ushirika wa siri (hekima ya ndani) kisha hekima ya namna nyingi itafunuliwa. Aya hii inaonyesha kwamba kanisa limeundwa na Mungu ili linapofikia katika ufunuo wa kitume na kinabii, likitembea katika uwana, likitawala na kutamalaki katika Kristo, watakatifu watanena na kuhubiri kwa nguvu kwamba mamlaka na nguvu zitakosheshwa na injili itaanza kujaza anga.

Ufunuo wa siri, wa 'Kristo ni nani', unafunua kwamba Kristo alipofufuka katika wafu alifufuliwa na nguvu za Mungu ***"akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa Roho; juu sana kuliko ufalme wote na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote"*** **Waefeso 1:20-23**. Hii inamaanisha kwamba Mungu amefanya kanisa, ambalo ni mwili wake kichwa cha mambo yote katika Kristo. Huu ndio ufunuo kwamba mambo yote, hata enzi na mamlaka katika ulimwengu usioonekana, ziliumbwa na Mungu kupitia Yesu Kristo **(Wakolosai 1:16).** Watawala kama hao ***"wanabatilika"*** **(1 Wakorintho 2:6**) kwa sababu ya ufunuo wa siri, mafundisho ya hekima ya ndani.

Nguvu za kanisa, likitembea katika ufunuo ulio komaa wa siri na, hivyo wakihamisha mamlaka na nguvu, inaonyeshwa katika **Mdo 8** wakati Filipo alienda Samaria na akaanza kuhubiri katika mji ule. Alihubiri ufalme wa Mungu na jina la Yesu Kristo na ishara za kuu na maajabu zikatendeka kudhibitisha mahubiri. Waume kwa wake waliamini injili na wakabatizwa. Kupitia mahubiri ya Filipo hekima ya Mungu ya namna nyingi ilijulikana na mamlaka na nguvu katika mji wa Samaria hata mtu mwenye nguvu mkuu wa mji, Simioni mchawi, alitaka kutii injili na kubatizwa.

Siri ya kanisa 'likienenda katika utimilifu"

Kanisa limeitwa ***"kuenenda katika utimilifu"*** **(Waebrania 6:1).** Tayari tumeongea kuhusu kanisa hili katika utangulizi. Ni wakati tu kanisa linatembea katika ukomavu, likienenda katika utimilifu ya kwamba utukufu wa Mungu utaonekana kanisani.

"Ondoka, uangaze, kwa kuwa nuru yako imekuja, na utukufu wa BWANA umekuzukia" **Isaya 60:1.** Mungu anasema kwa watu wake, 'ondoka, uangaze kwa kuwa utukufu wa Bwana umekuzukia'. Hii ni ya wakati huu! Nuru, Yesu amekuja, na leo utukufu wa BWANA unawazukia watu wake. ***"Dunia yote imejaa utukufu wake"***, maserafi wamesema katika **Isaya 6:3**. Utukufu huu utafunuliwa (kujulikana) wakati kanisa linafanyika madhabahu ya Mungu duniani.

"Maana tazama, giza litaifunika dunia, na giza kuu litazifunika kabila za watu; bali BWANA atakuzukia wewe, na utukufu wake utaonekana juu yako" **Isaya 60:2**. Hii ndio tunapata duniani sasa; inaongezeka. Mnyama anainuka. Giza inatanda duniani kote, bali kanisa linainuka ndani yake, katika utukufu wake.

"Na mataifa wataijilia nuru yako, na wafalme kuujia kuja kwa kuzuka kwako. Inua macho yako utazame pande zote; wote wanakusanyana; wanakujia wewe; wana wako watakuja kutoka mbali. Na binti zako watabebwa nyongani. Ndipo utakapoona na kutiwa nuru, na moyo wako utatetemeka na kukujuka; kwa kuwa wingi wa bahari utageuzwa kukujia, utajiri wa mataifa utakuwasilia" **Isaya 60:3-5**. Huu ndio ufunuo wa siri kwamba, katika siku hizi za mwisho, mataifa wanamjia Bwana kwa idadi ya kuongezeka. Hii inatendeka kwa sababu wakati wa mataifa umekaribia kutimizwa.

"Makundi yote ya Kedari yatakusanyika kwako, kondoo waume wa Nebayothi watakutumikia; watapanda juu ya madhabahu yangu kwa kibali, nami nitaitukuza nyumba ya utukufu wangu" **Isaya 60:7.** Kedari na Nebayothi walikuwa wana wa kwanza wa Ishmaeli. Kiunabii inawezekana kuamini kwamba Waislamu wengi wataokolewa siku za mwisho. Viongozi na makundi yao wataokolewa na kuja katika ufalme wa Mungu. 'Watapanda kwa kibali katika madhabahu yangu'; madhabahu haya ni Yesu. Waislamu wengi watakuja kwa Yesu na atawakubali.

Mafundisho ya Msingi ya Kristo

Fundisho la mitume linaweka kanisa katika kanuni za msingi, ama mafundisho ya kwanza, ya Kristo. Mafundisho haya ya msingi yameorodheshwa kwetu katika **Webrania 6:1-2;** ni lazima iwekwe vyema kabla ya kanisa lienenda katika ukomavu. Mafundisho ya msingi lazima yafundishwe kwa kina kwa waumini wote katika njia hizi sita kabla ya watakatifu waweze kuelewa hekima ya ndani ambayo Mungu anataka watakatifu wote wapokee.

Kuzitubia kazi zisizo na uhai ni fundisho la msingi wa imani ya injili. Kutubu ni kubadilika. Toba ni lazima ihubiriwe **(Luka 24:47).** Kama watu wakitubu, dhambi zao zinaondolewa [kusamehewa].

Imani kwa Mungu inafuta toba. Wakati tunatubu tunageuka kutoka kwa kitu kutazama kitu; tunageuka kuacha dhambi, tunamgeukia Mungu kwa njia ya imani katika Kristo. Injili ya Yesu Kristo itahubiriwa ili watu waje kwa imani kwa Mungu kupitia Yeye.

Mafundisho ya mabatizo, iwapo ni katika wingi, ya msingi ni ubatizo wa maji kwa jina la Kristo, zoezi la mitume likifwatwa katika kitabu cha Matendo. Katika **Warumi 6,** Paulo anafundisha kuhusu fundisho la ubatizo. Petro anafundisha kuhusu ubatizo **1 Petro 3: 20-22.** Mitume wote wawili wanafundisha, kupitia ubatizo, muumini huinuliwa katika maisha ya kufufuka [kuketishwa maeneo ya mbinguni].

Kuwekea mikono kimsingi inahusu kupokea Roho Mtakatifu. Wakati Sauli [Paulo] aliokoka, mwanafunzi Anania alikuja akamwekea mikono. Sauli aliponywa na akapokea Roho Mtakatifu.

Kufufuliwa wafu inahusu kutembea kwetu katika nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo. Kuna vipengele vitatu muhimu vya fundisho hili: Yesu ki halisi alifufuka kutoka kwa wafu; kupitia kufufuka kwake tunapokea uzima wa milele [kuzaliwa upya]; tatu, kila nafsi itafufuka , wengine kwenye ufufuo wa wenye haki na wengine kwenye ufufuko wa hukumu **(Yohana 5:28-29).**

Hukumu ya milele ni fundisho la hali ya milele, kuelewa kwamba kuna dhawabu na hukumu na kuelewa kwamba kanisa itafikia katika mahali pa hukumu ya kweli katika Kristo!

Fundisho la mitume ni kufundisha kwa mitume

Hawa ndio wametumwa na kuchaguliwa na Kristo ili wawakilishe kikamilifu nguvu na mamlaka, hekima na maarifa hapa duniani leo. Ni karama iliopeanwa kwa wengine, na Kristo, kwa kanisa Lake (**Waefeso 4:11).** Katika **Mathayo 10:40,** Yesu anaongea katika mazingira ya kutuma na kuchagua kwa mitume Wake. Anasema ***"Awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenituma"*** Ni Baba aliye mtuma Yesu. Yesu anasema kwa

mitume, ambao kwa hakika wamechaguliwa na kutumwa na yeye, wamwakilishe kikamilifu. Katika enzi ya kanisa, mitume kama hao ndio wamepokea karama ya kupaa ya mtume, kutoka kwa Kristo Bwana aliyepaa, kulingana na **Waefeso 4:7-11**. Mtume wa kweli ni yule anayekuja kwa jina la Bwana, ambaye anakuja sio kwa dini, ambaye haji akiwakilisha kanisa lo lote ama kikundi fulani lakini ajaye na moyo wa kweli wa Yesu kwa watu Wake na kwa mwili Wake. Kupitia mafundisho ya mitume, Yesu anafunuliwa.

Katika **Mathayo 23:39,** Yesu anazungumza na Wayahudi wakati aliposema ***"Kwa maana nawaambia, hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, 'Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana"'.*** Kwa Wayahudi wa leo, hii inamaanisha kwamba hawatamwona Bwana mpaka watakaposema 'Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana'. Aliyekuja kwa jina la Bwana ni Yesu. Ni nani anaye kuja kwa jina la Bwana leo? Kwanza, mitume wake amabao amewatuma, na pili kanisa lake, mwili wake wa kitume, ambao ametuma kwa ulimwengu wote.

VIPENGELE VITANO VYA HUDUMA YA MTUME

Kuna vipengele maalum vya mafundisho katika Agano Jipya ambazo zinahimizwa kwa njia moja ama nyingine kwa makanisa mengi kwa njia fulani katika mafundisho yao. Hata hivyo, ni vingumu kupata kanisa likipitia vipengele hizi zote kwa njia ya kimaandiko. Baadhi ya vipengele hivyo ni: tume kuu, kujenga kanisa, kuwakamilisha watakatifu, kuinuna katika dhiki na kujiandaa kwa kuja kwa Bwana.

1. TUME KUU

Hubiri injili

Jambo wazi ambalo Yesu aliambia kanisa kufanya ni kuhubiri injili. ***"Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini amehukumiwa"*** **Mariko 16:15-16.** Kila mmoja aliyeumbwa na sura na mfano wa Mungu anahitaji kusikia injili; wengine wataamini na kuokoka na wengine hawataamini wakahukumiwa. Katika **Mathayo 24,** ambapo Yesu anaelezea ishara za siku za mwisho za kuja kwake, anasema ***"Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja"*** **aya 14.** Mojawapo wa ishara ambazo tunaweza kuangalia na, kutambua, hapo, tujue mwisho unakaribia ni uinjilisti duniani mwote. Miaka ya 1990 ilitangazwa kuwa miaka ya injili duniani mwote. Ukuaji mkubwa katika uinjilisti duniani mwote kwa miaka kumi na mitano iliyopita. Ukristo ndio imani ama dini iliyo na ukuaji wa haraka na zaidi, licha ya ukuaji wa Uislaam ambao vyombo vya utangazaji vinapatia umakini sana. Mara kwa mara Uislamu uko katika wachache wachace, lakini kwa sababu ya mfumo wa ulimwengu , wana ushawishi zaidi ya idadi yao. Kanisa ndilo jawabu ya Mungu kwa Ulimwengu na kanisa lake litainuka na malango ya kuzimu haitaweza kulishinda.

Hata kama uinjilisti umeenea, kama ilivyotajwa mahali pengine katika kitabu hiki, injili iliyohubiriwa ni injili ya wokovu ikiwa na mtazamo wa kwenda mbinguni.

Ni injili ya ufalme ambayo italeta
"wana wa ufalme" ambao wataurithi ufalme
*Wa Baba hapa duniani (**Mathayo 13:38, 43).***

Fanya wanafunzi

Tume kuu ambayo Yesu alitupa inaanza na kuhubiri kwa injili ili watu waokoke, lakini inakamilika tu kwa kufanya wanafunzi.

"***Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari"*** **Mathayo 28:18-20**. Tumeitwa tuenende, kwa mataifa yote, vikundi vyote vya watu, tukiwabatiza na kuwafundisha. Yesu aliahidi kuwa nasi hadi kazi ikamilike mwisho wa dahari. Watu ambao hawajafikiwa wanapokea injili sasa. Kumekuwa na kuharakishwa kwa kazi katika **miaka 10-15.** Ishara ya injili, katika **Mathayo 24:14,** inatimizwa kwa haraka sana. Bwana asifiwe!

Tunaambiwa katika **Mariko 16:16,** kwamba wengine watasikia ujumbe na waokoke, wengine hawatasikia wahukumiwe. Hawa ndio watakaohukumiwa wakati wa kuja kwa Bwana: ***"wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu"*** **2 Wathesalonike 1:8.** Inaonekana kutakuwa na wale ambao watakataa kumwamini Mungu hata kama wameusikia ujumbe na kutakuwa na wale ambao watasikia injili na wakatae kuitii.

Ahadi ya Roho Mtakatifu.

Funguo za kutimiza tume kuu ni Roho Mtakatifu ambaye Yesu aliahidi wanafunzi wake, ***"na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu"*** **Luka 24:49.** ***"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria na hata mwisho wa nchi"*** **Mdo 1:8.**

Katika **Zaburi 2:7-8,** mwandishi wa Zaburi aliandika kiunabii "***Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa. Uniombe nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako".*** Mataifa yameahidiwa Yesu kama urithi wake lakini sisi ni washiriki wa urithi huu***. "Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi kwa 'wazao', kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja kwa 'mzao wako', yaani Kristo". "Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi"*** **Wagalatia 3:16, 29.** Yesu ameahidiwa mataifa; Yesu ndiye mbegu ya Ibrahimu ambaye ahadi zilifanywa kwake na, kama sisi ni wa Kristo, sisi pia ni warithi kulingana na ahadi.

2. KULIJENGA KANISA

Katika miaka ya 1980 wenye ujuzi wa maumivu ya kukua kwa kanisa ambao walisema wanajua kuongeza idadi kwa kanisa la mtaa. Jambao la kudhania lilikuwa jambo muhimu tu kuhusu kanisa lilikuwa ni watu wangapi walihudhuria jengo na kumfanya muhuduma aonekane amaefaulu. Ushauri uliopeanwa kwa semina kwa kukua kwa kanisa ilihusisha kuwa na vibao katika maeneo ya kuegeza magari, jinsi ya kuwakilisha mtu wa maeneo ya kuegeza, jinsi ya kuwafundisha wakaribishaji, na kadhalika. Kujenga kanisa ni kuhusu kuwakuza wanafunzi ambao Mungu anapatiana kwa kila wazee (Katika Agano Jipya, uongozi wa kanisa ulikuwa ni katika wingi) lango la kukuza kanisa ni kuwaleta waumini katiaka ukomavu wakiisha andaliwa (Kukamilishwa) wafanye kazi katika mwili vyema.

Yesu alisema kwa Petro ***"wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda"*** **Mathayo 16:18.** Petro alikuwa mtume wa msingi ambaye aliwekwa na Yesu Kristo. Baadaye Petro anazungumzia ufunuo wake wa kuwa jiwe la msingi na kwamba kanisa (Hekalu) inajengwa na mawe yaliyo hai ***"Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililo kataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule lenye heshima. Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmenjengwa muwe nyumba ya Roho"*** **1Petro 2:4-5**. Yesu

alisema jambo kama hili kwa Petro, ‘wewe ni jiwe lililo hai na kwa sababu una imani ndani Yangu, nitakutumia kujenga kanisa langu’.

Yesu alisema atalijenga kanisa lake na ataenda kuwatumia mitume kama msingi. Ataenda pia kuwatumia manabii, wainjilisti, wachungaji, waalimu na kila huduma ingine yote na karama ambazo Roho Mtakatifu ataachilia tena kwa kanisa. Kanisa hili litapata ushindi dhidi ya kuzimu. Yesu alisema, ‘nakupa wewe, kanisa la kitume, funguo za ufalme wa Mungu’. Hizi ndizo funguo ambazo zinanenwa katika **Mathayo 16:19** ***“Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni”.***

Kristo alipeana vipawa kwa kulijenga kanisa

Vipawa hizi ni huduma tano zilizopeanwa na Kristo katika kupaa kwake. ***“Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu”*** **Waefeso 4:11.** Bona zilipatianwa? Kujenga kanisa: ‘kwa kuandaa (kukamilisha) watakatifu; kwa kufanya kazi ya huduma na kwa kuujenga mwili wa Kristo’ (**Efeso 4:12).** Kanisa linastahili kujengwa (na huduma tano) mpaka litakapoufikia ukomavu. Lengo ni ukamilifu. Kuna hali ya ukomavu ya kukua kama muumini binafsi na kuna hali ya ukomavu ya kukua kama kanisa, ***“hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo”*** **aya 13**. Kristo, kama Mwana, anajenga nyumba ya Mungu na ndiye kichwa juu ya nyumba, kanisa (**wabrania 3:3).**

3. KUWAKAMILISHA WATAKATIFU

Katika vikundi vingi vya kikristo katika mwingo ya hivi pumde kumekuwa hakuna ufahamu wa kuwakamilisha watakatifu ama uhitaji wake. Hii ni kwa sababu ya kuelewa vibaya maoni ya siku za mwisho na kwa sababu kumekuwa na kupokea kidogo kwa huduma tano za **Waefeso 4:11.** Ila hali maandiko yanasema kwamba kazi ya huduma ya karama hizi zilizopeanwa na Kristo ni kuwakamilisha watakatifu. Lengo la Mungu ni kuwe na ***“Mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo”*** **aya 13.** Kukamilishwa kwa watakatifu kutatimizwa aje? Kupitia huduma ikifanywa kufuatana na muundo uliowekwa na Bwana Yesu. Katika **Wakolosai 1:24-29,** Paulo anaongea kuhusu huduma ya kujipatiana kwa Kristo na mwili wake kama muhuduma. Je unakubali kuteseka kama muhuduma wa injili? Paulo anasema kwamba, kuwa muhuduma aliyefaulu, ni lazima uwe tayari kuteseka kwa kuwa hiyo ni ya muhimu kwa huduma iliyofaulu katika Kristo.

Kazi ya huduma.

Utimilifu huja kwa njia ya mateso. ***“Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena natatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani kanisa lake; ambalo nimefanywa muhudumu wake sasa na uwakili wake; niliopewa kwa faida yenu, nilitimize neno la Mungu”*** **Wakolosai 1:24:25.** Katika kazi ya muhuduma, kuna mateso mengi kwa anjili ya ‘mwili wake’ ambao ni kanisa. Lengo ni Kristo aumbike kikamilifu katika maisha ya watakatifu. Katika kuwaandikia watakatifu Galatia, Paulo anasema ***“vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu”*** **Wagalatia 4:19.** Sisi ni wahuduma kulingana ‘na uwakili kutoka kwa Mungu’, ambayo ni neema tuliopewa kufanya kazi ya huduma.

Kazi ya huduma ni kujulisha ***"Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake"*** **Wakolosai 1:26.** Kuna vizazi ambavyo siri zimesitirika. Bado hawajasikia injili; na hata wengi ambao wamesikia wamesikia kwa sehemu. Bwana anataka waumini wote wafundishwe na waelekezwe katika maarifa ya siri. ***"Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu"*** **Wakolosai 1:27.**

Kuwaleta Watakaifu Katika Utimilifu

Utukufu wa Bwana umetuzukia, sasa, leo. Tunahitaji kuliambia kanisa siri! Kama kwa uaminifu tukipatiana ujumbe wa injili, itatanda na kuongezeka. Kuzaliwa mara ya pili ni siri kwa wale ambao hawajaamini, lakinii injili ni zaidi ya kuzaliwa mara ya pili. Katika mazingira ya Wakolosai, Paulo anazungumzia kanisa. Hahubiri injili kwa waliopotea; anaonyesha waumini jinsi ya kuenenda. Mwisho huu Kristo hahubiriwi kwa wokovu tu lakini kwa kutukuzwa. ***"Ambaye sisi tunamhubiri habari zake, tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo. Nami najitaabisha kwa neno lilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu"*** **aya 28-29.** Ni uweza wa nguvu za Kristo ambayo unafanya kazi ndani mwetu kuleta watakatifu katika ukomavu ndani ya Kristo.

Tukaze mwendo…

Katika **Wafilipi 3:12-14,** Paulo anasema, ***"si kwamba nimekwisha kifika au nimekwisha kuwa; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikiwa na Kristo Yesu. Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mende ya dhawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu".*** Tunaenenda kwa utimilifu, kwa kukamata (kukumbatia) kile ambacho tumeitiwa kufanya. Tunatakiwa kusahau ambacho kiko nyuma na tukaze mwendo kwa mambo mapya ambayo Mungu anafanya. Kumbatia ufunuo wa kitume ambayo Mungu anafunua. ***"Basi sisi tulio wakamilifu natuwaze hayo"*** **Wafilipi 3:15.** Kuna makubaliano yanayo kuja miongoni mwa wandugu ambao wanapokea fundisho la kitume, ambao wanawapokea mitume ambao Kristo anawatuma. Huduma kubwa ya mitume leo ni kujulisha ufunuo wa siri na kuhudumu ufunuo huu kwa kuwakamilisha watakatifu.

4. KUINULIWA KATIKA DHIKI

Kila fundisho katika Agano jipya kuhusu dhiki inawaambia watakatifu kuinuka katika dhiki, kutukuzwa katika dhiki, kustahimili katika dhiki. Paulo anasema katika **Warumi 5:3-5** ***"wala si hivyo tu, ila natufurahi katika dhiki pia; tukijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya zaburi ni udhabiti wa moyo; na kazi ya udhabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliye pewa sisi".*** Kufurahia katika dhiki inawezekana tu kwa kusimama katika neema. Tunaingia katika kusimama huko katika neema kupitia imani katika Yesu Kristo.

Neno '*dhiki'* SC# 2347 inamaanisha 'msukumo' na inatafsiriwa:- kuteswa, mateso, uchungu, kulemewa, mateso, dhiki, shinda. Wakati tunasimama katika imani katika Kristo neema ya Mungu inaachiliwa kwetu. Wahubiri wengi na waumini wanaogopa dhiki na sababu ya kipekee ya kuogopa dhiki ni kwa sababu mtu hajui uthihirisho wa neema ya Mungu. Kipengele

muhimu cha ufunuo wa kitume ni uhakika wa neema inayoonekana ya Mungu ambayo inamwezesha mtu kusimama katika dhiki na katika mateso yote.

Paulo anaomba kujua ***"ushirika wa mateso yake"*** na kufananishwa ***"na kufa kwake"*** **Wafilipi 3:10.** Ni uhakika huu wa kukumbatia mateso, wa kukusudia kufa kwa nafsi kwa kila njia, ambayo inaachilia neema wa kuvumilia, kustahimili, na kushinda katikati mwa dhiki. Njoo kanisa! Natuhubiri na kufundisha neno la Mungu na sio fundisho ama ujumbe ambao kichwa chake hakimo katika neno la Mungu.

Bwana atakuja baada ya Dhiki

Kuja kwa Bwana ni katika dhiki kanisani kulingana na **2 Wathesalonika 1:4-7.** Paulo anawaambia Wathesalonike ambao walikuwa wakipitia dhiki na mateso kwamba Mungu atakabiliana na wale wanasababisha mateso wakati Bwana Yesu anafunuliwa kutoka mbinguni. Mungu atawapatia watakatifu ambao wanateseka pumziko wakati Bwana Yesu atakuja.

Watakatifu watateseka

Sura ya 2 ya Wathesalonike inaongea kuhusu ***"mwana wa upotevu".*** Yuda Isikalioti alikuwa ni mwana wa upotevu furani na alimsaliti Mwanawa Mungu mwenyewe. Katika siku za mwisho, kunakuja mwana wa upotevu mwingine mwenye nguvu zaidi ambaye atakuwa na ushawishi wa kupotosha duniani kupitia roho ya uasi na uasi –sheria ambao unakuja juu ya dunia; atalilenga haswa kanisa la kweli, akishapokea nguvu kupitia kanisa la uongo, kanisa ambalo limeghafilika. Ni kanisa la siku za mwisho ambalo litateseka kwa mda kwa sababu huyu asi ameruhusiwa kutawala na kugandaniza watakatifu. Hii imetabiriwa wazi katika **Danieli 7:21,** na **ufunuo 13:7.** Ukitazama vifungo hivyo viwili utaona kwamba watakatifu wanashindwa na utawala wa mnyama, lakini uhakika wa ajabu ni kwamba hatimaye ***"nao watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu; na majira yakawandia watakatifu waumiliki ufalme***"**Danieli 7:22.** Wakati huu tu wa majaribu inarejelewa katika **Ufunuo 13:7-10** itaonyesha ***"subira na imani ya watakatifu".***

Mathayo 24:13-28 inaongea kuhusu dhiki kuu ambayo itakaribisha Mwana wa Adamu**.** ***"Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka"* aya 13.** Tunatakiwa kuvumilia hadi mwisho, sio mpaka kunyakuliwa kuje kutunusuru, lakini ni hata Yesu aje ambaye atakabiliana na andui zetu. Yesu aliahidi kwamba atakuwa na kanisa hadi mwisho wa dahari (**Mathayo 28:20)** hivyo atawezesha kanisa kuhubiri injili kwa kila taifa mpaka mwisho uje (**Mathayo 24:14).** Dhiki kuu ya **aya 21** kwanza inarejelea kuzingirwa kwa Rumi na uharibifu wa Yerusalemu katika AD70. Hata hivyo, kwa sababu Bwana wetu anajibu maswali kuhusu uharibifu wa hekalu, vile vile wa mwisho wa dahari na kuja kwake, kuna sababu nzuri ya kuelewa dhiki ingine kuu itafanyika katika mwisho wa dahari. Lakini hata dhiki hii ya mwisho ni, katika mazingira, katikati mwa ***"Uyahudi"* aya 16.** Ni neema ya Mungu tu ambayo inawawezesha watakatifu kuvumilia dhiki. Hakika Mungu ***"atapunguza siku hizo kwa sababu ya wateule"* (aya 22).**

Ishara ya kuja kwake Mwana wa Adamu inakuja ***"mara tu baada ya dhiki ya siku hizo".*** Hiyo inamaanisha kwamba Yesu anakuja baada ya dhiki kuwakusanya wateule wake ***"kutoka pepo nne"* aya 29-31.** Watakatifu, wateule, wanapitia dhik. Watakatifu wa kweli wamefanya hivyo katika kila karne ya majira ya kanisa na hakuna majira spesheli kwa misho wa karne ***ya 20,*** na mwanzo wa ***21***. Ni wakati wa kanisa, haswa magharibi, kujikaza na kufanyika watakatifu halisi wa Mungu aliye juu.

5. KUANDAA KWA KURUDI KWA BWANA

Wengi wamefundishwa kujiandaa kwa sababu ya kunyakuliwa ambayo itawanusuru waumini kutoka dunia kabla ya dunia ipate dhiki kuu. Katika mazingira ya fundisho hili waumini wameambiwa wawe tayari, kwa hakika, hawajatayarishwa kwa kurudi kwa Bwana.

Kutakaswa na kusafishwa

Huwa tunajitayarisha kwa njia gani kwa kurudi kwa Bwana? Katika **Waefeso 5:22-32,** Paulo anatufundisha Kristo mwenyewe ndiye anayeliandaa kanisa lake ili tuwe tayari kwa kurudi kwake. ***"Kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa anjili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno"*** **aya 25-26.** Wakati neno la mungu limehubiriwa na kufundishwa, linatumiwa na Yesu kulisafisha kanisa. ***"Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia"*** **Yohana 15:3.** Shukuru Mungu kwa kila nafasi unayoipata ya kuhubiri ama kufundisha, lakini hakikisha kwamba unafundisha fundisho la mitume. Neno ambalo linanenwa linatakasa kanisa ili kanisa lipate kuhudhulishwa mbele ya Yesu, "***apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa"*** **aya 27.**

Tunajitayarisha kwa jinsi gani kwa kurudi kwa Bwana?
Kwa kutakasa na kusafisha kanisa,
Kupitia kufundisha neno,
Tukilileta liwe kanisa lenye utukufu, safi, mwili mkamilifu.

Kanisa ni bibi- arusi wa Yesu Kristo na linastahili kuangaliwa kama takatifu. Tukihubiri 'kunyakuliwa' ambayo italinusuru kanisa kutoka kwa dunia ya shinda, waumini wataweka imani yao kwa kunyakuliwa. Tulihubiri kukihubiri kukamilishwa kwa kanisa, kuandaliwa kwa bibi-arusi mwenye utukufu, tukihubiri neema ya kustahimili dhiki na kuinuliwa ndani yake **(Warumi *5:3-5),*** basi tutakuwa tunahubiri na kufundisha neno la Mungu kwa usahihi na kutangaza kusudi lote la Mungu. Waumini wataamini kile wamefundishwa, kwa sababu ***"imani huja kwa kusikia"*** **(Warumi 10:17).**

Kujitakasa wenyewe

"Wapenzi, sisi tu wama wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo. Na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu" **1Yohana 3: 2-3.** Tunapaswa kujitakasa; hivi ndivyo tunapaswa kujiandaa kwa kuja kwa Yesu. Mioyo yetu inatakaswa na Mungu kupitia imani (**Mdo 15:8-9).** Petro anasema tutakase nafsi zetu ***"kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki"*** **1Petro 1:22.** Yakobo anasema ***"Itakaseni mikono yenu enyi wenye dhambi na kuisafisha mioyo yenu"*** enyi wenye nia mbili (**Yakobo 4: 8).** Yesu mwenyewe ametutakasa kuwa watu wake spesheli***, "wale walio na juhudi katika matendo mema"*** **(Tito 2:14).**

Kuja kwa Bwana

Paulo anatupa habari zaidi kuhusu kule kuja kwa Bwana katika **1Wathesalonike 4:13-18** na pia **2Wathesalonike 1:3-12** na **sura ya 2.** Maandiko inatuambia kwamba ***"hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye"*** **1Wathesalonike 1:4-13-15.** Hili ndilo tumaini la ajabu ambalo Paulo anarejelea katika **1Wakorintho 15,** ya kuwa waumini ambao wamelala

katika imani watafufuka tena na, ufufuo huo itafanyika, wakati wa kuja kwa Bwana. Miili ya roho ya watakatifu ambao wamekufa wako na Yesu sasa (**2Wakorintho 5:8*),*** na watarudi katika dunia pamoja na yeye. Kisha kwa njia ya miujiza miili yao ya utukufu itafufuka kutoka dunia. Kutakuwa na kikudi cha watakatifu ***"sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani"*** **1Wathesalonike 4:17**. Maneno haya kuhusu kuja kwa Bwana ni ya kuleta faraja na kuhimiza (**aya 18).**

Kutukuzwa katika watakatifu wake! Kustajaabiwa katika wale wote waliosadiki!

Wakati ***"Bwana Yesu anafunuliwa kutoka mbinguni na malaika wenye uwezo***", atakuwepo "***Katika utukufu wa nguvu zake atakapokuja, katika siku hiyo kutukuzwa katika watakatifu wake na kustaajabiwa katikati ya wale wote walio sadiki"*** **2 Wathesalonika 1:7, 9, 10.** Kurejelewa kwa ***"watakatifu"*** na "***wale waaminio"*** inaonekana ikirejelea kwa vikundi viwili vya watu. Yesu atatukuzwa miongoni mwa watakatifu. Watakatifu ni wale watakao kuwa wamejiandaa na tayari kwa kuja kwake na ni wale ambao watanyakuliwa kukutana na Bwana hewani. Inaonekana kuna kikundi kingine kikubwa cha watu ambao wameamini lakini sio watakatifu.

Watakatifu ni wale wenye utakatifu;
wakati mtu ametengwa mara wametakaswa!
Ni watakatifu ambao watapokea miili ya utukufu wakati wa kuja kwa Bwana.

Kutakuwa na wengi kama inavyoonyeshwa na wale wanawali watano wapumbavu (Mathayo 25) ambao wanaamini katika Yesu lakini hawatakuwa tayari kwa kuja kwake lakini " watamstaajabu " wakati atakapo kuja. Nadhania kwamba ni waumini hawa wote ambao watakao mtamani Yesu atakapo kuja ambao wataingizwa katika utawala wa miaka elfu moja. Twajua kwamba wale ***"wasio mjua Mungu na wao wasio itii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake"*** **(2 Wathesalonike 1:8-9)**. Kwa hivyo wanaoabudu sanamu, wasio amini Mungu, na wale wasioitii injili hawataishi wakati wa kuja kwa Bwana.

Kuja kwa Bwana pia kutashugulikia ***"yule asi, ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake"*** **2 Wathesalonika 2:8.**

Wengi wanafundisha na kuamini kuna kuja mara mbili lakini **2 Wathesalonike 1na 2** inaonyesha wazi kukusanyika kwa watakatifu kukutana na Bwana hewani ni sawa na kuja kwa Bwana Yesu Kristo ambayo itamwangamiza yule asi.

Fundisho la mitume ni nini?

Ni mafundisho ya neno la Mungu ***2Timotheo 3:16.***

Ni kusudi kamili la Mungu ***Matendo 20:27****.*

Ni ufunuo wa siri ***Waefeso 3:3-5.***

Ni hekima ya Mungu ya ndani ***1Wakorinto 2:6-10.***

Ni Kristo aliyefunuliwa, ***Waefeso 4:17, Wafilipi 3:8-11.***

Ni kuendelea kuhubiri na kufundisha Yesu kama Masihi ***Matendo 5:42.***

Picha ya mwisho tuliyonayo ya mtume Paulo

katika kitabu cha ***Matendo 28:30-31*** *ni yake*

“akihubiri habari za ufalme wa Mungu,

na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo,

kwa ujasiri mwingi asikatazwe na mtu”.

Hitimisho

UFUNUO WA KITUME

Katika miaka kumi iliyopita, kumekuwa na kuenea kwa huduma ya kitume kanisani mwa Yesu Kristo ulimwenguni kote. Kutembea katika duka ya vitabu vya kikristo miaka kumi iliyopita na kuona nyenzo katika 'mitume leo' ilikuwa ni kama haiwezekani. Ingewezekana pawe na kitabu kimoja ama viwili. Mnamo mwaka wa 2006 kuna vitabu kadha zilizoandikwa na mitume ambazo zinaleta mwangaza na ufahamu wa huduma ya mitume na wanatangaza urejesho wa mitume leo. Lakini zaidi ya neno lililoandikwa,

Kuna mitume zaidi na zaidi wanaohudumu katika mataifa, na hii inaleta mabadiriko ya ndani kimuundo katika mfano wa kanisa na inaachilia fundisho la ndani la neno la Mungu,
Hivyo ni, ufunuo wa siri.

Kama Bwana anavyotuleta katika ufunuo wa kitume wa neno lake, tunakuja kujua mamlaka ya Kristo, na kupitia neno lake. Ni hekima ya ndani ya neno la Mungu ambalo hakika linatuleta katika utukufu wa Mungu (**1Wakorintho 2:7).** Kama tulivyoona katika sura ya pili, Yesu anatuombea kupokea utukufu wake ambao alikuwa nao na Baba kabla ya nyakati (**Yohana 17:22).**

Ni ufunuo wa utukufu wa Kristo ambao unatuleta
Katika umoja na ni katika umoja
ambapo tunakuja katika utimilifu.
Hakuna njia ingine!

Hivi karibuni nilishiriki kutoka **Yohana 17** katika mkutano wa kanisa la nyumbani na waumini waliokomaa wachache. Tulipomaliza mafundisho ya neno na kuingia katika maombi, sisi sote tulihisi utukufu wake kwa wingi: uzito wa utukufu wake ulituzukia na baadhi ya wandugu walibadilishwa; hawangeondoka lakini walipata kumuabudu Mungu katika Roho na kweli! Tulifahamu kwamba Mungu alikuwa akishuhudia kwa neno lake na alikuwa akitudhibitishia ya kuwa tunaingia katika kiwango kipya, kiwango cha tatu; ya kuwa tunaingia katika mwelekeo mwingine, mwelekeo wa tatu ambapo tumefunikwa kabisa na utukufu wake. Kama matokeo, tunaweza kuwa katika patakatifu sana na Baba na kudhihirisha utukufu wake ambao ni ***"Kristo ndani yetu".*** Hatua hiyo ingine ni kutembea katika utukufu **– *"na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza"* Warumi 8:30.**

Dunia yote itajazwa na utukufu wake
kama wana waliokomaa, ambaye uwepo wake unakaa
Amedhihilisha utukufu wake, wanaubeba huo utukufu
katika maeneo wanaofanyia kazi, sokoni,
manyumbani, katika kila mahali
"wakizaa na kuongezeka na kuijaza nchi" ***Mwanzo 1:28.***

Tuko katika kizazi hicho cha mabadiliko ya milenia, wakati huo wa mabadiliko wa kipindi kipya, kipindi kijacho (**Waefeso 1:21)**. Wengine wanahubiri kuhusu hii kama siku ya tatu!

Tunaingia katika awamu ya tatu
Ya kusudi la Mungu likitimizwa.
Tunatakiwa kusherehekea sikukuu ya tatu na kubwa!

Sikukuu za mabanda zimesahaulika katika historia ya kanisa na badala yake kukawa na Krismasi na mtazamo wa kutimizwa wa vitu vyote umepotea. Tangu ufufuo wa mvua ya mwisho 1948, Mungu amekuwa akirejesha kwa kanisa maarifa ya, na matarajio kwamba, sikukuu ya mabanda itatimizwa.

Mungu anatuita kuja katika patakatifu sana. Ni wakati tu tunafahamu kwamba Yesu, kama kuhani mkuu wa milele, ametimiza siku ya upatanisho na ameingia ndani ya pasia kama mtangulizi wetu (**Waebrania 6:19-20),** ya kwamba sasa tunaweza kusikia tarumbeta (neno la kiunabii la Mungu) akituita katika ufunuo kamili wa kitume, kuelewa ukubwa wa kile ambacho Yesu ametenda kwa kumwaga damu yake msalabani na kisha kupaingia patakatifu sana mbinguni juu kwa damu yake mwenyewe (**Waebrania 9:11,12, 24).** Hii inaonyesha kwamba dhambi zote zimesamehewa na kuondolewa daima ***"nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena"*** **Yeremia 31:34b**

Hii ni ahadi ya agano jipya ambayo imefungwa katika damu ya Yesu ili kila mara tujapo katika meza ya Bwana na tunashiriki katika damu ya Kristo (**1 Wakorintho 10:16),** tunatambua kuwa Yesu, kwa damu yake, amausamehe uovu wetu wote na Mungu hakumbuki dhambi yetu tena. Tumefikia siku ya upatanisho, tukijua kwamba ***"Alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu"*** **Waebrania 10:12.** Yesu ***"kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa"*** **Waebrania 10:14.**

Wakati wa wakamilifu umefika!
Kila kitu kimetendeka!
Ni wakati wa kanisa kurithi,
Kuja katika utimilifu wa mambo yote katika Kristo.

Hii inamaanisha kwamba ni wakati wa Mungu kukaa ndani ya watu wake, ***"mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake"*** **Yohana 14:23.** Neno '*makao'* katika aya hii ni sawa na neno la Kiyunani *Mansion* **Yohana 14:2.** Inamaanisha **'mahali pa kukaa'**, inamaanisha **'hema'**. Ni wakati wa kutimizwa kwa sikukuu ya mabada! Ni wakati wa kuja mahali patakatifu sana na kupata ujuzi wa utukufu wa Baba.

Ni wakati wa kujua mtu wa tatu katika uungu ambaye ndiye mtu wa kwanza katika uungu, ***"wa kwanza atakuwa wa mwisho***". Ni wakati wa kujua Baba! Na hii inafanyika kwa njia gani! Yesu alisema ***"wakiwapokea ninyi (mitume) wanipokea Mimi; na wakinipokea mimi wamempokea yule (Baba) aliyenituma".***

Ni ya muhimu mitume kurejeshwa leo!
Ni wakati wa ufunuo wa kitume!

Kiabatisho i - BARAZA LA KITUME

Kwa nini tunahitaji baraza za kitume

Kuzuia kuwa na dini zaidi

Ni wakati wa viongozi wa kitume kuunda baraza za wazee ambazo zitatoa uangalizi na uongozi kwa wahuduma, huduma na mashirika ambao wanataka kuwa sehemu ya kanisa la kitume kama ilivyoonyeshwa na muundo wa maandiko na ambayo inainuka kila mahali leo. Baraza kama hiyo itahusisha viongozi wa vikundi vya kitume mbali mbali na miili ya kitume na kinabii. Baraza zikiundwa sio mwanzo wa harakati mpya, dini ama mtandao lakini ni utendaji kazi wa kimaandiko ulio halisi.

Imani ya kitume inakua

Kama wengine walionyesha karibu siku za usoni, kutakuwa na kikundi kikubwa cha idadi ya watakatifu, wahuduma na ushirika wote wakiongozwa na wahuduma wakijiunga na imani ya kitume ambayo ni ***"Imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu"*** **Jude 3.**

Ili mitume wahesabike

Katika nyakati hizi, mitume mbali mbali na manabii wameinuliwa na vikundi vimekusanyika kwao ama makanisa yamepandwa na kiongozi wa kitume, ama mashirika na wahuduma wao wamekuja katika uhusiano na mtume. Hata hivyo, viongozi hao hawana sehemu ama baraza ambapo wanaweza kuhusiana kama wenzao na kutii katika uhusiano wa pande zote na kuwajibika kwa fundisho na vitendo. Kwa sababu ya haya, tatizo ikitokea, kiongozi anaweza kufanya kazi peke yake na kuwa nje ya utaratibu, ikisababisha migawanyiko ambayo haifai na uharibifu.

Kuzuia kiongozi kuwavuta wanafunizi

Hatari ingine ambayo inaenea ni kwa kiongozi binafsi mwenye ushawishi mkubwa kupitia utafsiri wake wa fundisho la kitume na huduma (ni wazi inafanyika kwa nabii na mwalimu). Tunahatarishwa kwa kiongozi na msisitizo mwingi unawekwa kwa wazo la kiongozi huyo na maamuzi ya mambo yote. Hii maaendeleo mabaya ambayo inapotosha kutoka kwa kumtazama Yesu na ukuu ambayo anatakiwa kupewa kwa mambo yote. Maendeleo kama hayo inaelekeza kwa kiongozi wa huduma fulani na wale ambao wanashika mafundisho yake na kuyatenda harakati iliyoainishwa, isiwe tena huduma ya kitume halali kwa mwili wa Kristo.

Suala la kufunika

Suala la mhimu kwa wahuduma wengi ni hilo la kufunika. Baraza la wazee liko wazi chini ya kifuniko cha Bwana Yesu Kristo. Hakika hakuna kifuniko kingine kwa kanisa. Yesu peke yake ndiye kichwa chetu sisi wote na hakabidhi uongozi, katika kanisa lake kwa mwanadamu yeyote. Kupitia uwasilishaji wa pande zote wa washirika wote, baraza inatoa uongozi kwa kila mshirika. Baraza la kitume ni kulingana na Muundo katika **Mdo 15.**

Baraza la Yerusalemu

Matendo 15:5 inaripoti shida kubwa ambayo ilikuwa imeinuka kanisani kwa sababu ***"baadhi ya madhehebu ya mafarisayo walioamini wakasimama wakisema, 'ni lazima kuwatahiri*** **(waumini kati ya watu wa mataifa)** ***na kuwaagiza kuishika torati ya Musa"'***

Aya 6 Mitume na wazee wakakusanyika ***"wapate kulifikiri neno hilo".*** Kulikuwa ma kikundi kikubwa katika baraza hilo, ***"umati"*****aya 12.**

Aya 7 ***"kulikuwa na hoja nyingi"***

Aya 12 Lakini baada ya Petro kuongea kuhusu ujuzi wake katika nyumba ya Kornelio (**Mdo 10**) na Paulo na Barnaba walikuwa waongee sasa, mkutano wote wakanyamaza na wakasikiliza. Wakati mitume, wakiwa na ukweli wa sasa wa kushiriki wanaongea, wanaamuru usikizaji wa kila mmoja.

Aya 15 Yakobo analeta baraza katika hitimisho sawa kwa kuleta neno lililohuishwa kutoka kwa maandiko: **imeandikwa!** Hatimaye maandiko yanasuruhisha hoja na hiyo inatakiwa kuwa mada yetu: maadiko pekee. Maandiko ndiyo tu mamlaka yetu katika imani na utendaji.

Aya 22 Angalia kumbukumbu ***"kwa kikudi chao".*** Wazo la kikundi cha kitume lina msingi wa maandiko.

Aya 25 Wakati baraza lilianza kwa hoja, walimalizia kwa kusema ***"sisi tumeona vyema, hali tumepatana kwa moyo mmoja"***. Kuwa katika moyo mmoja ndiyo lengo ambayo tunaweza kufikia tukiwa na mapenzi ya kushughulikia hoja kwa njia ya kibiblia na kuruhusu Roho Mtakatifu na neno la Mungu kuwa suluhisho, sio mapenzi ya kiongozi mwenye nguvu.

Aya 28 ***"kwa maana ilimpendeza Roho Mtakatifu na sisi"*** **Roho Mtakatifu ndiye kiongozi wa baraza la kitume.**

Aya 31 Mazao mema yalipatikana kutoka kwa baraza la Yerusalemu: wakati barua ilisomwa kule Antiokia ***"wakafurahi kwa ajili ya faraja ile".***

Baraza ndogo ya kitume

Katika **wagalatia 2: 1-10,** Paulo anaeleza kwenda kwake Yerusalemu wakiwa na Barnaba na Tito kwa makusudi kupeleka injili ambayo alikuwa akihubiri ***"katika mataifa"*****aya 2.** Alikutana na Yakobo, Petro na Yohana ***"wenye sifa kuwa ni nguzo"*** **aya 9.** Paulo, kama mtume mkuu na mtu ambaye alielewa wazi mwito na kutumwa na Bwana na ambaye alipokea ufunuo wa ajabu wa injili, alitaka kuwasiliana na mitume viongozi Yerualemu. Ilikuwa ni katika mkutano huu wa mitume ambapo ilionekana wazi kwamba Paulo alikuwa aende kwa watu wa mataifa naye Petro alikuwa haswa aongoze huduma ***"kwa waliotahiriwa"*** **aya 7-8.**

Elewa kwamba kulikuwa hakuna ngazi ya uongozi miongoni mwa mitume hawa. Hakukuwa na 'baba wa kiroho' wa wengine. Lakini walielewa kwamba **walikuwa wanatoshana na kwamba Baba wa wote ni mtume Yesu Kristo.**

Lengo ni UMOJA

Baraza ni mahali ambapo viongozi wa vikundi mbali mbali wanaweza kuja pamoja kwa sababu ya kujitolea katika kushiriki kwa kusudi lililopo. Lengo hili limeelezwa wazi katika **Waefeso 4:12-16,** haswa **aya 15b-16** "***na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo".***

Kila kikundi kinafuatilia maono ambayo Bwana amewapatia na kwa hivyo wanachangia katika mwili kwa kujenga mwili wote. Baraza linawezesha viongozi mbali mbali kuja katika mahali pa usalama na ulinzi, ambapo wanatambuliwa na kupokelewa.